# MUUNDO WA SENTENSI YA KIIGEMBE: MTAZAMO WA EKSIBAA

**FRED JOHN MUTWIRI**

**Tasnifu hii imewasilishwa katika Shule ya Mafuzu ili kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili ya Kiswahili.**

**CHUO KIKUU CHA CHUKA**

**SEPTEMBA, 2019**

## UNGAMO NA IDHINI

**Ungamo**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa kwa minajili ya Shahada au Stashahada katika chuo kikuu kingine.

Sahihi_______________________ Tarehe 11/9/2019

Mutwiri Fred John
AM12/19182/15

**Idhini**

Tasnifu hii imetahiniwa, ikapitishwa na kuwasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa Chuo Kikuu.

Sahihi_______________________ Tarehe 11/09/2019

Prof. John M. Kobia
Idara ya Fani.
Chuo Kikuu cha Chuka.

Sahihi_______________________ Tarehe 11/09/2019

Dkt. Allan Mugambi
Idara ya Fani.
Chuo Kikuu cha Chuka.

**HATILINZI**

©2019

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuigwa, kunakili, kurudufisha, kuhifadhi kwa mifumo ya kieletroniki au kutoa vipengele fulani kwa namna yoyote ile bila idhini kutoka kwa mwandishi na Chuo Kikuu cha Chuka.

## TABARUKU

Kazi hii naitabarukia mama yangu mpendwa Martha Kabiro.

## SHUKRANI

Kwanza, namshukuru Maulana  kwa kunijalia uwezo na hekima katika vitengo vyote vya masomo kuanzia Shule ya Msingi, Shule ya Upili, Chuo Kikuu hadi sasa kiwango cha uzamili. Pili, natoa shukrani kochokocho kwa wasimamizi wangu Prof. John M. Kobia na Dkt. Allan Mugambi kwa ushauri wenu murua ambao umekuwa mwangaza wangu katika kukamilisha utafiti huu. Kila wakati mlipoongea nami mlinitia shime na hamu ya kuendelea na safari iliyodhihirika kwangu kuwa ngumu. Asanteni sana.

Aidha, natoa shukurani kwa walimu wangu katika kozi zote kwa jumla ambazo ziliniwezesha na kunitia nguvu kuendelea na kazi hii. Hao ni Dkt. Allan Mugambi, Bw. Enock Matundura, Bw. Kimathi Muembu, Bw. Mutahi Miricho na Bw. Sebastian Mbogo. Pia, siwezi kuwasahau wanafunzi wenzangu; Mbungu, Hilda, Mbeere, Susan, Mwendwa, Mutegi, Faith, Magdaline, Langat na Irine kwa ushauri wenu ulionichochea kutia juhudi. Magdaline shukrani sana kwa kunijuza kila wakati kujikaza katika maisha ya kiakademia.

Aidha, shukrani kwa wote walioikosoa kazi hii,  Mungu awakirimu na hekima zaidi. Kwa mpenzi wangu Lenah, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Mabanati ya St. Lawrence, Bw. Mambo, Bw. Rutha na Mwiti shukrani sana kwa usaidizi wenu wa dhati, Mungu awarehemu. Mwisho, shukrani zangu zimwendee mamangu mzazi Martha Kabiro kwa kunielimisha licha ya baba kuaga dunia nikiwa mchanga. Wote walionisaidia kwa njia moja au nyingine, na sijaweza kuwataja, naomba radhi na kuwaombea Mwenyezi Mungu awabariki.

**IKISIRI**

Sintaksia ni taaluma inayojihusisha na uchambuzi wa miundo ya sentensi. Utafiti huu ulichanganua muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe katika taaluma ya sintaksia. Kati ya vipashio vinavyotumika katika taaluma ya kisintaksia ni kama vile, kirai na kishazi ambavyo ndivyo vijenzi vya sentensi. Kĩĩgembe huzungumzwa katika maeneo ya kiutawala ya Igembe ya Kati, Igembe Kaskazini na Igembe Kusini katika Kaunti ya Meru, Kenya. Mwauo wa Maandishi ulibainisha kuwa, hakuna utafiti uliofanywa kuhusu muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe kwa mtazamo wa Eksibaa. Malengo ya utafiti huu yalikuwa; kueleza miundo ya virai na kufafanua miundo ya vishazi vya sentensi ya Kĩĩgembe kwa mujibu wa Nadharia ya Eksibaa. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Eksibaa iliyoasisiwa na Chomsky. Nadharia hii hubainisha virai na kuonyesha mpangilio wa viambajengo mbalimbali katika kategoria ya sintaksia. Kwa hivyo, nadharia hii ilifaa utafiti huu kwa kufafanua aina za virai na mpangilio wa kategoria za viambajengo mbalimbali katika sentensi ya Kĩĩgembe. Katika Nadharia ya Eksibaa, kirai ni kipashio cha muundo chenye neno moja au zaidi lakini kisicho na muundo wa kikundi nomino na kikundi tenzi. Kwa hivyo, ilifaa katika kueleza vipashio vya sentensi ya Kĩĩgembe na kuchanganua muundo wake. Data ya utafiti huu ilikuwa sentensi za Kĩĩgembe ambazo mtafiti alizipata nyanjani na pia mtafiti kuzalisha mwenyewe kutokana na umilisi wake kama mzawa wa lahaja hii. Utafiti huu ulibainisha miundo tofauti ya sentensi za Kĩĩgembe na kubainisha sheria zinazotawala uunganishwaji wa vipashio vinavyojaliza sentensi ya Kĩĩgembe. Data ya utafiti huu ilikuwa sentensi za Kĩĩgembe mia na ishirini zilizotumika katika uchanganuzi wa utafiti huu, sentensi hizo zilijumuisha; sentensi sahili, sentensi ambatano na sentensi changamano. Kwa hivyo, kila aina ya sentensi ilichanganuliwa kwa sentensi arubaini. Katika awamu ya uchanganuzi wa data, utafiti huu ulichanganua miundo ya virai kama vile; virai nomino, virai vielezi, virai vivumishi, virai tenzi na virai vihusishi huku ikibainika kuwa kulingana na Nadharia ya Eksibaa, sentensi ya Kĩĩgembe ina miundo anuai ya virai vyake. Aidha, utafiti huu ulichanganua aina za vishazi kama vile vishazi tegemezi ambavyo huwakilishwa na vitambulisho vifuatavyo; *nkîthîrwa, nûntû bwa, rîrîa, kinya kwethîrwa, nî kenda* na *kethîrwa.* Vishazi huru na vishazi viambatani vimefafanuliwa miundo yake pia na kuonyesha jinsi kichwa humiliki viambajengo vingine ili kuunda sentensi mbalimbali. Viambajengo hivi viliweza kuchanganuliwa kwa lengo la kufanikisha muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe. Matokeo ya utafiti huu yalibainisha isimu miundo kwa kubainisha muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe. Pia, utafiti huu unaweza kusaidia lugha za Kibantu kufanyiwa utafiti zaidi kwani lahaja ya Kĩĩgembe inaweza kutoa mwanga kuhusu lugha za Kibantu. Aidha, ulisaidia kuhifadhi Kĩĩgembe katika maandishi.

## ABSTRACT

Syntax is the study of structures of a sentence. This study was based on analysis of Kĩĩgembe sentence structure. Phrases and clauses are among the constituents that are used in syntax in formation of sentence structures. The Kĩĩgembe dialect is mostly spoken in Igembe North, Igembe Central and Igembe South sub counties in Meru County Kenya. Literature review revealed that no research has been done in regard to Kĩĩgembe sentence structure analysis. The study was guided by the following objectives; to explain the structure of the Kĩĩgembe sentence phrases and their relationship in formation of Kĩĩgembe sentence and describe the structure of Kiigembe clauses used in formation of Kĩĩgembe sentence. The study was guided by the X-bar theory as advanced by Chomsky. The theory was relevant since it seeks to analyze the structure of phrases and relationship between constituents of the sentence structures. The X-bar theory guides in analysis of the Kĩĩgembe sentence phrases since, phrases in this theory are referred to as a word or group of words that function as a single unit in the syntax of the sentence, usually consisting of a head or central word and elaborating words. The Kĩĩgembe sentence was generated from field research and also from the researcher for being a native speaker of the dialect. The research analyzed the Kĩĩgembe sentence structure. This research aimed to keenly research, on Kĩĩgembe sentence since it had not been given a lot of attention especially on syntax. In addition, this study analyzed the connection of different phrases and showed the rules that govern them. The researcher used both research in the field and also his intuitive knowledge as a native speaker of the dialect to generate sentences which were analyzed. So the researcher was a resource person in generating of the sentences together with the researched data in the field which were the key data in this research. The data of this research was 120 sentences which comprised of Kĩĩgembe simple sentences, complex and compound sentences. Each type of sentence, that is, simple sentence, complex and compound sentence, were analyzed with 40 Kĩĩgembe sentences. The findings analyzed Kĩĩgembe phrases like; noun phrase, verb phrase, adjective phrase, adverb phrase and preposition phrase. It was found that, in accordance to X- bar theory, Kĩĩgembe sentence has several structures of it's phrases that are made up of different constituents. In addition, Kĩĩgembe has six identifiers of Kĩĩgembe dependent clauses, which are *nkîthîrwa, nûntû bwa, rîrîa, kinya kwethîrwa, nî kenda* and *kethîrwa.* Independent clauses has also been analyzed and found how the head of a phrase combines with other constituents of a sentence in making different Kĩĩgembe sentence structures. The findings of the study will contribute to structural linguistics and understanding of Bantu langauges since the research was based on structural analysis of Kĩĩgembe sentence. The research will also contribute to further study by scholars on Kĩĩgembe since this research will shed some light on Kibantu langauge. It also assisted in preservation of Kĩĩgembe in written work.

## YALIYOMO

**UNGAMO NA IDHINI.................................................................................... ii**

**HATILINZI ................................................................................................. iii**

**TABARUKU................................................................................................. iv**

**SHUKRANI ...................................................................................................v**

**IKISIRI ......................................................................................................... vi**

**ABSTRACT................................................................................................. vii**

**YALIYOMO................................................................................................ viii**

**MAELEZO YA ALAMA NA VIFUPISHO ...............................................x**

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI ......................................................1**

1.1 Usuli wa Mada ..........................................................................................1

1.2 Suala la Utafiti...........................................................................................5

1.3 Madhumuni ya Utafiti ...............................................................................5

1.4 Maswali ya Utafiti.......................................................................................5

1.5 Sababu ya Kuchagua Mada .......................................................................6

1.6 Upeo wa Utafiti ...........................................................................................6

1.7 Maelezo ya Istilahi .......................................................................................7

**SURA YA PILI: MWAUO WA MAANDISHI .........................................8**

2.1 Maandishi kuhusu Sentensi za Kibantu ....................................................8

2.2 Maandishi kuhusu Sentensi ya Kiswahili ..................................................11

2.3 Maandishi kuhusu Kiigembe.......................................................................19

2.4 Misingi ya Nadharia ...................................................................................21

2.5 Hitimisho.....................................................................................................33

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI ................................................34**

3.1 Eneo la Utafiti ............................................................................................34

3.2 Mpango wa Utafiti .....................................................................................34

3.3 Kundi Lengwa ............................................................................................34

3.4 Uteuzi wa Sampuli .....................................................................................35

3.5 Maadili ya Utafiti .......................................................................................35

3.6 Mbinu za Ukusanyaji Data.........................................................................36

3.7 Uwasilishaji wa Matokeo ........................................ 37

**SURA YA NNE: MIUNDO YA VIRAI VYA SENTENSI YA KIIGEMBE ........ 38**
4.1 Utangulizi ........................................ 38
4.2 Muundo wa Sentensi ya Kĩĩgembe ........................................ 38
4.2.1 Miundo ya Virai ........................................ 39
4.3 Hitimisho ........................................ 55

**SURA YA TANO: MIUNDO YA VISHAZI VYA SENTENSI YA KIIGEMBE ........................................ 56**
5.1 Utangulizi ........................................ 56
5.2 Miundo ya Vishazi ........................................ 56
5.2.1 Miundo ya Vishazi Tegemezi ........................................ 61
5.2.2 Miundo ya Vishazi Huru ........................................ 67
5.2.3 Miundo ya Vishazi Viambatani ........................................ 75
5.3 Hitimisho ........................................ 78

**SURA YA SITA: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI ........................................ 80**
6.1 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti ........................................ 80
6.2 Hitimisho ........................................ 82
6.3 Mapendekezo ya Utafiti wa Baadaye ........................................ 82

**MAREJELEO ........................................ 83**
**KIAMBATISHO I: TAKWIMU ZA TASNIFU ........................................ 86**
**KIAMBATISHO 2: SENTENSI YA KIIGEMBE ........................................ 87**
**KIAMBATISHO 3: KIBALI CHA UTAFITI ........................................ 95**
**KIAMBATISHO 4: BARUA YA KIBALI CHA UTAFITI ........................................ 96**
**KIAMBATISHO 5: RAMANI YA MAENEO TAWALA YA IGEMBE ............ 97**

# MAELEZO YA ALAMA NA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **E** | Kielezi |
| **H** | Kihusishi |
| **I** | Kihisishi |
| **KE** | Kirai Elezi |
| **KH** | Kirai Kihusishi |
| **KN** | Kikundi Nomino |
| **KT** | Kikundi kitenzi |
| **KV** | Kirai Kivumishi |
| **KZ** | Kishazi |
| **N** | Nomino |
| **RN** | Kirai nomino |
| **RT** | Kirai kitenzi |
| **Š** | Kishazi tegemezi |
| **S** | Sentensi |
| **T** | Kitenzi |
| **Ts** | Kitenzi kisaidizi |
| **U** | Kiunganishi |
| **V** | Kivumishi |
| **W** | Kiwakilishi |
| **X** | Kategoria ya maneno |
| **'** | Baa moja |
| **''** | Baa mbili |
| **Ɵ** | Kapa |

# SURA YA KWANZA
# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Kîîgembe ni lahaja mojawapo inayozungumzwa na Wameru. Aidha, ni lahaja ya Kibantu inayozungumzwa katika maeneo ya kiutawala ya Igembe Kusini, Igembe Kaskazini na Igembe ya Kati. Kwa mujibu wa Mukuthuria (1997), anasema kuwa, lugha ya Kîmerû imegawanywa katika makundi tisa. Maoni yake yanatiliwa mkazo na kazi ya Kobia (2008) anayesema kuwa, Kîmerû kina makundi tisa ambayo ni ; Waigembe, Watigania, Waimenti, Watharaka, Wamwimbi, Waigoji, Wamuutine, Wamuthambi na Wachuka. Makundi haya tisa yanayorejelewa na Kobia (keshatajwa) na Mukuthuria (keshatajwa) ndiyo hutumia lahaja tisa za Kimeru ambazo ni ; Kîîgembe, Kîtigania, Kîîmenti, Kîtharaka, Kîmwimbi, Kîîgoji, Kîmuutine, Kîmuthambi na Kîchuka. Kwa hivyo, Kîîgembe ni mojawapo ya lahaja zinazozungumzwa Meru, Kenya, na ambayo ni lahaja ya Kibantu.

Kîîgembe huzungumzwa na Waîgembe. Waîgembe wanaishi katika maeneo ya utawala ya Igembe ya Kati, Igembe Kaskazini na Igembe Kusini. Lahaja ya Kîîgembe ni mojawapo ya lahaja za Kimeru zilizotambuliwa na Guthrie (1948), aliposhughulikia lugha za Kibantu. Aidha, alitumia mbinu za kisayansi ili kuziainisha lugha za Kibantu. Guthrie (keshatajwa) alibainisha lugha za makundi ya lugha za Kibantu na kuziweka katika kikundi cha E51. Katika migao yake, kundi hili lilijumuisha; Kikuyu, Kiembu, Kimeru, Kitharaka, Kikamba na Kidhaiso cha Tanzania.

Lugha yoyote ya ulimwengu hudumisha maendeleo yake kupitia ufafanuzi unaowasilisha imani na tamaduni zake kimaandishi. Kîîgembe ni mojawapo ya lahaja ambayo ina udhaifu wa sifa hii kwa kuwa na hali hii ya kutofanyiwa utafiti katika kategoria mbalimbali. Maandishi ya Kîîgembe ni machache mno. Utafiti huu ulichanganua muundo wa sentensi ya Kîîgembe. (Mbaabu 1991)

Kîîgembe kimeshughulikiwa katika vitengo kama vile; fonolojia na mofolojia. Kazi ya Kanake (2013), ilishughulikia kitengo cha fonolojia ya Kîîgembe alipoainisha makosa wanayofanya wanafunzi wa Kîîgembe wanapojifunza lugha ya pili ya Kiswahili. Anaonyesha makosa kama vile, ya udondoshaji wa sauti na uchopekaji wa

sauti pasipofaa katika maneno ya Kiswahili kutokana na athari ya Kĩĩgembe. Anatoa mfano wa neno 'rudi' ambalo wanaliandika kama rundi* kwa kuchopeka /n/ na kwa hivyo kuonyesha jinsi ambavyo wanafunzi wa Kĩĩgembe wanavyofanya makosa wanapojifunza lugha ya pili. Taitumu (2014) alibainisha jinsi ambavyo maneno huundwa. Kwa mfano; uundaji wa maneno kutokana na kazi ya mtu. Mfano aliyoitoa ya Kĩĩgembe ni kama vile; *mûrîmî* kwa maana ya mkulima. Vilevile, anasema kuwa mifano ya maneno hayo inaweza kuzalishwa kupitia kuunganisha zaidi ya neno moja kwa mfano; *muwati wa mwana* yaani mlezi wa watoto.

Sentensi ni kipashio muhimu katika mawasiliano ya binadamu ulimwenguni. Kwa mujibu wa Massamba na wenzake (1999) sentensi ni utungo ulio na miundo ya KN na KT na yenye kutoa maana kamili. Massamba na wenzake (keshatajwa) hawa walifafanua sentensi kwa mujibu wa muundo wake na kwa kurejelea sentensi kama kundi la maneno. Kwa mfano;

S1 *Ntîî awîta ndukene* – Kĩĩgembe
Mama ameenda dukani- Kiswahili.

Katika mfano wa S1 *Ntîî* ni KN na *awîta ndukene* ni KT kinachoonyesha kile ntîî anachokifanya. Kwa hivyo, KT hutoa maelezo zaidi juu ya KN. Sentensi za Kĩĩgembe hubainisha dhahiri kwamba Kĩĩgembe ni lahaja ya Kimeru ambayo ni ya Kibantu kwani vipashio vyake kama vile vitenzi huishia kwa irabu */a/* . Kwa mfano, katika lugha ya Kĩĩgembe ambayo ni ya Kibantu.

*S2Mûrîmî nîakûrîma – Kĩĩgembe*
Mkulima analima - Kiswahili

Kulingana na Kapinga (1983), sentensi ni kipashio kikubwa kuliko vipashio vingine vya kiisimu na huwa na wazo kamili. Aghalabu, sentensi huwasilisha maana ambayo ni; taarifa, ombi, amri, mshangao au swali. Kwa hivyo, sentensi ni kipashio cha juu kabisa kikilinganishwa na vipashio vingine vya sintaksia kama vile; neno, kirai na kishazi na ambavyo huwa ni vijenzi vya sentensi. Kwa mfano, katika lugha ya Kiigembe;

Neno: *mûrîtwa – Kĩĩgembe*
mwanafunzi. – Kiswahili

Kirai: *mûrîtwa ûmûraya – Kĩĩgembe*

mwanafunzi mrefu - Kiswahili

Kishazi: *Mûrîtwa nîakwandîka –Kîîgembe*

Mwanafunzi anaandika - Kiswahili

Sentensi: S3 *Mûrîtwa ûmûraya nîakwandîka – Kîîgembe*

Mwanafunzi mrefu anaandika – Kiswahili

Sentensi katika Kîîgembe zinaweza kuwasilishwa kulingana na uamilifu wake. Kwa mfano, sentensi ya Kîîgembe inaweza kutokea kama ; amri, taarifa, swali, ombi na mshangao. Kwa mfano.

*Mûrîtwa ûmûraya nîakwandîka.* – Kîîgembe

Mwanafunzi mrefu anaandika - Kiswahili

*Mûrîtwa ûmûraya nîakwandîka*? – Kîîgembe

Mwanafunzi mrefu anaandika? - Kiswahili

*Mûrîtwa ûmûraya nîakwandîka*! – Kîîgembe

Mwanafunzi mrefu anaandika! - Kiswahili

*Mûrîtwa ûmûraya andîka*! – Kîîgembe

Mwanafunzi mrefu andika! - Kiswahili


Hata hivyo, kazi hii ilichanganua muundo wa sentensi za Kîîgembe bila kuzingatia uamilifu wake.

Obuchi na Mukhwana (2015), kwa upande mwingine, walifafanua sentensi kwa kusema kuwa, sentensi husheheni kishazi huru kimoja ambapo kishazi huru hicho ndicho huunda kundi nomino pamoja na kundi tenzi. Mfano wa sentensi ya Kîîgembe;

*S4 Mwaana ûû nî mwathîki –Kîîgembe*

Mtoto huyu ni mtiifu – Kiswahili

Mchoroto huu unathibitisha suala hilo.




Sentensi ya Kîîgembe inajitokeza kuwa na kishazi huru ambacho husheheni kikundi nomino na kikundi tenzi. Mfano wa S4 unadhihirisha kishazi huru na kishazi tegemezi jinsi ambavyo kimeelezwa kwa mchoro S4.

Rubanza (2003) anasema kuwa, sentensi ni sehemu ya sarufi, yenye KN na KT. Sentensi ndicho kipashio cha juu kabisa cha kisintaksia. Sintaksia ni taaluma inayojihusisha na uchambuzi wa miundo ya lugha. Vipashio vingine katika taaluma ya kisintaksia ni kirai na kishazi ambavyo ndivyo vijenzi vya sentensi ya Kîîgembe. Muundo wa msingi wa sentensi unahusisha virai anuai vinavyoshirikiana kama ilivyoelezwa na Chomsky (1957), kuwa sarufi geuzi ya awali inaanza na vipashio vya kisarufi ambavyo vinajumuisha kanuni muundo virai yaani, kanuni za sintaksia zitumiwazo kuchambua viambajengo vya sentensi.

Kwa mujibu wa Radford (1997), Anasema kuwa, sentensi ni kipashio kikubwa kuliko vipashio vya kiisimu na huwa na wazo lililokamilika. Sentensi ni sehemu ya sarufi ambayo aghalabu hujisimamia kimaana. Kwa hivyo, sentensi ni kipashio muhimu kwa kuwa husababisha kuwepo kwa mawasiliano, ambayo ni kiungo muhimu katika maisha ya binadamu kwa jumla. Anasema sentensi ni dhana asili ya lugha ambayo hufafanuliwa kudhihirisha sehemu ya sarufi yenye neno moja au zaidi inayosimamia wazo kamili. Aidha, sentensi ni sehemu ya sarufi ambayo hujisimamia kisintaksia na huwa na kiima na kiarifa ambacho kina kitenzi kimoja au zaidi. Kutokana na ufafanuzi huu, ni kweli kuwa, sentensi ni sehemu ya sarufi, yenye kikundi nomino na kikundi tenzi na vilevile husimamia wazo kamili. Kadhalika sentensi hudhihirisha

sehemu ya leksia yenye neno moja au hata zaidi. Zaidi ya hayo, sentensi huweza kufafanuliwa kwa kuzingatia muundo wake ambao huwa ni aina tofauti za sentensi. Aidha, sentensi pia hufafanuliwa kwa mujibu wa dhima yake kwa mfano, sentensi zinazodhihirisha ombi, swali, amri, mshangao na taarifa. Kwa hivyo, ufafanuzi huu wote umejikita kwenye miundo na uamilifu wa sentensi, hata hivyo utafiti huu umepiga hatua kwa kuangazia muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe kwa mujibu wa Nadharia ya Eksibaa.

## 1.2 Suala la Utafiti

Lugha hushughulikiwa katika viwango mbalimbali kama vile fonolojia, mofolojia na sintaksia. Kĩĩgembe kimeshughulikiwa katika viwango vya fonolojia na mofolojia lakini hakuna utafiti uliofanywa unaoshughulikia sintaksia ya Kĩĩgembe kwa kuangazia uchanganuzi wa muundo wa sentensi kwa mtazamo wa Nadharia ya Eksibaa. Muundo ni suala muhimu linaloshughulikiwa katika sintaksia. Kila lugha ulimwenguni, huwa na sentensi zenye muundo maalumu. Viambajengo vinavyounda sentensi haviunganishwi kiholela ila hufuata utaratibu fulani. Kadri ya mtafiti ajuavyo, sentensi ya Kĩĩgembe huwa na muundo maalum. Kwa hivyo, kila anayetumia lahaja ya Kĩĩgembe lazima aelewe miundo ya virai na vishazi na jinsi huwiana na viambajengo vingine vinavyounda sentensi ya Kĩĩgembe. Kulingana na ujuzi wa mtafiti, hakuna utafiti uliowahi kufanywa kuhusiana na muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe. Suala ambalo ni kiini cha utafiti huu.

## 1.3 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na madhumuni yafuatayo;

i. Kueleza miundo ya virai katika sentensi ya Kĩĩgembe.
ii. Kufafanua miundo ya vishazi katika sentensi ya Kĩĩgembe.

## 1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulitumia maswali ya utafiti yafuatayo;

i. Ni miundo gani ya virai inayojitokeza katika sentensi ya Kĩĩgembe?
ii. Je, sentensi ya Kĩĩgembe ina miundo gani ya vishazi?

## 1.5 Sababu ya Kuchagua Mada

Utafiti huu ulichangia kazi za isimu kwa kuchanganua muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe. Sentensi hushughulikiwa katika kiwango cha sintaksia. Kwa hivyo, kazi hii imekuwa nyongeza kwa kazi za kiisimu zitakazofanywa hapo baadaye. Utafiti huu pia ulichanganua viambajengo vya sentensi ya Kĩĩgembe kwa kurejelea mifano ya sentensi ya Kĩĩgembe yaani; sahili, ambatano na changamano. Kazi hii, pia ilifafanua lahaja ya Kĩĩgembe, kuiendeleza na kuhifadhi maandishi yake kwani hakuna uchunguzi ulikuwa umefanywa wa uchanganuzi wa muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe katika kiwango cha sintaksia. Aidha, kulingana na Mbaabu (1991), lugha yoyote ile duniani hudumisha maendeleo yake kupitia ufafanuzi wa kimaandishi. Utafiti huu umekuwa muhimu kwa watafiti wa baadaye wa Kĩĩgembe kwani umetoa mwanga kuhusu sentensi ya Kĩĩgembe kwa kuwawezesha kuelewa muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe. Utafiti huu ni wa manufaa katika uelewa wa muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe.

## 1.6 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu ulijihusisha na uchanganuzi wa muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe kwa msingi wa Nadharia ya Eksibaa. Utatifi huu, ulibainisha viambajengo vya sentensi ya Kĩĩgembe, kueleza miundo ya virai na kufafanua miundo ya vishazi ambavyo ni kati ya viambajengo vinavyounda sentensi ya Kĩĩgembe. Kazi hii ilijishughulisha na muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe bila kulinganisha na lugha nyingine yoyote ile au kushughulikia uamilifu wa sentensi. Utafiti huu ulijihusisha na sentensi za Kĩĩgembe zifuatazo; sentensi sahili, sentensi changamano na sentensi ambatano. Kwa hivyo, miundo ya vishazi na virai vya sentensi ya Kĩĩgembe tu ndivyo vilivyohusishwa. Data ya utafiti huu ilipatikana katika maeneo tawala ya Igembe Kusini, Igembe Kaskazini na Igembe ya Kati. Maeneo haya yana wazungumzaji asilia wa Kĩĩgembe.

## 1.7 Maelezo ya Istilahi

Katika utafiti huu, istilahi zifuatazo zilitumika kulingana na maana iliyodokezwa.

**Eksibaa:** Nadharia ambayo hutumika kuainisha muundo wa virai na kuonyesha uhusiano wa vipashio vya sentensi.

**Kiambajengo:** Kipashio kinachoshirikiana na vipashio vingine ili kuunda sentensi. Mifano; kirai na vishazi.

**Kichwa:** Neno kuu katika kirai.

**Kĩĩgembe:** Ni lahaja mojawapo inayozungumzwa na Wameru.

**Kirai:** Ni neno au fungu la maneno katika sentensi ya Kĩĩgembe lililo na maana lakini maana yake haijakamilika

**Kishazi:** Tungo lenye kikundi nomino na kikundi tenzi vilivyo ndani ya sentensi.

**Muundo:** Taratibu na kanuni za kisarufi zinazohusu uhusiano wa maneno uliopo katika kishazi, kirai au sentensi.

**Umilisi:** Ni hali ya kuwa na ujuzi au ueledi wa mfumo wa lahaja.

**Sentensi:** Kipashio cha tungo kikubwa zaidi cha Kĩĩgembe chenye muundo uliokamilika.

# SURA YA PILI

# MWAUO WA MAANDISHI

## 2.1 Maandishi kuhusu Sentensi za Kibantu

Kuna kazi ambazo zimefanywa kuhusu sentensi katika lugha tofauti za Kibantu. Guthrie (1948) alishugulikia lugha za Kibantu. Aidha, alitumia mbinu za kisayansi ili kuziainisha lugha za Kibantu. Guthrie (keshatajwa) alibainisha lugha za makundi ya lugha za Kibantu zinazopatikana mashariki mwa Kenya. Kikundi cha E51 katika migao yake, kundi hili lilijumuisha; Kikuyu, Kiembu, Kimeru, Kitharaka, Kikamba na Kidhaiso cha Tanzania. Aidha, Guthrie (keshatajwa) alieleza kuwa, nyingi za lugha hizi zina irabu saba yaani; /a/ /£/ /c/ /o/ /u/ /e/ /o/. Aidha, alishughulikia lugha hizi katika kiwango cha fonolojia. Kazi hii ilisaidia kwani lahaja ya Kĩĩgembe ni mojawapo ya lahaja za Kimeru zinazozungumzwa na wanajamii wa Meru. Aidha, kazi ya Guthrie (keshatajwa) ni msingi wa kazi ya Kibantu ambayo ilishughulikiwa katika utafiti huu. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti na kazi ya Guthrie (keshatajwa) kwani, ulishughulikia uchanganuzi wa muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe kwa kueleza miundo ya virai na kufafanua miundo ya vishazi vya sentensi ya Kĩĩgembe.

Kwa upande mwingine, Maringah (1987) alichunguza muundo wa kitenzi cha Kimbeere. Aliainisha vipashio mbalimbali vya kitenzi cha Kimbeere kama vile; nyakati, ngeli, mnyambuliko na virejeshi. Kazi yake ina umuhimu katika utafiti huu kwani, alishughulikia muundo wa kitenzi cha lugha ya Kibantu kama ilivyoshughulikiwa katika Kĩĩgembe. Kwa hivyo, kazi yake ilisaidia katika ujenzi wa historia ya lugha za Kibantu. Hata hivyo, kazi hii ni tofauti na ya Maringah (keshatajwa). Kwanza, utafiti huu ulishughulikia muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe. Pili, utafiti huu ulishughulikia viambajengo mbalimbali vya sentensi, kinyume na kazi yake iliyoshughulikia kitenzi tu.

Akijishughulisha na kulinganisha mifanyiko ya kimofolojia baina ya mnyambuliko wa kitenzi cha Kiswahili na cha Kikabarasi, Omusula (1998) alitambua kauli za mnyambuliko kama vile kutenda, kutendea, kutendesha na kutendeka miongoni mwa nyingine. Pia alitambua umuhimu wa viambishi katika kitenzi. Anasema kuwa kitenzi cha Kikabarasi kinaweza kuambishwa viambishi awali ambapo viambishi hivyo hubeba maana za kisarufi. Utafiti wa Omusula (keshatajwa) ulitoa mwelekeo kwa

utafiti huu. Kazi hii ni muhimu kwani  Kikabarasi ni lugha ya Kibantu kama ilivyo lahaja ya Kîîgembe. Hata hivyo, kazi hii ni tofauti na ya Omusula kwani ilishughulikia uchanganuzi wa muundo wa sentensi ya Kîîgembe. Kwa hivyo, utafiti huu ulipiga hatua kuelezea zaidi juu ya muundo wa sentensi ya Kîîgembe ambapo kitenzi ni kipashio kimojawapo kinachotumika kuunda sentensi. Viambajengo vingine vya Kîîgembe ni kama vile,  virai na vishazi.

Kwa mujibu wa Massamba na wenzake (1999)  lugha za Bantu hushabihiana kimuundo na kisifa. Aidha wanasema kuwa, lugha hizo huwa na mfuatano wa viambishi na mizizi.Viambishi hivyo huweza kutokea awali au baada ya mizizi. Kazi ya waandishi hawa imekuwa muhimu katika utafiti huu kwa sababu viambajengo vya sentensi vilivyotajwa na wataalam hawa ndivyo vimekuwa nguzo za utafiti huu kwa jumla. Mbali na hayo, dhana ya sentensi waliyoshughulikia ndiyo imetufaa mno katika kazi hii kwa kuwa imewezesha kubaini viambajengo vya sentensi na pia muundo wa sentensi ya Kîîgembe. Kadhalika, kazi yao imerahisisha utafiti huu kwa kuwa walifafanua muundo wa sentensi kwa jumla na pia kuangazia viambishi vinavyopachikwa kwenye mzizi. Aidha, ilisaidia katika kujenga msingi wa lugha za Kibantu kwani Kîîgembe ni lahaja ya Kibantu. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti kwani ulishughulika na kuchanganua muundo wa sentensi ya Kîîgembe kwa mujibu wa Nadharia ya Eksibaa. Aidha, Nadharia ya Eksibaa ilitumika kufafanua aina za virai na mpangilio wa kategoria za viambajengo mbalimbali vya sentensi.

Mukuthuria (2004) alitafiti kuathiriana kwa Kiswahili na Kimeru. Aligundua kuwa lugha ya Kiswahili na Kimeru ziliathiriana katika viwango vya fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Mchango wa utafiti wake ni kuwa ulishughulikia lugha ya Kimeru ambayo Kiigemmbe ni lahaja yake. Aidha, anasema kuwa athari ya lugha ya kwanza ambayo aghalabu huhusishwa na makosa na ambayo ni mojawapo ya athari za kisintaksia au sentensi ambayo utafiti unaangazia muundo wake. Hata hivyo, utafiti wetu uliegemea zaidi makosa katika ufundishaji lugha ya pili moja kwa moja wala haukueleza muundo wa sentensi.  Kazi hii ni muhimu kwa utafiti huu kwani lahaja ya Kîîgembe ni lahaja za Kimeru. Aidha, ilisaidia katika kujenga msingi wa lugha za Kibantu kwani Kimeru ni lahaja ya Kibantu. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti kwani ulishughulika na kuchanganua muundo wa sentensi ya Kîîgembe kwa mujibu wa

Nadharia ya Eksibaa. Aidha, Nadharia ya Eksibaa ilitumika kufafanua aina za virai na mpangilio wa kategoria za viambajengo mbalimbali vya sentensi.

Lugha ya Kichuka huwa na vipashio tofauti kuanzia cha chini hadi cha juu yaani, kipashio cha neno hadi sentensi (Mbaka, 2013). Mbaka (keshatajwa), katika kazi yake ya sarufi muundo wa virai vya Kichuka, anasema kuwa, virai mbalimbali hutumika kama viambajengo vya kuundia sentensi. Aidha, kulingana na Mbaka (keshatajwa), virai ni vipashio ambavyo huchanganuliwa katika kategoria ya sintaksia. Utafiti wake ulikuwa muhimu katika kazi hii kwani, virai alivyoshughulikia ni kati ya viambajengo vya sentensi ya Kĩĩgembe vilivyoshughulikiwa katika utafiti huu. Virai alivyoshughulikia ni kama vile virai nomino, virai vivumishi, virai vitenzi na virai vihusishi. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti na kazi yake, kwani ulishughulikia uchanganuzi wa muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe kwa misingi ya Nadharia ya Eksibaa.

Nyandago (2013) katika utafiti juu ya uchaguzi linganishi wa sintaksia ya sentensi sharti ya Kiswahili sanifu na Ekegusii. Utafiti ulionyesha kuwa kishazi sharti cha Kiswahili na Ekegusii vina uhusiano wa karibu sana. Alieleza kuwa vishazi hivi hujitokeza katika kategoria ya kielezi katika sentensi na kuendelea kufafaua kwamba kishazi sharti cha Kiswahili na Ekegusii vina uamilifu wa kielezi katika muundo wa sentensi. Vinatumika kama vipashio vielezi vinavyofafanua vishazi shurutia, vishazi hutoa maelezo ya hali ya matendo ambayo sharti yatimizwe kwanza, ndipo hali au matendo yanayotajwa na vishazi shurutia yaweze kufanyika. Utafiti wake ulikuwa muhimu katika kazi hii kwani, sentensi aliyoshughulikia ni kati ya sentensi za Kĩĩgembe itakayoshughulikiwa. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti na kazi yake, kwani ulishughulikia uchanganuzi wa muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe kwa misingi ya Nadharia ya Eksibaa.

Kwa mujibu wa Kirimi (2016), makosa ya kifonolojia na kimofolojia hujitokeza katika kazi andishi za wanafunzi wa shule za upili za Kitigania wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Anasema kuwa, uwasilishaji wa lugha ya kwanza hadi lugha ya pili ndicho kiini kikuu cha makosa ya kifonolojia na kimofolojia. Aidha, anasema kuwa makosa mengi hujitokeza katika kategoria ya vitenzi kuliko kategoria

nyingine kwani kitenzi ni kipashio cha lazima katika sentensi. Kitenzi ni kategoria ya lazima katika sentensi. Isitoshe, baadhi ya makosa yanayojitokeza katika insha huwa, ni kutokana na unazalishaji wa fonimu, udondoshaji wa sauti, uchopekaji wa irabu na utumiaji wa sauti mbadala. Kazi hii ni muhimu kwa utafiti huu kwani lahaja ya Kitigania inahusiana na Kĩĩgembe kwani zote ni lahaja za Kimeru. Aidha, ilisaidia katika kujenga msingi wa lugha za Kibantu kwani Kĩĩgembe ni lahaja ya Kibantu. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti kwani ulishughulika na kuchanganua muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe kwa mujibu wa Nadharia ya Eksibaa. Aidha, Nadharia ya Eksibaa ilitumika kufafanua aina za virai na mpangilio wa kategoria za viambajengo mbalimbali vya sentensi.

**2.2 Maandishi kuhusu Sentensi ya Kiswahili**

Chomsky (1957) aliwasilisha sintaksia mtazamo unaotambuliwa na Sarufi Geuza Maumbo Zalishi. Kazi hii ndiyo ilikuwa chanzo na asili ya sarufi zalishi. Alikusudia kukuza fafanuzi mwafaka za hali ya sintaksia ya lugha mbalimbali yaani jinsi lugha mahususi zinavyounganisha maneno kuunda sentensi. Vilevile, kazi hiyo ilidhamiria kukuza nadharia ya kijumla ya sintaksia inayobainisha ni mambo yapi ya kijumla ya masuala hayo na yanavyotofautiana katika uwanja huu wa sintaksia. Hii ndio kwa kawaida inaitwa Nadharia ya Sarufi Bia. Utafiti huu ulibainisha vishazi na virai vya sentensi ya Kĩĩgembe kuonyesha muundo wake.

Lyons (1968), anasema kuwa upatanishi wa nomino katika sentensi kwa kukubaliana na vipashio vingine vya sentensi. Aidha anamaanisha kuwa, nomino iliyo katika sentensi hukubaliana na viambajengo vingine katika tungo au matini husika. Katika kazi hii aliweza kugundua kuwa lugha ya Kiswahili huwa na ngeli za kimofolojia ambazo hutokana na dhana za: rangi, uhai, mguso na umbo zinazoambatanishwa na nomino mbalimbali. Aidha, anasema kuwa sentensi huwa na viambajengo viwili vya lazima: kikundi nomino na kikundi tenzi ila kikundi nomino kinaweza kuwa huria. Kwa hivyo sentensi zote lazima ziwe na kikundi tenzi . Mpangilio wa maneno katika sentensi ndio unaoleta muundo maalum wa sentensi na maana iliyokusudiwa. Uhusiano baina ya Kiswahili na Kĩĩgembe ni kuwa zote ni lugha za Kibantu. Kwa hivyo, uchunguzi wa Lyons kuhusu lugha ya Kiswahili ulitoa mwelekeo mwafaka katika uchanganuzi wa sentensi ya Kĩĩgembe.

Mkude (1983) anaeleza fasili ya vishazi na viambajengo vinavyounda virai mbalimbali. Virai hivi huunda vishazi mbalimbali ambavyo pia huunda sentensi. Kazi hii ni muhimu kwani utafiti huu ulibainisha aina za virai kama vile, virai vitenzi, virai vivumishi, virai nomino na virai vihusishi. Vilevile, vishazi alivyoshughulikia ni kati ya viambajengo vya sentensi ya Kĩĩgembe kwa hivyo, kazi hii ilikuwa ya muhimu katika utafiti huu kwa kueleza vipashio vya sentensi ya Kĩĩgembe. Nadharia ya Eksibaa ambayo ilitumika katika utafiti huu ni nadharia ambayo huchunguza aina za virai na mahusiano ya virai katika uundaji wa sentensi. Virai hivi, huweza kuunda vishazi na vishazi kuunda sentensi. Utafiti huu ni tofauti na kazi ya Mkude (keshatajwa) kwani ulipiga hatua kuainisha muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe.

Kwa mujibu wa Besha (1994), maarifa aliyonayo mjua lugha ni pamoja na kujua muundo sahihi wa sentensi za lugha yake. Sentensi ni tungo iliyo kamili kisarufi, isiyotegemea mazingira ya mawasiliano ili kueleweka kikamilifu. Sifa kuu za uchambuzi wa sentensi ni kubaini mfuatano wa maneno katika sentensi, uainishaji wa maneno katika makundi, kubaini uhusiano wa maneno yanayojenga sentensi, na kubaini uhusiano kati ya sentensi. Sentensi inaundwa na sehemu kuu mbili: kundi nomino na kundi tenzi. Maelezo ya muundo wa sentensi unaweza kujitokeza kwa namna ifuatavyo, Sentensi (S) - Kundi Nomino (KN) Kundi Tenzi (KT)

Wazo la Besha (1994) lilisaidia kubainisha vipashio vikuu vijengavyo sentensi ya Kĩĩgembe kama vile; virai nomino, virai vivumishi, virai vitenzi na virai vihusishi. Hata hivyo, vipashio hivi vikihusishwa na muundo wa sentensi vilijitokeza katika sentensi sahili, sentensi ambatano ambayo huwa ni sentensi sahili mbili na sentensi changamano. Kipashio cha kiisimu cha sintaksia kimekuwa muhimu katika kazi hii kwa kuwa kitengo hicho hushughulikia uchanganuzi, mpangilio na uhusiano wa vipashio vinavyounda sentensi. Dhana hiyo pia hushughulikia muundo wa sentensi na elementi zinazounda sentensi. Aidha, kitengo hiki huhakiki mpangilio wa maneno yanayounda sentensi na vilevile kusisitiza utaratibu mwafaka wa sheria za uundaji wa sentensi zenye maana.

Harly (1995) anasema kuwa ni kanuni ya kimsingi ya kila nadharia ya sarufi kuwa sentensi au kishazi lazima kiwe na kiambajengo ambacho kwa njia moja au nyingine

ni kikundi nomino. Katika kushughulikia kikundi nomino Harly amelipa suala hili mtazamo wa nafasi za kisintaksia ambapo viambajengo (KN) hivi hutokea katika sentensi. Hata hivyo, ni mwepesi wa kutaja kuwa nafasi hii si moja tu, kwa maana kuwa kuna nafasi kadhaa katika sentensi zinazoweza kutajwa kama nafasi za kikundi nomino. Anaeleza kuwakutegemea kigezo kinachotumika kuvitambulisha viima katika sentensi, kunaweza kuwa na viambajengo zaidi ya kimoja vinavyobainika kama kikundi nomino. Mchango mkubwa wa Harly kwa suala linalotafitiwa ni kuwa ametubainishia mbinu mbalimbali zinazoweza kutumika kubainisha muundo wa sentensi ya Kîîgembe katika lugha mbalimbali ulimwenguni. Anasema kikundi nomino cha sentensi kinaweza kufasiriwa kama kiambajengo cha sentensi ya Kîîgembe.

Massamba na wenzake (1999) waliainisha virai vya Kiswahili kama vile, kirai kivumishi, kirai kielezi, kirai nomino na kirai kihusishi. Katika kazi hii, walijihusisha na kanuni miundo virai iliyo katika Nadharia ya Sarufi Zalishi Geuza Maumbo (SZGM). Aidha, walieleza kuhusu viambajengo vya virai vya Kiswahili. Mbali na hayo, walionyesha tofauti iliyopo baina ya vishazi huru na vishazi tegemezi ambavyo vilirejelewa na sentensi changamano ya Kîîgembe. Kwa hivyo, utafiti huo ni muhimu kwa utafiti huu katika uchanganuzi muundo wa sentensi ya Kîîgembe kutokana na mwanga waliotoa katika utafiti wao. Isitoshe, utafiti huu ni tofauti kwani ulirejelea sentensi ya Kîîgembe kinyume na kazi yao iliyoshughulikia sentensi ya Kiswahili.

Kwa mujibu wa Massamba na wenzake (keshatajwa), sentensi ni kipashio kikubwa kabisa cha kimuundo ambacho kimekamilika kimaana. Mpangilio wa maneno katika sentensi unafanywa kwa utaratibu maalum kufuatwa na neno lingine ambalo lina uhusiano nalo. Miundo ya sentensi huhusisha vipashio vingine vidogo kimuundo. Vipashio hivyo ni virai na vishazi. Wanaendelea kusema kwamba muundo wa msingi wa sentensi huwa unahusisha virai tu, na hasa kirai Nomino na kirai kitenzi. Massamba na wenzake (keshatajwa) wamefasili kirai kuwa ni kipashio cha kimuundo chenye zaidi ya neno moja lakini ambacho hakina mahusiano ya kiima-kiarifu. Wazo hili liliupa utafiti huu dira kwani lilisaidia kubainisha viambajengo vya sentensi ya Kîîgembe. Hata hivyo, sentensi ya Kîîgembe inaweza kuundwa na kirai cha neno moja.

Kulingana na Massamba na wenzake (keshatajwa), wanasema kirai ni neno au fungu la maneno lililodokeza maana lakini maana hiyo si kamilifu. Haina muundo wa kikundi nomino na kikundi tenzi kama ule wa sentensi. Kinabeba tu sehemu ya sentensi. Kirai ni kipashio cha kisarufi kinachoundwa na neno moja au zaidi na hakina mwingiliano wa kimuundo wa kiima na kiarifa. Wanadai kuwa, kirai ni kipashio cha kimuundo chenye zaidi ya neno moja lakini ambacho hakina uhusiano wake si wa kuhusisha mtendaji wa tendo na tendo lililotendwa. Aidha, wanasema kirai ni mfuatano wowote wa maneno katika lugha yoyote na maneno yenyewe ni ya kategoria fulani. Kuna mfuatano wa maneno ulio mfupi kuliko sentensi lakini ni ndefu kuliko neno moja. Kwa hiyo kuna virai vilivyo virefu kuliko neno moja lakini fupi kuliko sentensi. Anaendelea kudai kuwa, sentensi pia ni ya kategoria fulani ya kirai kinachoitwa sentensi. Kirai pia kinaweza kuwa neno moja. Maelezo haya yalisaidia katika kubaini muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe kwani utafiti ulibainisha muundo wa viambajengo na mpangilio wa viambajengo ambalo ni lengo la utafiti huu. Aidha, utafiti huu ni tofauti na kazi yake kwani ulijikita kuchanganua muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe kwa kuainisha muundo wa vishazi na virai kwa kutumia nadharia ya Eksibaa.

Khamisi na Kiango (2002) wamebainisha elementi za muundo wa sentensi. Wametumia sarufi mapokeo kama mkabala wao wa kiuchambuzi. Elementi walizozitaja hapa ni kikundi nomino na kikundi tenzi. Kimsingi, hizi ni kazi zinazofanywa na vipashio vikubwa vinavyojenga sentensi, yaani virai na vishazi. Wanaeleza kuwa muundo wa msingi wa sentensi huhusisha kikundi nomino na kikundi tenzi ambapo virai hujitokeza kama vile, kirai nomino, kirai tenzi. Pia, Kirai Kivumishi, Kirai Kielezi na kirai kihusishi. Kuna miundo ya sentensi inayohusisha miundo kadhaa ya msingi iliyounganishwa kwa njia mbalimbali. Miundo hii huitwa vishazi. Utafiti huu ulihusu muundo wa sentensi. Kazi hii ni ya muhimu sana katika utafiti huu kwani iliupa msingi wa aina za sentensi. Hata hivyo, aina tatu za sentensi walizoshughulikia ni za Kiswahili. Utafiti huu ulipiga hatua kuainisha muundo wa sentensi sahili, ambatano na changamano katika Kĩĩgembe.

Kwa upande mwingine, Jerono (2003) aliainisha kishazi huru arifu katika Kiswahili kwa mtazamo wa Nadharia ya Eksibaa. Utafiti wake ulionyesha miundo ya virai

ambavyo hutumika kuunda kishazi huru arifu vikiwemo; virai nomino, virai vielezi, virai vitenzi na virai vivumishi. Jerono (keshatajwa) pia alitumia Nadharia ya Eksibaa katika utafiti wake. Kazi yake ni muhimu kwa utafiti huu kwa kuelewa Nadharia ya Eksibaa. Aidha, anaeleza kuwa Nadharia ya Eksibaa kuwa, ni nadharia ambayo hutumika kueleza miundo ya virai vya lugha zote. Kazi yake ni tofauti na utafiti huu, kwani Jerono (keshatajwa) aliangazia kishazi huru arifu cha Kiswahili ilhali utafiti huu uliangazia sentensi sahili, ambatano na changamano ya Kĩĩgembe zilizo na dhamira mbalimbali kama vile, arifu, ulizi, hisi na agizi. Kwa hivyo, utafiti huu ulipiga hatua kueleza zaidi muundo wa kishazi huru arifu ambacho ni kipashio katika muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe.

Sentensi ni utungo ulio na kikundi nomino na kikundi kitenzi. Kikundi nomino kinaweza kuwa kimedondoshwa kiasi cha kuonekana kana kwamba hakipo. Ukamilifu wa sentensi ni kuwa na maana kamili. Sentensi sio mkururo wa maneno yasiyokuwa na muundo maalumu. Sentensi huundwa na viambajengo vya daraja tofauti kama vile, neno, kirai na kishazi. Daraja hizo ni sauti ambazo husukwa kwa kanuni ya lugha husika na kuunda maneno. Maneno pia, kwa utaratibu wa lugha husika, yana kanuni ambayo hufuatwa katika kuyaunda na kuyafuatisha ili yaunde virai. Virai huunda vishazi ambavyo huunda sentensi (Rubanza, 2003). Wazo hili lilisaidia katika kuwasilisha lengo la utafiti huu kwani mtafiti aligawa sentensi katika kiwango cha kirai na kishazi ili kueleza muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe. Kazi ya Rubanza (keshatajwa) ni muhimu kwa utafiti huu kwani iliainisha sentensi za Kiswahili sanifu. Utafiti huu ulipiga hatua kuainisha sentensi za Kĩĩgembe kwa kurejelea sentensi sahili, ambatano na changamano.

Kwa upande mwingine, Habwe na Karanja (2004) waliainisha aina tatu za sentensi: sahili, changamano na ambatano. Aidha, wanasema kuwa, sentensi ambatano huundwa kwa mawazo mawili au zaidi na sentensi sahili huwa na wazo moja. Kulingana na maoni yao, sentensi ambatano ni sentensi ambayo inaweza kuundwa na sentensi mbili sahili au zaidi. Aidha, sentensi changamano ni sentensi ambayo huwa na kishazi huru kimoja au zaidi na kishazi tegemezi ambacho hakiwezi kujitegemea kuwasilisha maana ila hutegemea kishazi huru ili kukamilika kimaana.

Habwe na Karanja (keshatajwa), wanaeleza kuwa viambajengo vya kimsingi vya sentensi ni maneno. Maneno huweza kuunda viambajengo vya viwango vya juu kama virai na vishazi ambavyo ni vidogo kuliko sentensi. Kipashio cha kimsingi katika uchambuzi wa sentensi ni neno. Maneno tofauti hufanya kazi tofauti katika uundaji wa sentensi. Wazo hili ni muhimu kwa sababu limebainisha umuhimu wa neno katika uchambuzi wa sentensi kwamba bila maneno basi hapana sentensi. Hata hivyo, kusema kuwa neno ndiyo kipashio kidogo cha uchambuzi wa sentensi ni hoja ambayo haikubaliki kwa wanaisimu miundo kwani maneno pia yana miundo yake. Wamefafanua kategoria za kisarufi kuwa vipengele vya kisarufi vya viambajengo vinavyobainishwa ili vitumike katika uchambuzi wa kiisimu.Vipengele hivi husaidia kuonyesha mahusiano ya kategoria za maneno katika sentensi. Kwa mujibu wa Habwe na Karanja (2004) kuna kategoria za kisarufi za viambajengo mbalimbali ambazo huunda sentensi.

Njogu, Mwihaki na Buliba (2006) walifafanua sentensi sahili kwa kusema kuwa, sentensi sahili huwa na kishazi kimoja ambacho kinaweza kuwa, arifu, agizi, ombi au swali. Isitoshe, sentensi sahili huwasilisha wazo kamili bila kutegemea viambajengo vingine ili kutoa maana. Kulingana na Njogu, Mwihaki na Buliba (keshatajwa) sentensi sahili ni kipashio kilichokamilika kimaana. Sentensi sahili ya Kĩĩgembe ni mojawapo ya sentensi zilizoainishwa katika utafiti huu. Kwa jumla, utafiti huu ulibaini kuwa, kila sentensi hutambuliwa kupitia sifa yake ya kuwa kishazi kimoja au zaidi. Tofauti baina ya sentensi sahili kwa mfano, na sentensi ambatano ni kuwa sentensi sahili ina kishazi kimoja huku ambatano ikiwa na zaidi ya kishazi kimoja huru. Mfano katika sentensi ya Kĩĩgembe.

*S5 Nthaka înthongi nîkûrîma mundene- Kĩĩgembe (sahili)*

Ghulamu mtanashati analima shambani – Kiswahili (sahili)

*S6 Ntîî nîakurua irio akîthambia cûlia- Kĩĩgembe (ambatano)*

Mama anapika huku akiosha sufuria – Kiswahili (ambatano)

Katika mifano hii miwili ya sentensi sahili na ambatano ni kweli kuwa sentensi sahili imebeba wazo moja ambalo ni kulima huku sentensi ambatano ikiashiria mawazo mawili ambayo ni kupika na kuosha sufuria. Vilevile, kishazi huundwa kwa kirai nomino na kirai kitenzi kimoja. Kirai kitenzi ndicho kipashio cha lazima katika

sentensi. Vipashio katika muundo wa kishazi hujitokeza kwa utaratibu maalumu wa kuunda sentensi. Utaratibu na kaida za sintaksia ambazo zinafanikisha muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe ndizo zilizolengwa katika utafiti huu wa muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe.

Njogu, Mwihaki na Buliba (keshatajwa) wanasema kuwa, miundo ya sentensi huhusisha vipashio vidogo kimiundo. Vipashio hivyo ni neno, virai na vishazi. Muundo wa msingi wa sentensi huhusisha virai tu, na hasa kirai nomino na kirai tenzi. Pia, Kirai Kivumishi, Kirai Kielezi na kirai kihusishi. Kuna miundo ya sentensi inayohusisha miundo tofauti ya msingi iliyounganishwa kwa njia mbalimbali. Miundo hii huitwa vishazi. Maelezo haya yalisaidia katika kubaini muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe kwani utafiti ulibainisha muundo wa viambajengo na mpangilio wa viambajengo ambalo ni lengo la utafiti huu. Sentensi sahili kwa ilitambuliwa kuwa pamoja na kuwepo kwa kishazi kimoja na wazo moja katika sentensi sahili, kuna dhana ya ukumilifu. Hii ina maanisha kuwa sentensi sahili ni kamilifu isiyotegemea miundo mingine kujikamilisha kimaana na kimantiki.

Kwa jumla,tuliweza kufahamu kuwa kila sentensi hutambuliwa kupitia sifa yake ya kuwa na kishazi au vishazi. Tofauti baina ya sentensi moja na nyingine ni idadi ya vishazi vinavyoziunda. Aidha, kuna maafikiano ya jumla kuwa, kishazi kimeundwa kwa kirai nomino cha mtenda kimoja na kirai kitenzi kimoja. Vipashio katikamuundo wa kishazi havijitokezi tu kiholela ila kwa utaratibuwa kiupatanishi unaowezeza usarufi. Utaratibu huo ndio ualilengwa na utafiti huu kwa kuangazia upatanishi baina ya kirai nomino na vivumishi kwa upande mmoja na kirai nomino na vitenzi kwa upande mwingine katika sentensi ya Kichuka.

Massamba na wenzake (2009) wanaeleza kirai katika Kiswahili Sanifu kwa kuonyesha kuwa kirai huundwa kutokana na mahusiano maalumu baina ya maneno. Mahusiano huwa ni ya asili katika lugha na hujidhihirisha kisarufi. Muundo wa kirai hukitwa katika neno kuu katika lugha kama vile nomino, vitenzi, vivumishi, vielezi, na vihusishi. Maneno haya makuu huonyesha aina mbalimbali za virai. Kwa mfano, virai vya Kiswahili ni; Virai Nomino, Virai Vitenzi, Virai Vivumishi,Virai Vielezi na Virai Vihusishi. Kwa kuwa sentensi ya Kĩĩgembe huundwa na virai mbalimbali,

mawazo ya Massamba na wenzake (keshatajwa) ni mwongozo katika uchambuzi wa utafiti wa uchanganuzi wa sentensi ya Kîîgembe.

Kijenzi ni umbo lenye kazi mahususi za kisarufi katika sentensi. Kazi hiyo hutegemea nafasi kilipo kijenzi hicho katika muundo wa sentensi kama vile, kikundi nomino (KN) na kikundi tenzi (KT) (Khamis, 2011). Vijenzi alivyovitaja Khamis (keshatajwa) vinadhihirika ndani ya muundo wa sentensi ambayo ni kiini cha utafiti huu. Maoni yake ni muhimu kwani yalisaidia kubainisha vijenzi vya sentensi ya Kîîgembe. Utafiti huu, ni tofauti kwani ulichanganua muundo wa sentensi ya Kîîgembe.


Koech (2013) alichanganua miundo tofauti ya kijalizo cha Kiswahili huku akibainisha miundo ya kijalizo ambayo ni kirai nomino, kirai tenzi, kirai husishi na kirai elezi. Kazi yake ilikuwa muhimu katika utafiti huu kwani utafiti huu ulibainisha viambajengo vya sentensi ya Kîîgembe vikiwemo aina ya virai ambavyo utafiti huu ulishughulikia. Hata hivyo, utafiti wa muundo wa sentensi ya Kîîgembe ulipiga hatua zaidi kwa kubainisha viambajengo vingine kama vile, kirai na vishazi na miundo ya viambajengo hivyo.

Kila sentensi huundwa kwa sehemu za msingi mbili ambazo pia zinaweza kuwa na visehemu vyake vidogo. Sehemu kuu na ndogo za sentensi hujulikana kama viambajengo vya sentensi. Viambajengo vya sentensi ndivyo vinavyochangia muundo wa sentensi (Wesana-Chomi, 2017).

Mfano:

*S7 Mwarimû nîakûritana  bwea mûno- Kîîgembe*

Mwalimu anafunza  vizuri sana – Kiswahili



Sentensi hii ina sehemu mbili kuu ambazo ni kikundi nomino na kikundi tenzi ambazo zinaunda sentensi ya Kĩĩgembe.

Wesana-Chomi (2017) ameandika kuwa sentensi ni tungo iliyo na kifungu nomino na kifungu tenzi. Kifungu nomino kinaweza kuwa kimedondoshwa kiasi cha kuonekana kana kwamba hakipo. Ukamilifu wa sentensi ni kuwa na maana kamili. Sentensi sio mkururo wa maneno yasiyokuwa na muundo uliokamilika. Sentensi huundwa na viambajengo vya kategoria mbalimbali. Kategoria hizo ni sauti ambazo husukwa kwa kanuni ya lugha husika na kuunda maneno. Maneno pia kwa utaratibu wa lugha husika yana kanuni ambayo hufuatwa katika kuyaunda na kuyafuatisha ili yaunde virai. Virai huunda sentensi. Wazo hili lilitusaidia katika kuliendea lengo la utafiti huu kwani iliwezesha kuigawa sentensi katika kategoria za kirai na kishazi.

Massamba na wenzake (1999) wameifasili sentensi kuwa ni kundi la maneno lenye sehemu kuu mbili: kikundi nomino na kikundi tenzi na ambalo halitegemei au kujitegemeza kwenye kundi jingine la maneno ili kupata maana kamili. Pia, wametaja aina tatu za sentensi ambazo ni sentensi sahili, sentensi ambatani na sentensi changamano. Besha (1994) akishadidia kazi ya wataalamu hawa anasema kuwa sentensi ni tungo ya neno moja au kikundi cha maneno chenye kikundi nomino na kikundi tenzi pamoja na kuwa na maana au taarifa inayojitosheleza au maana iliyokamika. Sentensi ikikosa kikundi nomino na kikundi tenzi basi huwa ni tungo tu bali si sentensi. Kwa mujibu wa muundo wake wa kikategoria sentensi ni tungo iliyoundwa kwa kishazi kimoja au zaidi. Ufafanuzi huu wa sentensi ulisaidia katika kutambua miundo ya aina mbalimbali za sentensi za Kĩĩgembe. Hata hivyo, sentensi za lahaja ya Kĩĩgembe hakuzigusia hata kidogo katika kazi yake. Aidha, utafiti huu ni tofauti na kazi yake kwani ulijikita kuchanganua muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe kwa kuainisha muundo wa vishazi na virai kwa kutumia nadharia ya Eksibaa.

### 2.3 Maandishi kuhusu Kiigembe

Kanake (2013) alishughulikia makosa ya kifonolojia miongoni mwa wanafunzi wa Kĩĩgembe katika ujifunzaji wa Kiswahili. Aidha, anasema kuwa, makosa huweza kutokea kutokana na mwingiliano wa lugha hizi mbili. Utafiti wake unaonyesha kuwa, wanafunzi wa Kĩĩgembe wameathiriwa na lugha ya kwanza kwa njia zifuatazo;

Kwanza, ni udondoshaji wa sauti katika maneno ya Kiswahili kutokana na ukweli kuwa, Kiswahili kina konsonanti ishirini na tano huku Kîîgembe kikipungukiwa na konsonanti zingine kwa mfano; Kîîgembe hakina kipasuo kwamizo. Kwa mfano; konsonanti za Kîîgembe ni; /p/ /b/ /t//d/ /k/ /tʃ//ɟ//f//ð/s//z/ /ʃ/ /ɤ/ /h/ /m/ /n/ /ɲ/ /ŋ/ /l/ /c/ /nd/ /y/ /t/ /k/ /b/ /s/ /n/ /l/ /r/ /w/. Pili, wameathirika kwa uchopekaji wa sauti kwa mfano, neno 'rundi' badala ya 'rudi'. Vilevile, alitumia nadharia ya uchanganuzi linganuzi katika kazi yake ambayo ilitumika kulinganisha lugha mbili yaani Kiswahili na Kîîgembe kuonyesha jinsi zinavyofanana au kutofautiana. Kazi hii ni muhimu kwa utafiti huu kwani iliupa msingi wa lahaja ya Kîîgembe. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti kwani ulishughulikia uchanganuzi muundo wa sentensi ya Kîîgembe kwa msingi wa nadharia ya Eksibaa. Kwa hivyo, utafiti huu, ulibainisha aina ya viambajengo kama vile; vishazi na virai vinavyotumika kuunda sentensi ya Kîîgembe.

Taitumu (2014) alishughulikia uundaji wa maneno katika lugha ya Kimeru. Katika kazi yake mifano mbalimbali ya maneno ya Kîîgembe imejitokeza kwa mfano;
*mûwatimwana - Kîîgembe*
*Baby sitter – English*
*Mûrimi – Kîîgembe*
Farmer – English
(Taitumu, 2014: 93)

Taitumu (keshatajwa) anaeleza kuwa, maneno yanaweza kuundwa kutokana na kazi anayoifanya mtu. Kwa mfano, anatumia neno la Kîîgembe *mûrui* yaani mpishi kutokana na kitendo chake cha kupika. Aidha, *Mûrimi* ni jina la Kîîgembe linalomaanisha mkulima kutokana na hali ya mtu ya kulima. Isitoshe, anasema kuwa, uundaji wa vivumishi hutegemea nomino, kwa mfano neno *ûmuthongi* yaani mrembo linategemea nomino *mwari* yaani msichana. Aidha, anasema kuwa uundaji hutokana na uambatanishaji wa maneno. Kwa mfano, *karamu ka rangi* yaani kalamu ya rangi, *mwariocukuru* kumaanisha msichana wa shule. Vilevile, anaonyesha kuwa maneno yanaweza kuundwa kwa njia ya kubuni. Kwa mfano; *ngwatîra nthoni mwana athome* – nipe heshima mtoto asome ni jina linalorejelea lapulapu zinazovaliwa na maskini ambao hawana uwezo wa kununua viatu vya ghali. Kazi hii ni muhimu sana katika

utafiti huu, kwani maneno aliyoyaunda Taitumu (keshatajwa) katika kitengo cha mofolojia ni mojawapo wa viambajengo vya sentensi ya Kîîgembe. Aidha, utafiti huu ni tofauti na kazi yake kwani ulijikita katika kuchanganua muundo wa sentensi ya Kîîgembe kwa kuainisha muundo wa vishazi na virai kwa kutumia nadharia ya Eksibaa.

**2.4 Misingi ya Nadharia**

Nadharia ambayo ilitumika katika utafiti huu ni Nadharia ya Eksibaa. Nadharia ya Eksibaa iliasisiwa na Chomsky (1970). Nadharia hii inajikita katika mfumo wa muundo virai. Nadharia hii iliibuka ili kueleza kirai kwa ukamilifu baada ya Sarufi Miundo Virai kuonekana kuwa na upungufu wa kuwa na kanuni nyingi. Aidha, Nadhari ya Eksibaa huongozwa na dhana ya kichwa (neno kuu) katika kirai na uhusiano wake na vipengele vingine ambavyo vimetumika kuunda kirai. Nadharia ya Eksibaa husaidia kuchanganua sentensi kwa kutekeleza majukumu kama vile; kubainisha muundo wa kirai, kuelezea mahusiano ya vipashio katika kirai, kuonyesha jinsi umilikaji unavyojitokeza baina ya vipashio na kuonyesha matumizi ya kanuni za kijumla katika kufafanua muundo wa kirai. Nadharia hii ilizuka ili kurekebisha taratibu za sarufi za awali.

Kwa mujibu wa Chomsky (1986) Nadharia ya Eksibaa hutumika katika uchanganuzi wa sentensi ili kuwezesha ujumlishaji wa sifa zinazojitokeza katika aina mbalimbali za virai kama vile virai nomino, virai vitenzi, virai vivumishi, virai vielezi na virai vihusishi. Alama ya (X) husimamia kichwa au neno kuu katika kirai na alama ya ritifaa (‘) (baa) husimamia vipashio vinavyofuatana na neno kuu (X’) katika kirai husika.

Kulingana na Chomsky (1986) muundo wa virai huchukuliwa kuwa na viwango vitatu vya uchomozi ambavyo ni;kiwango cha uchomozi wa neno, kiwango cha uchomozi wa kati na uchomozi wa upeo. Kiwango cha uchomozi upeo huwakilishwa na herufi ya neno kuu katika kirai pamoja na baa mbili juu yake (X’’). Kwa upande mwingine uchomozi wa kati huwakilishwa na herufi ya neno kuu katika kirai pamoja na baa moja (X’). Uchomozi wa neno huwakilishwa na alama (X). Nadharia ya Eksibaa inaonyesha kwamba, katika lugha zote, kila kirai huwa na kichwa lakini


mpangilio wa vipashio vinavyofuatana na kichwa hicho hutegemea lugha maalum. Katika mfano; ‘mtoto wangu,’ kichwa ni nomino ‘mtoto’ ilhali katika kirai kitenzi ’ameandika vizuri,’ kichwa ni kitenzi ‘ameandika.’ Kwa hivyo, kanuni kuu ya nadharia hii ni: KX → ..X… ambayo inaonyesha kwamba lazima kila kirai KX kiwe na kichwa cha X ili kirai chenyewe kiwe sahihi. Kwa hivyo KX → ..N.. na KX …T…ambapo N ni nomino na T ni kitenzi.

Kwa mujibu wa Cowper (1992) Nadharia ya Eksibaa ni nadharia ya Sarufi Miundo iliyoendelezwa badala ya ile ya Sarufi Miundo Virai. Hoja muhimu katika nadharia hii ni kwamba sheria za Sarufi Miundo Virai hazina budi kudhibitiwa; na kwamba kategoria zaidi za virai hazina budi kuongezwa. Udhaifu wa kanuni miundo virai ni kuwa kanuni hazikudhibitiwa na kwamba zilichukua muundo huru. Kauli ya Cowper (keshatajwa) inalingana na maoni ya Newmeyer (1986) anayesema kuwa, Nadharia Eksibaa ilitokana na ile hali ya kupata suluhisho baada ya kufahamika kuwa Nadharia ya Sarufi Miundo Virai ilikuwa na kanuni nyingi zilizohitaji kudhibitiwa.

Kulingana na Radford (1988) kuna viwango vitatu vya kuchanganulia virai; kategoria ya kiwango cha neno, kategoria ya kiwango cha kati na kategoria ya kiwango cha kirai. Aidha, anabaini kuwa kategoria za kati huwa kubwa kuliko kategoria kileksia lakini ndogo kuliko kategoria kamili (kirai kikuu). Kuna viambajengo vilivyo vikubwa kuliko nomino lakini vidogo kuliko kirai nomino. Kirai nomino lazima kiwe na nomino, kirai tenzi lazima kiwe na kitenzi, kirai husishi lazima kiwe na kihusishi, kirai elezi lazima kiwe na kielezi na kirai kivumishi lazima kiwe na kivumishi. Kipashio ambacho ni cha lazima katika kikundi fulani cha kirai kinaitwa kichwa cha kategoria. Sifa za kichwa zinakuwa sifa za kirai chote. Kichwa huamua upatanisho wa kisarufi katika kirai.

Kwa kuzingatia RN, RT, KV, KE na KH inawezekana kuwa na kirai ambacho kina kichwa pekee (Cowper 1992; 21) katika virai hivi vyote. Kipashio muhimu na cha lazima ni kichwa cha kirai. Vipashio vingine vyote ni huria (si vya lazima). Nadharia ya Eksibaa inaongozwa na dhana ya neno kuu (kichwa) katika kirai na uhusiano wake na vipengele vingine katika kuunda kirai. Katika Nadharia ya Eksibaa, alama X hutumika kuwakilisha neno kuu katika kirai na (‘) au baa huwakilisha vipashio

vifuatilizo vya neno kuu/kichwa katika kirai husika . Na X’’ huwakilisha kirai cha X. Maelezo haya yanaweza kuelezwa kwa mchoro ufuatao,




X ni kategoria ya maneno kama vile N (nomino), T (kitenzi), H (kihusishi),V (kivumishi), E (kielezi). Kibainishi na kijalizo si za kategoria leksia bali huwakilisha mahusiano. Kibainishi ni neno linalotumika pamoja na nomino (Habwe na Karanja 2004:4). Kulingana Radford (1988:229), jukumu la kibainishi katika nadharia ya Eksibaa ni kupanua N’ hadi N’’ katika kielelezo tungo. Mabano yaliyowekwa kwenye kibainishi na kijalizo yanadhihirisha kuwa vipengele hivi ni huria na wala si vya lazima.

Kategoria X hubadilika ili kuwakilisha kategoria zote za kileksika yaani nomino, vitenzi, vivumishi, vihusishi na vielezi. X ni mvurumisho wa baa moja wa kichwa X na X’’ ni baa mbili ama uvurumisho wa juu kabisa wa kitengo X. hubadilika ili kuwakilisha kategoria zote za kileksika yaani nomino, vitenzi, vivumishi, vihusishi na vielezi. X ni mvurumisho wa baa moja wa kichwa X na X ni baa mbili ama uvurumisho wa juu kabisa wa kitengo X.  X inatoa tafsili ya vijalizo na chagizo cha kichwa X. Kijalizo ni aina ya neno ambalo hukamilisha maana hasa katika vitenzi vishirikishi. Vijalizo vingi hutokana na nomino,viwakilishi na vivumishi. Katika nadharia hii, kuna dhana ya kichwa cha kirai ambacho ni lie kategoria inayotawala fungu la maneno.

Kichwa cha kirai kinaweza kuwa mwanzoni ama mwishoni mwa kifungu kinachounda mvurumisho wa Eksibaa moja kwa kutegemea lugha husika. Kîîgembe ni lugha iliyo na nafasi ya kichwa mwanzoni. Vijalizo pamoja na vibainishi ni muhimu katika mvurumisho wa hali ya juu kabisa wa kirai. Kufuatana na maendeleo ya kinadharia vichwa vinavyosimama bila vibainishi au vijalizo vimekuja kuchukuliwa kuwa virai kamili kutokana na haja ya kubana nadharia hii ili kuweza kutumika kuwakilisha miundo mbalimbali. Kutokana na hali hii nafasi hizi


huchukuliwa kuwa kapa pale ambapo hazijazwa. Vilevile vipashio vingine vidogo kama vile mofu huchukuliwa kama virai kamili.

Kwa mujibu wa Leffel na Bouchard (1991), Eksibaa husimama kama neno kuu ambalo linaweza kuwa nomino, kitenzi, kielezi, kivumishi na kadhalika katika muundo wa kirai, nayo husimama kama muundo kiini. Hivyo kirai cha kategoria fulani kitakuwa na neno ambalo ndicho kiini cha kirai hicho. Kwa mfano, kirai nomino (KN) kiini chake kitakuwa ni nomino (N) ambayo itachukuwa nafasi ya X katika muundo wa kirai itakavyotumika katika utafiti huu. Vilevile kistari juu ya Eksibaa humaanisha vijalizo ambavyo hulifuata neno kuu katika muundo wa kirai.Vistari hivyo vitaweza kuwa vivumishi, vielezi, sentensi na kadhalika.

Nadharia ya Eksibaa inazingatia upangaji wa vipashio mbalimbali vya kileksia katika viwango tofauti katika sentensi. Ni upangaji unaobaini ni kipashio kipi kina uhusiano wa ngazi moja na ni kipi kinamiliki kingine. (Radford 1988), alitumia istilahi kama vile;

a) dada (viambajengo vilivyo katika ngazi moja)
b) binti ya (viambajengo vinavyomilikiwa na vingine)
c) shangazi (uhusiano usiotokana na kifundo kimoja)
d) kifundo (uhusiano katika kiwango cha udada)
e) kijalizo (kipashio kinachofafanua kichwa cha kirai katika kirai husika)
f) kibainishi (kategoria ya kileksia na hasa hutumika na nomino)
g) spesifaya (neno linalotumika na nomino na kwa kurejelea kategoria leksia huitwa kibainishi)
h) chagizo (sehemu inayoonyesha uhusiano wa uelezi)


Istilahi hizi zinaweza kuelezwa vyema kwa kutumia mchoro ufuatao;




Katika mchoro huu, (kibainishi) ni dada ya N’ na dada hao wawili yaani kibainishi na N’ ni binti za N’’. Wanamilikiwa na N’’. Chagizo ni dada na binti ya N’ na kijalizo ni dada ya N na binti za N’ chagizo ni shangazi ya N. Kijalizo hupanua N hadi N’. Nacho chagizo hupanua N’ hadi N’. Kibainishi hupanua N’ hadi N’’. Kutokana na maelezo haya inadhihirika kuwa uchanganuzi wa Eksibaa unatusaidia kueleza uhusiano wa viambajengo kwa kuzingatia muundo pekee. Ufafanuzi zaidi unadhihirika katika kielelezo kifuatacho;

S8 Û*rîa mwini wa rwîmbo kuuma Mutuati.* (Kîîgembe )

Yule mwimbaji wa wimbo kutoka Mutuati. (Kiswahili)




Kipashio KN kinamiliki vifundo vya kibainishi na N’. Kifundo cha kibainishi na cha N’ ni cha kiwango kimoja (dada). N KH (Kijalizo) ni vipashio vya ngazi moja na

vinamilikiwa na N’. N’ na KH (chagizo) pia ni vipashio vya ngazi moja na vinamilikiwa na N’ Kwa kuzingatia maelezo ya mchoro huu uhusiano baina ya nomino N na chagizo ni wa mbali. Lakini kuna uhusiano wa karibu sana kati ya kichwa N na kijalizo. Hii ndiyo sababu haiwezekani kukitenganisha kijalizo na kichwa cha kirai na kukihamisha hadi mwisho wa kirai.

Kwa mujibu wa Leffel na Bouchard (1991), Nadharia ya Eksibaa huwakilishwa na neno kuu ambalo linaweza kuwa, kitenzi, nomino, kielezi, kivumishi na kihusishi kwani ndio hubeba sifa za kirai. Kwa hivyo, kirai kitakuwa na sifa za kategoria fulani ya neno ambalo ndicho au neno kuu la kirai hicho. Kwa mfano, kirai nomino (RN) kiini chake kitakuwa ni nomino (N) ambayo itachukuwa nafasi ya X katika muundo wa kirai kilivyotumika katika utafiti huu. Kwa mfano;

*S9 Mwarimû nîakûritana - Kîîgembe*
Mwalimu anafundisha – Kiswahili

Katika mfano huu, neno *mwarîmû* ni nomino ambayo imesimama kama neno kuu la kirai nomino na wakati huo huo limesimama kama kirai nomino katika fungu hilo. Nadharia ya Eksibaa inaeleza kuwa, muundo wa kirai unaweza kuwa na mchomozo mpana wa kibainishi kimoja au zaidi. Hali hii hujitokeza kwa neno kuu kama nomino kufuatwa na kibainishi kingine katika muundo wa kirai. Mfano ufuatao kutoka Kîîgembe unafafanua dhana hii:

*S10 Ngûkûû îrîa îrareterwe îoro îukua- Kiigembe*
Kuku aliyeletwa jana amekufa- Kiswahili

Mfano huu unaonyesha kuwa sentensi ya Kiigembe inaweza kuwa na mchomozo mpana kwa kuchukua vibainishi zaidi. Kwa kuangalia umuhimu wa kuchanganua sentensi na virai kwa kutumia nadharia inayoangalia kategoria kama hii ya Eksibaa, iliweza kuchanganua miundo ya vishazi na virai mbalimbali vya sentensi ya Kîîgembe. Hii ni kwa sababu, sentensi huundwa kwa mpangilio maalumu ambao huwa na virai ambavyo vimewekwa katika seti maalumu ya kategoria ambapo kategoria ya virai na vishazi ni sehemu muhimu ya sentensi ya Kîîgembe

**Mihimili ya Nadharia ya Eksibaa**

Mihimili ifuatayo iliweza kutumika katika utafiti wa kazi hii. Hii ni pamoja na;

(i) Kila kirai huwa na neno kuu

Kulingana na Leffel na Bouchard (1991), nadharia ya Eksibaa huwakilishwa na neno kuu katika kirai ambalo hubeba sifa za kirai kile. Neno kuu katika kirai nomino cha Kîîgembe huwa ni neno la kwanza katika kirai nomino, ambalo huwa ni nomino au kiwakilishi cha nomino. Kwa mfano;

*S 11Mwaana mûkuî aûkûlûka – Kiigembe*

Mtoto mfupi amepita - Kiswahili


Neno kuu la kirai nomino ni " mwaana"

Radford (1988) anasema kuwa, kila mahali kunapotokea kategoria ya kirai ni lazima kuwe na kategoria ya leksia. Hii inamaanisha kwamba, kila mahali ambapo kwa mfano; kirai nomino kinapotokea lazima kuwe na nomino na kila kirai kihisishi kinapojitokeza lazima kuwe na kihisishi na kila kirai tenzi kinapojitokeza lazima kuwe na kitenzi. Vipashio hivi yaani, nomino, kitenzi, kihisishi hujulikana kama, kichwa kwani ndio hubeba sifa za kategoria ya kirai kile. Nadharia ya Eksibaa huongozwa na ``kichwa'' ambalo ni neno kuu katika kirai. Kategoria hizi za chini huweza kuwakilishwa na (X). Jerono (2003) anasema kuwa, kategoria za juu huweza kuwakilishwa na kategoria za chini katika uchanganuzi kwa kutumia matawi. Kichwa cha kirai kinaweza kuwa mwanzoni ama mwishoni mwa kifungu kinachounda mvurumisho wa Eksibaa moja kwa kutegemea lugha husika. Kîîgembe ni lugha iliyo na nafasi ya kichwa mwanzoni. Vijalizo pamoja na vibainishi ni muhimu katika mvurumisho wa hali ya juu kabisa wa kirai. Kufuatana na maendeleo ya kinadharia vichwa vinavyosimama bila vibainishi au vijalizo vimekuja kuchukuliwa kuwa virai kamili kutokana na haja ya kubana nadharia hii ili kuweza kutumika kuwakilisha miundo mbalimbali. Kutokana na hali hii nafasi hizi huchukuliwa kuwa kapa pale ambapo hazijazwa. Vilevile vipashio vingine vidogo kama vile mofu huchukuliwa kama virai kamili.

Kwa mfano;

*S11 Mũritwa ũrĩa mwea awîta cukuru -Kiigembe*

Mwanafunzi yule mzuri ameenda shuleni - Kiswahili




ii) Vipashio katika kirai hupangwa katika ngazi tofauti

Hadhi ya vipashio inapaswa kuonyeshwa vizuri na kwa uwazi zaidi. Ubainishaji wa hadhi ya vipengele vya kileksia ndio huonyesha ni vipashio vipi vinamiliki vipi katika sentensi au kirai. Aidha, ubainishaji huu ndio hudhihirisha vipashio vilivyo katika ngazi sawa au kuwa na uhusiano wa udada. Kichwa cha kirai huwakilishwa kwa X. Hii ndiyo ngazi ya chini kabisa na huwa haina baa yoyote. Ngazi ya pili huwa na baa moja (X') ilhali ile ya tatu huwa na baa mbili (X'') na kuendelea hivyo kutegemea muundo wa kirai. Kwa mujibu wa Radford (1988) anasema kuwa, kila kategoria ya kirai kuna kategoria ya leksika. Hii ni kumaanisha kila mahali ambapo kwa mfano ; kirai tenzi kinapojitokeza lazima kuwe na kitenzi, kila kirai nomino lazima kuwe na nomino na kila kirai kihisishi kinapojitokeza lazima kuwe na kihisishi. Vipashio hivi yaani, nomino, kitenzi, kihisishi hujulikana kama , kichwa kwani ndio hubeba sifa za kirai kile. Nadharia ya Eksibaa huongozwa na ``kichwa'' ambalo ni neno kuu katika kirai. virai huweza kujitokeza katika viwango vitatu, navyo ni kama vifuatavyo;

a) Kategoria ya kiwango cha neno

N- nomino

T- kitenzi

V- kivumishi

H- kihusishi

E- kielezi

I – kihisishi

b) Kategoria ya kiwango cha kati kama vile;

N- nomino baa moja

V- kivumishi baa moja

H- kihusishi baa moja

E- kielezi baa moja

T- kitenzi baa moja

c) Kategoria ya kiwango cha kirai kwa mfano;

RN- kirai nomino

RT- kirai tenzi

KV- kirai kivumishi

KH- kirai kihusishi

KE- kirai kielezi

KI- kirai kihisishi

Radford (1988:227) anabaini kuwa kategoria za kati huwa kubwa kuliko kategoria kileksia lakini ndogo kuliko kategoria kamili (Kirai kikuu). Kuna viambajengo vilivyo vikubwa kuliko nomino lakini vidogo kuliko kirai nomino na jinsi ambavyo kuna virai vikubwa kuliko nomino lakini vidogo kuliko Kirai nomino, ndivyo ilivyo kwa mfano;

i. Virai elezi vilivyo vikubwa kuliko vielezi lakini vidogo kuliko virai vielezi kamili.
ii. Virai vivumishi vilivyo vikubwa kuliko vivumishi lakini vidogo kuliko virai vivumishi kamili
iii. Virai vitenzi vilivyo vikubwa kuliko vitenzi lakini vidogo kuliko virai vitenzi kamili.
iv. Virai nomino vilivyo vikubwa kuliko nomino lakini vidogo kuliko virai nomino kamili.

Mifano katika sentensi ya Kîîgembe;

S12 *Johana nî* [ RN *ûria mûrîmi wa mpempe*]. – Johana ni yule mkulima wa mahindi

S13 *Mwarîmû nî* [*KV ûrîa mûkuî mûno* ].- Mwalimu ni yule mfupi sana

S14 *Mwarîmû* [RT *ûyû nîakuritana aritwa bake*].- Mwalimu huyu anafunza wanafunzi wake.

Viambajengo vilivyofungiwa kwenye mabano ni virai vya sentensi ya Kĩĩgembe vilivyo na maumbo tofauti. Viambajengo hivi ni virai kamili na ndani yake pana virai vya kati kama ifuatavyo;

S12 *Mûrîmî* = N (Kichwa)

*Mûrîmî wa mpempe* = (Kirai cha kati)

*ûrîa mûrîmî wa mpempe* = (Kirai kamili)

S13 *mûkuî* = V (Kichwa)

*Mûkuî mûno* = (Kirai cha kati)

*Urîa mûkûî mûno* = (Kirai kamili)

S14 *nîakûritana* = T (Kichwa)

*Nîakûritana aritwa bake* = (Kirai cha kati)

*ûyû Nîakûritana aritwa bake* = (Kirai kamili)

Kutokana na mifano iliyo hapo juu, ni kweli kuwa, kategoria za kati huwa kubwa kuliko kategoria za kileksia lakini ndogo kuliko kategoria kamili. Aidha, kila kategoria ya kirai kina kategoria leksika. Kirai nomino lazima kiwe na nomino, kirai tenzi lazima kiwe na kitenzi, kirai vumishi lazima kiwe na kivumishi jinsi ambavyo imejitokeza katika mifano ya S12 – S13.

iii) Kipambanuzi

Kipambanuzi ni kipashio kinachobeba maneno ambayo kimuundo si lazima yawepo katika kirai. Kuhusishwa kwa maneno hayo hukusudia tu kufafanua neno kuu. Aghalabu vivumishi ndivyo hutumiwa kama vipambanuzi katika virai nomino ilhali vielezi ndivyo hutumiwa kama vipambanuzi katika virai vitenzi. Kwa mfano;

*S12 Johana nî ûria mûrîmi wa mpempe - Kiigembe*

Johana ni yule mkulima wa mahindi – Kiswahili

Kipambanuzi ni kivumishi kionyeshi " yule" ambacho kinafafanua nomino mkulima.

iv) Kijalizo

Kijalizo ni sehemu ya kirai ambayo huwa imeunganishwa kwa karibu sana na kichwa cha kirai hicho. Kila aina ya kirai huwa na kijalizo chake. Kijalizo huwa na uhusiano wa udada na kichwa cha kirai ;mfano,

*S84 Mwiti nî ûmûûme- Kiigembe*

Mwiti ni mwerevu - Kiswahili

Kijalizo kinatokea kwenye kirai kitenzi na kijalizo hicho ni kivumishi “mwerevu”.

v) Kipanuzi

Kipanuzi ni sehemu ya kirai ambayo hutoa maelezo zaidi kuhusu kirai na huwa hakina uhusiano na kichwa, kipambanuzi au kijalizo. Kwa mfano katika kirai nomino cha sentensi:

*S15 Mwarî ûrîa mwikumia aûkoloma - Kîîgembe*

Msichana yule mwenye maringo ameketi - Kiswahili

Kipanuzi ni “mwenye maringo.” Kirai kinaweza kubeba kipanuzi kimoja,viwili,vitatu au zaidi. mfano; Msichana yule mwenye maringo, ambaye ni mfupi ameketi.

Kuna njia mbalimbali ambazo hutumika katika kuchanganua muundo wa sentensi. Kwa mfano; matawi na mabano. Matumizi ya mabano ya mraba hutenganisha vipashio vyote vilivyomo katika kiambajengo kwa kutumia mabano hayo. Kiambajengo huvidhibiti viambajengo vidogo vinavyounda kirai au sentensi. Mfano ufuatao unaonyesha uchanganuzi wa muundo wa sentensi kwa njia ya mabano:

*S16 Mûritwa ûmûraya akwîja - Kîîgembe*

Mwanafunzi mrefu amefika - Kiswahili

[RN [N mûrîtwa] [V ûmûraya][T *ak*wîja].


Neekemiah (2010:18) anaeleza kuwa ni vizuri kuchanganua miundo ya kisintaksia kwa kuangazia uchanganuzi wa kategoria ya virai na si kwenye mkabala wa maneno tu. Kutokana na hali hiyo, utafiti huu ulitumia nadharia hii kujaribu kuonyesha miundo mbalimbali ya virai vya sentensi ya Kîîgembe. Aidha, nadharia ya Eksibaa huwa na vifundo ambavyo hupangana kisafu na hujulikana kama vifundo dada ambavyo hutawaliwa moja kwa moja na kifundo cha juu (Fromkin, 2000). Kwa mfano, ikiwa KN kitakuwa ni kifundo cha juu na kitatawalia N na V ambavyo vitakuwa ni vifundo vya chini na pia ni viambajengo vidogo.Taratibu hizi za mpangilio wa vifundo vya viambajengo kiwima na kisafu zimeibua dhana mbili muhimu zinazojulikana kama utawalia na utangulizani. Utawalia huhusu uhusiano wa kifundo cha juu na cha chini yake.Uhusiano huo unaonyeshwa kwa mistari, huonyesha kuwa kifundo cha chini ni kiambajengo cha kifundo cha juu. Kifundo cha juu huweza kutawalia kifundo cha chini kimoja, viwili, vitatu au zaidi.Utangulizani

kwa upande mwingine huonyesha uhusiano wa vifundo kisafu. Hapa vifundo vya chini vinavyotawaliwa moja kwa moja na kifundo cha juu huitwa dada.Vifundo dada hujipanga katika daraja sawa kisafu na huwa jirani pale vinapohusika vifundo viwili vinavyotawaliwa moja kwa moja na vifundo vya juu.

Katika utafiti huu, miundo ya virai vya sentensi ya Kĩĩgembe ilichanganuliwa kwa kutumia matawi ya kisintaksia kwa sababu, matawi huonyesha uhusiano wa moja kwa moja wa vipashio vinavyounda viambajengo vya sentensi kama vile; virai. Kwa kawaida matawi haya huchomoza kutoka kwenye viambajengo. Kila kifundo huwakilisha kiambajengo kilichomo katika muundo wa kirai au sentensi. Kifundo kinachokaa juu katika mti wa kisintaksia hufahamika kama kifundo cha juu na ndicho kiambajengo kikubwa. Kifundo hiki ndicho hutawala vifundo vya chini ambavyo hubeba viambajengo vidogo. Katika matawi haya, vifundo vya daraja la chini hupangana kuonyesha kipashio kipi hutangulia kingine. Mfano wa sentensi ya Kĩĩgembe;

*S17 Mwekûrû ûyû mûkuî endete kûrîma rûkîrî mûno- Kiigembe*

Mama huyu mfupi anapenda kulima asubuhi sana- Kiswahili




Aidha, nadharia ya Eksibaa huwa na vifundo. Vifundo hivi hupangana kisafu na hujulikana kama vifundo dada ambavyo hutawaliwa moja kwa moja na kifundo cha juu (Fromkin, 2000). Kwa mfano, ikiwa KN kitakuwa ni kifundo cha juu kitatawalia na N na V ambavyo vitakuwa ni vifundo vya chini na pia ni viambajengo vidogo vya kifundo cha juu.

## 2.5 Hitimisho

Sura hii ilishughulikia sentensi ya Kibantu, sentensi ya Kiswahili na Kîîgembe. Maandishi haya yanadhihirisha kuwa lahaja ya Kîîgembe haijafanyiwa utafiti wa kina hasa katika kiwango cha sintaksia. Kazi hizi zilimpa mtafiti uelewa wa njia za kitaaluma za kutafiti kazi za kiisimu. Nadharia ya Eksibaa iliyoasisiwa na Chomsky (1970), na kuendelezwa na Radford (1988) ndiyo iliyoongoza utafiti huu. Misingi ya Nadharia ya Eksibaa ilielezwa kwa kina kwani ni Nadharia ambayo ilitumika kuchanganua muundo wa sentensi ya Kîîgembe

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanywa maeneo tawala ya Igembe Kusini katika eneo la Maua, Igembe Kaskazini eneo la Laare na Igembe ya Kati katika eneo la Mûringene ambayo ni maeneo yenye wazawa asilia wa Kîîgembe. Aidha, ni maeneo ambayo hajaathirika na lahaja zingine za Kimeru. Kwa hivyo, wazungumzaji wa Kîîgembe kutoka maeneo haya wana ujuzi na umilisi wa sentensi ya Kîîgembe. Watafitiwa walikuwa jumla ya watu thelathini ambao ni jumla ya watu kumi kutoka kila eneo tawala la Laare, Maua na Mûringene. Watafitiwa walikuwa  ni watu kumi wa kwanza kuhojiwa na mtafiti katika maeneo ya Laare, Maua na Mûringene. Kwa vile lahaja hii haina maandishi mengi na aghalabu inatumika zaidi kwa mazungumzo ya ana kwa ana, mtafiti alinakili kwenye kitabu ili   kuchanganua muundo wa sentensi ya Kîîgembe. Licha ya tofauti za kiumri, tajriba na cheo wakaazi hawa hutumia sentensi za Kîîgembe katika mawasiliano yao yakiwemo ya kibiashara, kisiasa, furaha na huzuni. Mtafiti alifanya utafiti katika maeneo tawala Laare, Maua na Mûringene na kupata data kutoka kwa wazawa ambao wana tajriba na uweledi wa lahaja ya Kîîgembe na kuweza kupata data ya sentensi 120 za Kîîgembe.

## 3.2 Mpango wa Utafiti

Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data ya sentensi ya Kîîgembe. Mtindo huu ulifaa  katika utafiti huu kwa kuafikia lengo la utafiti huu ambalo ni uchanganuzi wa muundo wa sentensi ya Kîîgembe. Aidha, ulibainisha muundo wa sentensi ya Kîîgembe kwa kuchanganua virai na vishazi vya sentensi ya Kîîgembe kulingana na data zilizopatikana kutoka kwa watafitiwa thelathini na tajriba ya mtafiti ambaye ni mzawa wa lahaja ya Kîîgembe.

## 3.3 Kundi Lengwa

Kwa mujibu wa Walliman (2011;124), kundi lengwa ni jumla ya vitu na watu wote wanaohusika katika utafiti kwa nia ya kusaidia kupata kinachotafitiwa katika utafiti. Katika utafiti huu kundi lengwa ni wakaazi wote wa Igembe ambao ni watumiaji wa asili wa lahaja ya Kîîgembe. Walengwa wa lahaja ya Kîîgembe 30 walipatikana katika maeneo tawala matatu ambayo ni, Laare, Maua na Mûringene. Walengwa hao

walikuwa ni watu wazima wanawake kwa wanaume. Mtafiti alichagua kundi la watu 30 kwa vigezo kuwa ni wenyeji na wajuzi wa Kîîgembe, wazawa asilia na ambao hawajaathirika na lahaja zingine za Kimeru. Idadi hii pia ilitumika kuthibitisha na kuhakiki data iliyozalishwa na mtafiti.

### 3.4 Uteuzi wa Sampuli

Kwa mujibu wa Kothari (2009), usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kuafikia lengo la utafiti. Utafiti huu ulitumia sampuli ya watu 30, yaani watu wa kwanza kumi kuhojiwa katika maeneo tawala matatu Laare, Maua na Mûringene. Uteuzi huo wa watu 30 pekee ulifanywa kwa kuwa watu wazungumzaji wa lugha yoyote ile wana ujuzi na umilisi wa lugha husika usitofautiana mno na kwa hivyo idadi kubwa haingeleta tofauti yoyote kwa utafiti huu. Aidha, sampuli hii ilitumiwa katika kuhakiki data iliyozalishwa na mtafiti ambaye ni mzawa wa lugha hii. Kothari (keshatajwa) anasema kuwa, uzuri wa utafiti ni kwa mtafiti kuchagua watafitiwa watakaofanikisha utafiti wake. Hivyo, sampuli kusudio ilimsaidia mtafiti kupata watoa taarifa wanaofaa. Utafiti huu ulihusisha mawasiliano ya miktadha ya harusi, matanga, biashara na siasa. Muundo wa sentensi katika Kîîgembe ni wa hulka funge kuliko mada inayohusu tabia za watu wenyewe. Hivyo basi, mtafiti aliridhika kuwa na sampuli ya miktadha ya harusi, matanga, biashara na siasa kwani, ilitosha kupata data ya senteni ya Kîîgembe. Mtafiti alichagua watu thelathini yaani watu wa kwanza kumi katika kila eneo tawala la Laare, Maua na Mûrîngene. Wazungumzaji katika maeneo tawala ya Laare, Maua na Mûrîngene wana ujuzi wa lahaja ya Kîîgembe; hii ni kwa sababu lahaja hii ndiyo hutumika katika shughuli mbalimbali za maisha yao. Kwa hiyo, data walizotoa zilikuwa za kuaminika

### 3.5 Maadili ya Utafiti

Kulingana na Kothari (2009) maadili ni suala muhimu sana katika kila kazi ya utafiti. Kwa hivyo, kazi hii haikuepuka suala la kimaadili. Ni kutokana na sababu hiyo, mtafiti alipata kibali kutoka kwa Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi cha kufanya utafiti. Utafiti huu ulifanywa kwa njia wazi na kwa kuzingatia masuala ya uadilifu kama vile, kulinda haki ya watafitiwa, kuweka siri za watafitiwa na kuwa mwaminifu. Mtafiti alikusanya jumla ya sentensi 120 za Kîîgembe kwa

kuzalisha yeye mwenyewe kutokana na umilisi wake wa kuwa mzawa wa lahaja hii na pia kufanya utafiti nyanjani. Data hii ilitumika kuainisha aina tatu za sentensi huku kila aina ya sentensi ikishughulikiwa na jumla ya sentensi arubaini. Data iliyotumiwa ilikuwa ya kuaminika. Kulingana na Kothari (keshatajwa), mtafiti aliweza kuonyesha maadili ya utafiti kwa kuwa na usiri wa kutotoa siri za watafitiwa wa Kîîgembe na kuwahakikishia usalama kwa kutotoa siri zao. Aidha, mtafiti alishirikiana na watafitiwa yaani Waigembe na kupata data ya sentensi 120. Mtafiti alilinda haki za watafitiwa wa Kîîgembe kwa kutotoa siri zao, kwa kuwa wazi kuhusu utafiti, kuheshimu watafitiwa katika utafiti wake, kuweka siri, kuwa mwaminifu na mwadilifu kwa utafiti wake ili kufanikisha masuala ya kimadili.

### 3.6 Mbinu za Ukusanyaji Data

Mbinu zifuatazo ziliweza kutumika ili kufanikisha utafiti huu.

#### a) Mbinu ya Uchunzaji

Hii ni mbinu ambayo mtafiti alikusanya data kwa kushiriki katika mazingira ya kundi lengwa. Mtafiti aliweka kumbukumbu za taarifa lengwa katika daftari. Kothari (2009) anasema kuwa, matumizi ya mbinu ya uchunzaji humlazimu mtafiti awepo katika yale mazingira halisi ili aweze kupata data iliyo sahihi. Aidha, mtafiti anapaswa kutumia viungo vya kuona na kusikia zile taarifa za watafitiwa. Ili uchunzaji uwe wenye kuafikia shabaha, mtafiti alimakinika katika kuandika data zilipotolewa, ili kuafikia malengo ya ukusanyaji wa data.

#### b) Uzalishaji Binafsi

Mtafiti alitumia chanzo cha data zaidi ya kimoja ili kupata data zinazofaa na za kutosha kutoa matokeo bora. Njia kuu ilikuwa mtafiti kuzalisha zile sentensi mwenyewe kwa kuwa mzawa wa lahaja na pia kukusanya data nyanjani ili kuondoa shaka la kuwa na upendeleo. Jumla ya data ya sentensi zilizokusanywa ni 120. Mtafiti alitunga data ya sentensi ya Kîîgembe na pia kukusanya nyanjani na kuichanganua kwa misingi ya Nadharia ya Eksibaa. Chomsky (1986), akijibu swali ni kivipi mzawa wa lahaja anayezalisha sentensi ataepukana na upendeleo, anasema kuwa, kuna aina mbili za umilisi yaani, umilisi wa kisanyansi na umilisi kisarufi. Aidha, anasema kuwa, umilisi wa mzawa wa lugha yeyote ile hudhihirika kwa kuwa na ufahamu wa

fonolojia, sintaksia na semantiki ya lugha hiyo. Ni kutokana na ukweli huu anasema kwamba, mzawa wa lugha ana uwezo wa kuunda sentensi kamilifu kutokana na kuelewa sauti za lugha yake na zilizo na maana iliyokusudiwa bila upendeleo au utata wowote ule kwani anaelewa sentensi zilizo na kasoro. Kwa hivyo, suala hili lina maana kuwa, mzawa wa lugha anaweza kuzalisha sentensi bila upendeleo. Hata hivyo, mtafiti alitafiti nyanjani na kutmia sampuli ya watu 30 kuthibitisha data ili kuondoa shaka la upendeleo na kufanikisha kupata jumla ya sentensi 120 zilizochanganuliwa.

### 3.7 Uwasilishaji wa Matokeo

Utafiti huu, ni utafiti wa kimaelezo na ulilenga kuchanganua muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe. Data za sentensi ya Kĩĩgembe zilichanganuliwa kwa misingi ya Nadharia ya Eksibaa. Baada ya mtafiti kutunga na kukusanya data za sentensi mbalimbali za Kĩĩgembe alifafanua miundo ya viambajengo vya sentensi ya Kĩĩgembe kama vile virai na vishazi. Aidha, alieleza miundo mbalimbali ya virai kama vile; virai nomino, virai tenzi, virai vivumishi, virai vielezi na virai vihusishi. Mtafiti alifafanua miundo ya vishazi kwa kurejelea aina tatu za vishazi ambavyo ni pamoja na; vishazi tegemezi, vishazi huru na vishazi viambatani. Uchanganuzi huu ulifanywa kwa kurejelea aina tatu za sentensi za Kĩĩgembe ambazo ni; sentensi sahili, ambatano na changamano. Aidha, data ilihitajika kutafsiriwa katika lugha ya Kiswahili ambayo iliweza kutolea maelezo ya sentensi. Utafsiri uliozingatiwa katika kazi hii ni ule wa muundo. Nadharia ya Eksibaa ndiyo iliyoongoza katika uchanganuzi muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe. Hii ni kwa sababu ni nadharia ambayo huonyesha uhusiano wa viambajengo vya sentensi na miundo ya virai ambavyo ni viambajengo vya sentensi hii ya Kĩĩgembe.

# SURA YA NNE

# MIUNDO YA VIRAI VYA SENTENSI YA KIIGEMBE

## 4.1 Utangulizi

Sentensi ni tungo kubwa zaidi za kimuundo kuliko kirai na kishazi na husheheni maana iliyokamilika. Huainishwa kwa kuzingatia muundo na uamilifu yaani lengo la sentensi. Kwa kuzingatia kipengee cha muundo ambao ni lengo la utafiti huu tuna aina tatu kuu za sentensi ambazo ni: sentensi sahili, sentensi ambatano na sentensi changamano. Kwa kuchukulia kipengee cha dhamira tuna: sentensi za ombi, sentensi za amri, sentensi za taarifa, sentensi agizi na sentensi hisishi ambazo hasitazingatiwa katika utafiti huu kwani lengo lake ni kueleza muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe. Sentensi huwa na makundi mawili makuu yanayobeba virai tofauti. Kikundi cha kwanza ni kikundi nomino na cha pili ni kikundi tenzi. Ndani ya makundi haya kuna virai tofauti kama vile kirai vumishi, kirai nomino, kirai elezi, kirai tenzi na kirai husishi. Kirai ni kiambajengo muhimu katika uundaji wa sentensi ya Kĩĩgembe. Nadharia ya Eksibaa huainisha virai katika sentensi kwa kueleza uhusiano wake na viambajengo vingine vinavyotumika katika Kĩĩgembe. Uchanganuzi huu ulifanywa kwa kuzingatia lengo ambalo ni kueleza miundo ya virai vya sentensi ya Kĩĩgembe kwa mujibu wa Nadharia ya Eksibaa. Ili kufanikisha lengo kuu la utafiti huu yaani, kuchanganua muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe. Katika sura hii utafiti huu ulishughulikia aina mbambali za virai kama vile, virai nomino, virai tenzi, virai elezi, virai vihusishi na virai vivumishi  kulingana na nadharia ya Eksibaa iliyoasisiwa na Chomsky (1970).

## 4.2 Muundo wa Sentensi ya Kĩĩgembe

Miundo ya sentensi za lugha za Kibantu huwa na uhusiano mkubwa. Sentensi zake huundwa na kikundi nomino na kikundi tenzi. Kikundi nomino na kikundi tenzi huundwa kwa viambajengo vya kileksia. Kikundi nomino na kikundi tenzi ndivyo viambajengo ambavyo huweza kuunda sentensi ya Kĩĩgembe. Kikundi tenzi ni kiambajengo cha lazima katika sentensi kwani sentensi haiwezi kujisimamia kimaana bila kuwa na kikundi tenzi. Uchambuzi wa sentensi zilizokusanywa katika maeneo ya Kĩĩgembe ulizingatia sentensi sahili, sentensi changamano na sentensi ambatano. Sentensi hizi ziligawanywa katika makundi hayo matatu kwa msingi wa kuangalia viambajengo vinavyojenga sentensi yaani kirai na kishazi.

Sentensi yenye kishazi huru kimoja tu ilichanganuliwa kama sentensi sahili. Sentensi yenye kishazi tegemezi na kishazi huru ilichanganuliwa kama sentensi changamano huku sentensi yenye vishazi viambatani viwili au zaidi kama sentensi ambatano. Katika sura hii, utafiti huu ulishughulikia muundo wa kirai na jinsi ambavyo hufanikisha muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe. Kulingana na Massamba na wenzake (1999) kirai ni kipashio cha kimuundo chenye neno moja au zaidi lakini hakina muundo wa kikundi tenzi na kikundi nomino. Aidha, Wesana-Chomi (2017;14) anasema kuwa, kirai ni tungo iliyoundwa kwa neno au kundi la maneno ya kategoria tofauti yanayoshikamana. Kwa hivyo, sentensi ya Kĩĩgembe huwa na kiambajengo hiki ambacho kinaweza kuchukuliwa kama neno au fungu la maneno ambalo hufuata utaratibu mahususi kufanikisha muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe.

Lyons, J. (1986) anadokeza kwamba ni kanuni msingi ya sarufi kwamba kila sentensi sahihi ina sehemu mbili kuu za lazima katika muundo wake; kikundi nomino na kikundi tenzi na huenda pia iwe na kipambanuzi au kipanuzi kimoja au zaidi, ambacho ni cha hiari. Kimuundo kielezi hizo zaweza kuondolewa na bado sentensi ikabakia na maana msingi. Kitenzi kwenye kikundi tenzi ndicho huamua ikiwa sentensi sharti iwe na kitendwa kitendewa au la. Utafiti huu utatathmini ukweli wa maoni haya katika lugha ya Kĩĩgembe na maelezo haya yatazingatiwa katika kuweka wazi muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe. Kirai cha Kĩĩgembe hutegemea neno kuu yaani kichwa katika kirai husika kwa mwongozo wa Nadharia ya Eksibaa. Kirai ni kiambajengo cha juu cha sentensi ya Kĩĩgembe. Nadharia ya Eksibaa huchanganua sentensi ya Kĩĩgembe kama mkusanyiko wa virai mbalimbali. Uchanganuzi wa sentensi kwa mujibu wa Nadharia ya Eksibaa hueleza viambajengo vya sentensi kwa kuanza na virai na kisha vishazi.

### 4.2.1 Miundo ya Virai

Miundo ya virai hujikita katika neno kuu au kichwa cha kirai. Kulingana na Leffel na Bouchard (1991) neno kuu katika kategoria za virai ndio husimama kama neno kuu ambalo ni; kitenzi, nomino, kielezi, kivumishi au kihusishi. Kwa hivyo, aina za maneno katika sentensi ya Kĩĩgembe ndizo hutawala virai kulingana na mahusiano ya maneno katika sentensi. Virai huainishwa na aina tano za maneno yaani; virai nomino, virai tenzi, virai elezi, virai vihusishi na virai vivumishi. Aina za maneno

kama vile viwakilishi huchukuliwa kama virai nomino kutokana na uhusiano kati ya nomino na viwakilishi vya nomino. Aidha, vihisishi huchukuliwa kama virai elezi, huku viunganishi vikichukuliwa kama virai vihusishi kulingana na uhusiano wake.

Virai hujitokeza katika kategoria mbalimbali kama vile nomino, kivumushi, kitenzi na kadhalika. Kategoria ya kisintaksia ya neno huamua muktadha ambamo neno husika hutokea katika sentensi. Sarufi ya lugha fulani kama Kĩĩgembe huwa na sifa za kila kategoria ambazo huwa ni vijenzi vya muundo. Maneno ya kategoria mbali mbali huwekwa pamoja ili kuunda sentensi. Hata hivyo huu uwekaji pamoja wa maneno kuunda sentensi si wa kiholela holela bali hupangwa kingazi ambapo maneno huungana kujenga viambajengo vikubwa vinavyoitwa virai, vishazi na kisha sentensi. Kulingana na nadharia ya Eksibaa kila kirai huwa na neno kuu ambalo hutambulisha anwani ya kirai kwa vile hili neno kuu ndilo linalomiliki viambajengo vingine vya kirai husika. Virai hivi vinaweza kuwa: kirai nomino (RN), kirai kitenzi RT), kirai kivumishi (KV), kirai kielezi (KE) na kirai kihusishi (KH). Ni sifa za neno kuu la kila kirai ndizo zinazoamua vipashio vingine vinavyoshirikiana nacho kukikamilisha. Kwa mujibu wa Haegeman (1991) viambajengo vinavyoshirikishwa na neno kuu kuunda kirai.

#### 4.2.1.1 Miundo ya Virai Nomino

Nomino ni neno linalotaja kitu, kiumbe au hali. Yaani jukumu lake ni kukipambanua kitajwa. Nomino katika lugha ya Kĩĩgembe huainishwa katika ngeli mbalimbali. Virai nomino huweza kutumika kama kikundi nomino katika sentensi. Miundo ya virai nomino imejikita kwenye nomino au mahusiano maalum baina ya nomino na neno au mafungu ya maneno. Virai hivi vinatawaliwa na nomino au viwakilishi vyake ambavyo ndivyo vichwa vyake. Kwa mujibu wa Massamba na wenzake (1999) kirai nomino ni kirai ambacho muundo wake hutegemea nomino au mahusiano ya nomino na maneno mengineyo katika sentensi. RN ni kirai kinachohimiliwa na nomino au kiwakilishi chake. Hii ina maana kuwa neno kuu la RN ni nomino au kiwakilishi cha nomino. Virai vilivyo na neno kuu ambalo ni nomino vinarejelewa katika kazi hii kama RN halisi. RN pia kinaweza kuwa na kiwakilishi kama neno kuu lake. Viwakilishi katika lahaja iliyotafitiwa. Miundo mbali mbali ya RN imejadiliwa hapo chini. Kama ilivyoelezwa hapo awali, uhusiano wa kiwakilishi na nomino huwa ni wa

karibu sana. Kwa hivyo, kiwakilishi kilichukuliwa kama nomino mahali ambapo kinatokea katika sentensi ya Kîîgembe.

Sentensi ya Kîîgembe ina miundo ya kirai nomino ifuatayo;

(a) Kirai nomino cha nomino moja pekee.

Aina hii ya kirai nomino huundwa na neno moja tu ambalo ni nomino au kiwakilishi cha lugha ya  Kîîgembe. Kwa mfano;

S18  Mûritwa awîta cukuru (Kîîgembe)

Mwanafunzi ameenda shule (Kiswahili)


S19 Ntîî nîakûrimira mwarocia (Kîîgembe)

Mama anamlimia dadangu (Kiswahili)

S20  Nîwe ûkareta mûûkania (Kîîgembe)

Wewe utaleta bwana harusi (Kiswahili)

Muundo wa kirai nomino cha nomino moja pekee ya Kîîgembe unaonekana kwa kielelezo cha mchoro kama ifuatavyo;




Katika sentensi za S18- S20 virai nomino vya muundo wa neno moja ni *mûritwa*, *ntîî* na *nîwe* ni virai nomino ambavyo vimesimama kama neno kuu la kirai nomino kwani vimejengwa na nomino moja au kiwakilishi chake kama mfano wa S20. Kama ilivyoelezwa hapo awali ni kuwa kiwakilishi huchukuliwa kuwa nomino kwa sababu ya kuwepo na uhusiano wa karibu kwani kiwakilishi huweza kusimamia nomino katika sentensi ya Kîîgembe.

Radford (1988), anasema kuwa, Kulingana na Nadharia ya Eksibaa kila mahali ambapo kirai kinatokea lazima kuwe na kategoria ya leksia. Kategoria hizi za maneno ndizo hubeba sifa za kirai. Hii ni kumaanisha kuwa, kila kunapotea kirai nomino lazima kuwe na nomino jinsi ambavyo imewasilishwa na S19. Nadharia ya Eksibaa

huongozwa na kichwa ambalo ni neno kuu la kirai. Katika Nadharia ya Eksibaa kibainishi huweza kupanua N’ hadi N’’ ila wakati ambapo kirai nomino huwa na muundo wa nomino pekee huweza kujipanua hadi kiwango cha N’’.

( b) Kirai nomino cha nomino na kishazi tegemezi

Sentensi ya Kĩĩgembe huwa na kirai nomino ambacho kinaundwa na nomino na kishazi tegemezi. Mifano ifuatayo imethibitisha.

S21 *Mwiki ûrîa ûraikîrue îoro* nî ûmûnthongi (Kĩĩgembe)

Bibi arusi aliyeolewa jana ni mrembo (Kiswahili)

S22 *Miraa îria îraûrîrwe îoro* nî yeetû (Kĩĩgembe)


Miraa iliyonunuliwa jana ni yetu (Kiswahili)

S23*Mûate yûrîa yûraûrîrwe* yûkûthûka (Kĩĩgembe)

Mkate ulionunuliwa umeharibika (Kiswahili)

Muundo wa kirai nomino cha nomino na kishazi tegemezi cha Kĩĩgembe kinajitokeza kwa namna ifuatayo;

S21




Kwa mujibu wa Nadharia ya Eksibaa kipanuzi ni sehemu ya kirai ambayo hutoa maelezo zaidi kuhusu kirai. Kirai kinaweza kubeba kipanuzi kimoja, viwili au zaidi. Katika mifano ya S21 – S23 vishazi tegemezi vimetumika kama vipanuzi. Kipanuzi si kategoria ya lazima katika kirai kwani vishazi tegemezi katika mifano ambayo imetumika inaweza kutolewa na kirai kiweze kujipanua. Maneno yaliyoandikwa kwa herufi za mlazo ni muundo wa kirai nomino cha Kĩĩgembe ulio na kirai nomino na kishazi tegemezi kwa mfano; *Mwiki ûrîa ûraikîrue îoro, miraa îrîa îraûrîrwe îoro* na *mûate yûrîa yûraûrîrwe*. Vishazi tegemezi vinapotumika pamoja na nomino hufanya kazi ya kuvumisha nomino ambayo imetumika. Kwa mfano; *ûrîa ûraikîrue îoro îrîa*

*îraûrîrwe îoro na yûrîa yûraûrîrwe* ni vishazi tegemezi vinavyovumisha nomino zilizo katika S21- S23

.

(c) Kirai nomino cha nomino na kivumishi

Kivumishi hiki huwa kinaelezea nomino ambayo ni kichwa cha kirai moja kwa moja. Kivumishi katika muundo huu kinaweza kuwa kimoja au zaidi. Nadharia ya Eksibaa hueleza dhana ya kipambanuzi kama kipashio kinachobeba maneno ambayo kimuundo si lazima yawepo katika kirai. Aidha, Nadharia ya Eksibaa inatilia mkazo kuwa, kuhusishwa kwa kivumishi kimoja au zaidi hukusudia tu kufafanua neno kuu (kichwa). Aghalabu vivumishi ndivyo hutumiwa kama vipambanuzi katika virai nomino ilhali vielezi hutumika kama vipambanuzi katika virai vitenzi. Kwa mfano;

S24 *Mûate yûû* nî yûmwea (Kîîgembe)

Mkate huu ni mzuri (Kiswahili)

S25 *Mwekûrû ûyû* ûmûraya akûra munda (Kîîgembe)


Mama huyu mrefu amenunua shamba (Kiswahili)

S26 *Maûta yakwa* yakûthira (Kîîgembe)


Mafuta yangu yameisha (Kiswahili)

Muundo huu unaweza kuwakilishwa katika mchoro kama ifuatavyo;

S24




S25




Mifano S24 – S26 inayoonyesha muundo wa kirai nomino (kilicho katika herufi za mlazo) ambacho kinaundwa na nomino na kivumishi. Vivumishi, kulingana na

Nadharia ya Eksibaa, vinafanya kazi ya kupanua nomino. Hata hivyo, kirai nomino cha Kîîgembe kinaweza kuchukua muundo wa nomino na vivumishi viwili au zaidi kwa mfano, S25.

(d) Kirai nomino cha kiwakilishi pekee

Kwa mujibu wa Kamusi Sanifu ya TUKI (1990), kiwakilishi ni neno linalosimama badala ya nomino. Kwa hivyo viwakilishi ni maneno ambayo kiuamilifu, huwakilisha nomino katika miktadha mbali mbali na hivyo basi ni aina ya RN. Hiki ni kirai nomino ambacho muundo wake ni wa kiwakilishi pekee. Hapo awali ilielezwa kuwa kiwakilishi huchukuliwa kama nomino kwa sababu ya uhusiano wake na nomino. Kiwakilishi hutumika kuwakilisha nomino mahali ambapo nomino haijaweza kutumika. Mifano ya kirai hiki ni kama ifuatayo,

S27 *Wee* nîakûthambîa mwaana (Kîîgembe)

Yeye anaosha mtoto (Kiswahili)

S28 *Kîî* kîkûrîrwa mûrîtwa (Kîîgembe)

Hiki kimenunuliwa mwanafunzi (Kiswahili)

Muundo wa kirai nomino cha nomino na kivumishi unaweza kuwakilishwa kwa kielelezo kifuatacho;

RN
|
N'
|
wee

Mifano hii iliyoandikwa kwa herufi za mlazo zinaonyesha mifano ya virai nomino vya Kîîgembe ambavyo vinaundwa na kiwakilishi pekee. Nadharia ya Eksibaa huongozwa na kichwa ambalo ni neno kuu katika kirai. Utafiti huu uliweza kuangazia aina tano za virai yaani virai nomino, virai elezi, virai tenzi, virai vivumishi na virai husishi. Aina za maneno huwa nane lakini virai huwa aina tano. Hii ni kwa sababu kategoria za maneno ambazo huwa na uhusiano kama vile, vihisishi na viunganishi huchukuliwa kama virai husishi huku viwakilishi vikichukuliwa kama virai nomino

kila mahali ambapo kiwakilishi kinapotokea. Maneno yaliyoandikwa kwa herufi za mlazo katika mifano ya S27-S28 ni viwakilishi ambavyo ni virai nomino.

(e) Kirai nomino chenye muundo wa kiwakilishi na kivumishi

Kirai nomino cha Kîîgembe huundwa na kiwakilishi na kivumishi. Mifano ifuatayo inaelezea zaidi.

S29 Yûû mûraya yûatemwa (Kîîgembe)

Huu mrefu utakatwa (Kiswahili)

S30 Yaa maîngî nî ya?(Kîîgembe)


Haya mengi ni ya nani? (Kiswahili)

S31 Kîî kînene kîatûka nîkîetû (Kîîgembe)

Hiki kikubwa kimevunjika ni chetu (Kiswahili)

Kirai nomino cha Kîîgembe chenye muundo wa kiwakilishi na kivumishi, kimewakilishwa na; *yûû mûraya, yaa maîngî na kîî kînene*. Muundo wa kirai hiki unaonekana hivi;

S29




Katika mifano S29- S3I, vivumishi ambavyo vimetumika vinafanya kazi ya kupambanua kirai nomino ambacho kimewakilishwa na viwakilishi katika sentensi hizo.

(f) Kirai nomino chenye muundo wa kitenzijina

Nadharia ya Eksibaa huongozwa na dhana ya kichwa (neno kuu) katika kirai na uhusiano wake na vipengele vingine ambavyo vimetumika kuunda kirai. Nadharia ya Eksibaa husaidia kuchanganua sentensi kwa kutekeleza jukumu kama vile; kubainisha muundo wa kirai. Katika muundo huu wa kirai nomino, nadharia hii ilitumika kuonyesha muundo wa kirai hiki ambacho ni kirai ambacho kiliundwa na nomino ya

kitenzijina pekee. Sentensi ya Kîîgembe huwa na muundo wa kirai nomino ambacho kina muundo wa kitenzijina. Kwa mfano:

S32 *Kûtheka* kûkatûwîrîa mûno (Kîîgembe)


Kucheka kutatufurahisha sana (Kiswahili)

S33 *Kûîna* nîkûkwea (Kîîgembe)

Kuimba ni kuzuri (Kiswahili)

Kirai nomino cha kitenzijina kina muundo ufuatao katika Kîîgembe,

S32




Mifano iliyoandikwa kwa herufi za mlazo ni mifano ya vitenzi jina vya Kîîgembe ambavyo vinatumika kuundia kirai nomino hiki. Hivi ni kama vile; *kûtheka* na *kûîna*.

(g) Kirai nomino cha muundo wa kitenzi jina na kivumishi

Hiki ni aina ya kirai cha Kîîgembe ambacho huundwa kwa kutumia kitenzijina na kivumishi. Mifano ifuatayo inathibitisha hilo.

S34 Kûîna kwake nî kûtûwîria (Kîîgembe)

Kuimba kwake kunafurahisha (Kiswahili)

S35 Kûcetha kûû tî kûkwea (Kîîgembe)


Kucheza huku si kuzuri (Kiswahili)

S36 Kûthoma kwake nî kwakûrîarania (Kîîgembe)

Kusoma kwake ni kwa kushangaza (Kiswahili)

Kirai nomino cha Kîîgembe chenye muundo wa kitenzijina na kivumishi unaweza kujitokeza ifuatavyo;

S35




Nadharia ya Eksibaa huzingatia upangaji wa vipashio mbalimbali vya kileksia katika viwango tofauti katika sentensi. Huu ni upangaji unaobaini ni kipashio kipi kina uhusiano wa ngazi moja na ni kipi kinamiliki kingine. Radford (1988) alitumia istilahi kama vile; dada (viambajengo vilivyo katika ngazi moja) kwa mfano; N’ na V’ viko katika ngazi moja, na binti ya (viambajengo vinavyomilikiwa na vingine) kwa mfano tulioutoa S35 N’ na V’ ni binti wa N’’ ambacho ndicho kirai kamili. Katika muundo huu wa kirai cha Kĩĩgembe chenye muundo wa kitenzijina na kivumishi vimeweza kuwakilishwa na; *Kûîna kwake, kûcetha kûû na Kûthoma kwake.*

(h) Kirai nomino chenye nomino mbili

Kirai cha Kĩĩgembe kinaweza kujitokeza na muundo wa kirai nomino chenye kichwa ambacho ni cha nomino mbili. Mifano ifuatayo inaweza kuthibitisha.

S37 *Mwekûrû o mûthoi* nî ûyû (Kĩĩgembe)


Mke wa msasi ni huyu (Kiswahili)

S38 *Mûwati o mwana* awîta (Kĩĩgembe)

Mlezi wa mtoto ameenda (Kiswahili)

S39 *Mwarîmû o twaana* nîakûrîtana (Kĩĩgembe)

Mwalimu wa watoto anawafunza (Kiswahili)



Mifano S37- S39 iliyoandikwa kwa herufi za mlazo ni mifano ya virai vya nomino vya Kĩĩgembe vyenye muundo wa nomino mbili ambavyo ni kama vile; *Mwekûrû o mûthoi, mûwati o mwana* na *mwarîmû o twana.*

**4.2.1.2 Miundo ya Virai Vivumishi**


Virai vivumishi ni aina ya virai ambavyo muundo wake huundwa kwa kivumishi.Hili ni fungu la maneno lenye kivumishi ambacho ndicho kichwa au neno kuu la kirai hicho. Kirai kivumishi hufanya kazi ya kutoa maelezo zaidi juu ya nomino au kiwakilishi chake. Aghalabu kirai cha Kĩĩgembe hujitokeza katika kirai cha nomino na kikundi tenzi hasa baada ya kikundi tenzi chenye muundo wa kitenzi kishirikishi. Kirai kivumishi cha Kĩĩgembe kinaweza kujitokeza kwa miundo ifuatavyo;

(a) Kirai kivumishi chenye kivumishi pekee.

S40 *Mûrîtwa* ***ûmuraya,*** *aûkîruka kîerîo.* (*Kĩĩgembe*)

Mwanafunzi mrefu amepita mtihani (Kiswahili)

Muundo wa kivumishi unaweza kujitokeza kama ifuatavyo;





Neno lililokoleshwa rangi ni kirai kivumishi chenye muundo wa kivumishi pekee.

(b) Kirai kivumishi chenye muundo wa zaidi ya kivumishi kimoja

S40 Mûrîtwa ûmuraya ûmûthongi aûkîruka kîerîo. (Kĩĩgembe)

Mwanafunzi mrefu mrembo amepita mtihani (Kiswahili)



Kulingana na Cowper (1992), muundo wa virai huchukuliwa kuwa na viwango vitatu vya uchomozi ambavyo ni; kiwango cha uchomozi wa neno, kiwango cha uchomozi wa kati na uchomozi wa upeo. Kiwango cha uchomozi upeo huwakilishwa na herufi ya neno kuu katika kirai pamoja na baa mbili juu yake (X’’). Kwa upande mwingine uchomozi wa kati huwakilishwa na herufi ya neno kuu katika kirai pamoja na baa moja (X’). Uchomozi wa neno huwakilishwa na alama (X). Uchomozi ambao unajitokeza katika mifano hii ni wa (X) ambao umethibitishwa kwa mchoro wa S40.

(c) Kirai kivumishi chenye kivumishi na kielezi

Kirai kivumishi cha Kîîgembe kinaweza kuchukua muundo wa kivumishi na kielezi kama inavyojitokeza katika mifano ifuatayo;


S41 Mwana ûmûkuî mûno nîakûrîra (Kîîgembe)

Mtoto mfupi sana analia (Kiswahili)

S42 Mwarîmû ûmûme mûno nîakûandîka (Kîîgembe)

Mwalimu mwerevu sana anaandika (Kiswahili)

Muundo wa kirai kivumishi cha Kîîgembe chenye muundo wa kivumishi na kielezi unaweza kujitokeza ifuatavyo ;





Vielezi katika virai vivumishi hivi vya S41- S42 vilitumika kama kipambanuzi ambacho kinakamilisha kirai kivumishi.

(d) Kirai kivumishi chenye kivumishi na nomino

Muundo wa kirai kivumishi unajitokeza kuwa na kivumishi na nomino kulingana na mifano hii inayothibitisha hilo.

S43 *Mwekûrû wa îtonga akwîja* (Kîîgembe)

Mke wa tajiri amekuja (Kiswahili)




Kirai kivumishi cha Kîîgembe chenye muundo wa kivumishi na nomino hujitokeza aghalabu katika vivumishi vya a-unganifu. Aidha, kulingana na Nadharia ya Eksibaa kila kirai huongozwa na neno kuu. Neno kuu katika mifano ya S43 ni kivumishi na hii ndio sababu, utafiti huu ulibainisha kuwa mfano huu ni wa kirai kivumishi.

**4.2.1.3 Miundo ya Virai Elezi**


Hivi ni virai vya sentensi ya Kîîgembe ambavyo hutumika kutolea maelezo zaidi juu ya kivumishi, kitenzi au kielezi kingine. Kwa mfano;

(a) Kirai kielezi chenye kielezi pekee

S44 *Ntîî awîta mundene* (Kîîgembe)

Mama ameenda shambani (Kiswahili)

Muundo huu unaweza kujitokeza ifuatavyo;





Kirai kielezi ambacho ni cha kielezi pekee kimetumika kujipanua kwani kulingana na Nadharia ya Eksibaa kirai cha neno huweza kujipanua kutoka E- E’ hadi E’’

(b) Kirai kielezi chenye kielezi zaidi ya kimoja

S45 Mwarîmû akûritana bwea mûno (Kîîgembe)

Mwalimu amefunza vizuri sana (Kiswahili)

Muundo wa kirai kielezi unaweza kujitokeza ifuatavyo;




Kulingana na Nadharia ya Eksibaa, kijalizo ni sehemu ya kirai ambayo huwa imeunganishwa kwa karibu sana na kichwa cha kirai hicho. Kila aina ya kirai huwa na kijalizo chake. Kijalizo huwa na uhusiano wa udada na kichwa cha kirai. Katika mfano S45 neno *mûno* ni kijalizo cha kirai kielezi kwani linaelezea zaidi kuhusu bwea. Aidha, linaonyesha uhusiano wa udada katika tungo hilo kwani E kinapambanua E’ hadi E’’.

#### 4.2.1.4 Miundo ya Virai Vihusishi

Kirai kihusishi, kama ilivyo aina nyingine za virai huwakilishwa na neno kuu yaani kichwa cha kirai ambacho ni kihusishi. Aghalabu kirai kihusishi hutokea sehemu ya kikundi nomino na kikundi tenzi. Iwapo kitatokea upande wa kikundi nomino basi hufanya kazi kama kielezi. Hata hivyo, kitokeapo upande wa kikundi nomino hufanya kazi ya kuvumisha. Miundo ya virai vihusishi inaweza kujitokeza ifuatavyo;

(a) Kirai husishi chenye kihusishi na kielezi


S46 Mpempe *cia mundene* ikûma (Kĩĩgembe)

Mahindi ya shambani yamekauka (Kiswahili)

S47 Aini *ba kanicene* bakwiya (Kĩĩgembe)

Waimbaji wa kanisani wamefika (Kiswahili)

Muundo huu wa kirai husishi unaweza kuwasilishwa kwa namna ifuatayo;



Muundo huu wa kirai husishi maneno yaliyoandikwa kwa herufi za mlazo ni virai vihusishi. Ilibainika kuwa virai husishi vya Kĩĩgembe vinaweza kutumika kama vielezi vinapotumika pamoja na kielezi.


(b) Kirai husishi chenye muundo wa kihusishi na nomino

S48 Biakûrîa **vya ngûûkû** bîkûya (Kĩĩgembe)

Vyakula vya nyanya vimeiva (Kiswahili)

S49 Kîratû **kîa mûranû** nî kîthongî (Kĩĩgembe)

Kiatu cha harusi ni kizuri (Kiswahili)




Virai husishi ambavyo vimekoleshwa rangi ni mfano wa virai vya Kĩĩgembe vinavyochukua muundo wa kihusishi na nomino. Katika nadharia ya Eksibaa kipambanuzi ni kipashio kinachobeba maneno ambayo hukusudia tu kufafanua neno kuu. Katika mifano ya S48-S49, maneno kama vile, *ngûûkû* na *mûranû* ni mifano ya vipambanuzi katika virai hivi vihusishi kwani vinatumika kuelezea vihusishi.

#### 4.2.1.5 Miundo ya Virai Vitenzi

Kitenzi ni aina ya neno ambalo linatoa taarifa juu ya tendo linalofanyika au linalitendwa au litakalotendwa na kiumbe au kitu. Kirai tenzi ni neno ama fungu la maneno ambalo huwa na kitenzi kama kichwa cha kirai. Kirai tenzi huwa na miundo mbalimbali. Kirai Kitenzi ni kirai ambacho kimeundwa katika mahusiano ya kitenzi na mafungu ya maneno (Massamba na wenzake, 1999). Kama kawaida ya virai neno kuu katika kirai kitenzi huwa ni kitenzi. Kirai kitenzi ni mojawapo wa kipashio cha lazima katika sentensi ya Kĩĩgembe. Miundo ya kirai kitenzi ni kama ifuatayo;


(a) Kirai kitenzi chenye kitenzi halisi pekee.

S50 Akûwa (Kîîgembe)

Ameanguka (Kiswahili)

S51 Nîakûthoma (Kîîgembe)

Anasoma (Kiswahili)




Muundo huu ni wa kirai kitenzi kimoja ambacho kinaweza kujisimamia kama sentensi ya Kîîgembe. Kichwa cha kirai ambacho ni neno kuu la kirai huweza kuwa neno moja ambalo hubeba sifa za kirai kikuu. Mifano hii inathibitisha muundo wa kirai ambacho kimeundwa na neno moja ambalo ni kitenzi cha pekee. Muundo wa Kîîgembe


( b) Kirai kitenzi chenye muundo wa kitenzi na kielezi

S52 Mwarîmû *akûrîtana mûno* (Kîîgembe)

Mwalimu amefunza sana (Kiswahili)

S53 Munda *niyûkûrîmîka bwea* (Kîîgembe)

Shamba linalimika vizuri (Kiswahili)




Virai vilivyoandikwa kwa herufi za mlazo ni mfano wa virai vitenzi vyenye muundo wa kitenzi na kielezi. Aidha, katika kielelezo cha matawi S52 neno *mûno* limetumika kama kijalizo ambacho ni dada ya kitenzi na hupanua kitenzi T' na T' hujinua hadi T''.


(c) Kirai kitenzi chenye muundo wa vitenzi viwili

S54 *Ndamûtîrîmîre akinaa* (Kîîgembe)

Nilimkuta akiimba (Kiswahili)

S55 *Noo akûthamba* (Kîîgembe)

Angali anaoga (Kiswahili)




Radford (1988) anadai kuwa vitenzi visaidizi ni vitenzi vinavyohitaji vitenzi vikuu hili kukamilishwa. Kitenzi kisaidizi hujalizwa na kitenzi kikuu. Aidha, vitenzi halisi huchukua aina tofauti za kategoria za maneno kuzijaliza.

Muundo wa kirai kitenzi chenye vitenzi viwili aghalabu hujitokeza hasa ambapo sentensi ya Kîîgembe imewakilishwa na kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu. Katika Nadharia ya Eksibaa kitenzi kikuu kinapoandamana na kitenzi kisaidizi, kinafanya kazi ya kujaliza kitenzi kisaidizi. Kijalizo hutumika kutolea maelezo kuhusu neno kuu ambalo ni kichwa cha kirai. Vitenzi kama vile, *ndamûtîrîmîre na noo* ni vitenzi ambavyo hukamilishwa na vitenzi *akinaa na akûthamba*

(d) Kirai kitenzi chenye muundo wa kitenzi na nomino

Massamba na wengine (I999) anasema kuwa kirai kitenzi ni kirai ambacho kimekitwa katika kitenzi na neno au mafungu mengine ya maneno. Hii ina maana kuwa neno kuu katika aina hii ya kirai ni kitenzi. Anaendelea kuwa katika miundo yote vipashio vinavyoandamana nacho (kitenzi) ni vya lazima. Hii inamaana kwamba kitenzi kinachohusika, kwa maumbile yake, aghalabu huaandamane na kipashio au vipashio vya aina zinazojitokeza mbele yake. Kwa mfano anadai kuwa, kila mara kinapotajwa

kitenzi kama rîma – lima huwa kuna matarajio sehemu yenyewe itajwe pia kwa mfano,

*Rîma munda* - Kîîgembe

lima shamba. – Kiswahili

**4.3 Hitimisho**

Katika Sura ya Nne utafiti huu ulichanganua miundo ya sentensi ya Kîîgembe kwa kuchanganua muundo wa virai. Mtafiti alieleza aina za virai katika sentensi ya Kîîgembe na kubaini kuwa kuna aina tano ya virai ambavyo ni; virai nomino, virai vielezi, virai vitenzi, virai vivumishi na virai vihusishi. Utafiti ulifafanua muundo wa sentensi za Kîîgembe kwa kurejelea uhusiano na mpangilio wa viambajengo vya sentensi kulingana na Nadharia ya Eksibaa. Hivi kwamba, sentensi ya Kîîgembe huundwa kwa mpangilio maalum wa virai ila si kupachika maneno tu. Uhusiano wa viambajengo hivi ndivyo hufanikisha miundo mbalimbali ya sentensi ya Kîîgembe. Kutokana na matokeo hayo, miundo ya virai katika lahaja ya Kîîgembe inaonekana kufanana kwa kiasi fulani na miundo ya virai katika Kiswahili. Mfano, katika Kiswahili kuna kirai nomino ambacho kinaundwa na nomino moja, Kirai Kielezi chenye vielezi viwili au kirai kivumishi kinachoundwa na kivumishi na kielezi. Hali hii inaonyesha kuwa inawezekana muundo wa virai katika lugha mbalimbali za Kibantu unafanana. Lakini utafiti zaidi unahitajika katika lugha nyingine za Kibantu ili ubainishe zaidi.

## SURA YA TANO
## MIUNDO YA VISHAZI VYA SENTENSI YA KIIGEMBE

### 5.1 Utangulizi

Sura ya Tano ilichambua data zilizozalishwa na mtafiti na kukusanywa nyanjani kuhusu muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe. Uchanganuzi ulifanywa kwa kuzingatia lengo la utafiti; ambalo ni kufafanua miundo ya vishazi vya sentensi ya Kĩĩgembe. Mathews (1997) anasema kuwa, kishazi ni kipashio cha kisintaksia ambacho umbo lake limeshushwa kutoka kategoria ile ya sentensi. Aghalabu huhusisha kitenzi na viambajengo vingine vinavyoandamana nacho. Wesana-Chomi (2017) anasema kuwa, kishazi ni kipashio kilicho na kikundi nomino na kikundi tenzi na ambacho kinaweza kuhusisha vipashio vingine. Vishazi hivyo basi, ni vipashio vya kimuundo ambavyo vipo kati ya sentensi na virai. Vishazi ni vidogo kuliko sentensi na kubwa kuliko virai. Uchanganuzi huu, ulizingatia mihimili ya Nadharia ya Eksibaa ambayo mwaasisi wake ni Chomsky (1970).

Habwe na Karanja (2004), alishughulikia aina mbili za sentensi: ambatani na changamani. Wataalamu hawa walisema kuwa sentensi ambatani imeundwa kwa sentensi mbili sahili zinazoshirikishwa pamoja kwa kiunganishi. Hii ina maana kuwa sentensi ambatani huwa na vishazi viwili huru vilivyounganishwa. Kinyume na hayo sentensi changamano huwa na kishazi kimoja huru na kingine tegemezi. Vilevile, sentensi changamano inaweza kuundwa kwa vishazi viwili tegemezi. Kishazi husemekana kuwa tegemezi iwapo hakiwezi kujitosheleza kimaana bila kutegemea kategoria nyingine katika sentensi. Aina zote tatu za sentensi kama Habwe na Karanja (mtaje), walivyozichanganua katika Kiswahili zilichunguzwa katika Kĩĩgembe.

### 5.2 Miundo ya Vishazi

Lengo mojawapo la utafiti huu, lilikuwa kufafanua miundo ya vishazi katika lahaja ya Kĩĩgembe. Utafiti huu ulibaini kuwa katika lahaja ya Kĩĩgembe kuna aina tatu kuu ya vishazi ambavyo hutumika kuundia aina tatu za sentensi za Kĩĩgembe;

a) Vishazi huru
b) Vishazi tegemezi
c) vishazi viambatani

Vishazi huundwa kutokana na mahusiano maalum ya virai mbalimbali. Utafiti huu uliainisha muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe kwa kuainisha miundo ya vishazi kwa

mujibu wa nadharia ya Eksibaa. Aidha, Radford (1981) anasema kuwa katika Nadharia ya Eksibaa, vishazi huundwa kwa kuandamanishwa virai mbalimbali. Kila kirai kimsingi huwa na neno kuu ambalo ni kichwa.

Kulingana na Chomsky, (1957) kishazi ni kipashio muhimu sana katika kujenga sentensi ya Kĩĩgembe. Mwanaisimu anapochambua sentensi hukizingatia kipashio hiki kama kijenzi cha lazima cha sentensi. Tungo haiwezi kuitwa sentensi pasipo kuundwa kwa kishazi. Uainishaji wa sentensi hufanywa kwa kuzingatia idadi na aina ya vishazi vinavyoijenga sentensi hiyo. Lyons (1968) na Massamba na wenzie (1999) ameifasili dhana ya kishazi kama kundi la maneno lenye kikundi nomino na kikundi tenzi, hasa likiwa ndani ya sentensi kuu. Kishazi ni kipashio cha kimuundo chenye neno moja au zaidi, kikubwa kuliko kirai na kidogo kuliko sentensi, chenye kitenzi ndani yake na kinachodhihirika ndani ya sentensi ya fulani. Msingi wa kishazi ni kuwepo kwa kitenzi ndani yake ambazo huweza kujisimamia au kuambatanishwa na kishazi kingine kuunda sentensi ya Kĩĩgembe.

Kulingana na Chomsky (1957), kishazi ni kipashio muhimu sana katika kujenga sentensi. Mwanaisimu anapochambua sentensi lazima akizingatie kipashio hiki kama kijenzi cha lazima cha sentensi. Uainishaji wa sentensi hufanywa kwa kuzingatia idadi na aina ya vishazi vinavyoijenga sentensi hiyo. Massamba na wenzake (1999) wameifasili dhana ya kishazi kama kundi la maneno lenye kirai nomino na kirai tenzi, hasa likiwa katika sentensi kuu. Kishazi ni kipashio cha kimuundo chenye neno moja au zaidi, kikubwa kuliko kirai kwani hapo awali ilielezwa kuwa kirai ndicho kipashio kinachounda kishazi. Kishazi huwa kidogo kuliko sentensi, chenye kitenzi ndani yake na kinachodhihirika ndani ya sentensi. Neno la msingi katika kishazi ni uwepo wa kitenzi ndani yake. Kwa mfano;

S56 Mwari ***awikûa*** na mûrano ( Kĩĩgembe)

Msichana ameolewa kwa harusi (Kiswahili)

S57 ***Mbenderîa*** miraa mûrûme (Kĩĩgembe)

Niuzie miraa bwana (Kiswahili)

S58 Mwari urîa ***ûraîkîrue*** nî ûmûthongi( Kĩĩgembe)

Msichana yule aliyeolewa ni mrembo (Kiswahili)

S59 Mûkûrû ***ararire*** iriû birori (Kĩĩgembe)

Mzee alikula ndizi zilizooza (Kiswahili )

S60 Tûkîmenyana kûîo, ***tûikania***(Kîîgembe)


Tungejuana mapema, tungeoana (Kiswahili)

S61 Ûkethirwa ûmwendete, ***ûkamwîra*** (Kîîgembe)


Ukiwa unampenda utamwambia (Kiswahili)

Vishazi hivi vinaweza kuwakilishwa kwa michoro ifuatavyo;


S56




S57



S58




Sentensi za S56 hadi S59 zimeundwa na vishazi. Maneno yaliyoandikwa kwa herufi za mlazo ndio msingi wa kishazi. Maneno haya yanaingia katika kategoria ya kitenzi.

Sentensi inaweza kuwa na kishazi kimoja au zaidi. Vishazi vinavyotoa taarifa inayojitosheleza huitwa vishazi huru (Obuchi na Mukhwana, 2015). Vishazi vingine ambavyo havitoi taarifa iliyo kamili huitwa vishazi tegemezi. Kishazi kiambatani kama kilivyofasiliwa na Massamba na wenzake(1999) ni kishazi ambacho kimeunganishwa katika sentensi kuu na kiunganishi. Kishazi hiki kina sifa kwamba kikiondolewa katika sentensi kuu husimama chenyewe kama sentensi inayojitegemea. Mfano;

S62 Mwana awîta kûtheeka mbûri na ina nîakûrua(Kîîgembe)

Mtoto ameenda kufunga mbuzi na mamake anapika (Kiswahili)


S63 Mwarimû nîakûritana îndî mûrîtwa nîakûmama(Kîîgembe)

Mwalimu anafunza lakini mwanafunzi analala (Kiswahili)


S64 Tûkîonana kûeo, ûîmbenderia mîraa(Kîîgembe)

Tungeonana mapema ungeniuzia miraa.

S62




S63




Tukichunguza mifano hapo juu tutabaini kuwa sentensi hizo zote ni changamano. Sentensi hizo zimeundwa kwa kishazi au vishazi tegemezi pamoja na kishazi huru. Sentensi hizo zina vipashio vinavyoshusha hadhi ya vipashio vinavyojenga sentensi. Vipashio hivyo ni pamoja na viambishi rejeshi, viunganishi tegemezi pamoja na viambishi vya masharti. Kila tungo ina vishazi viwili. Tungo la S62 mpaka S63 vishazi vyake ni huru kwa sababu hata vikiondolewa katika sentensi hizo na kuwekwa pekee yake bado maana yake itabaki. Vipashio hivyo, vikiondolewa kwenye sentensi kuu husimama na kuunda sentensi sahili. Hata hivyo, S64 iliundwa kwa vishazi viwili ambavyo kila kimoja kikiondolewa katika sentensi hakiwezi kusimama au

kujikamilisha kimaana. Kishazi tegemezi ni kishazi ambacho hakiwezi kusimama pekee kama sentensi mara tu kikiondolewa kutoka katika kishazi kinachokikamilisha katika muktadha wa sentensi ya Kîîgembe. Hiki ni kishazi ambacho hakijakamilika kimaana, yaani hakiwezi kujitegemea. Mtu anaposoma uhisi kuwa pana haja ya kuongezwa taarifa fulani ambayo haipo na inahitajika ili pawepo na maana kamili ya kishazi kitegemezi cha Kîîgembe. Maana yake, inakamilika pindi tu vishazi tegemezi vya Kîîgembe vinapohusishwa na vishazi vingine vinavyoandamana navyo katika muktadha wa Sentensi ya Kîîgembe.

### 5.2.1 Miundo ya Vishazi Tegemezi

Utafiti huu ulichanganua muundo wa sentensi ya Kîîgembe kwa kurejelea Nadharia ya Eksibaa. Kwa mujibu wa Nadharia ya Eksibaa vishazi huundwa kwa kuunganisha virai mbalimbali. Vishazi tegemezi huwakilishwa na vijalizo vya Kîîgembe kama vile *nkîthîrwa, nûntû bwa, kinya kwethîrwa, nî kenda, kethîrwa na rîrîa*. Vishazi tegemezi ambavyo vimeelezwa vilidhihirisha muundo wa sentensi ya Kîîgembe kwa kurejelea Nadharia ya Eksibaa.

#### 5.2.1.1 Vishazi tegemezi vyenye vitambulisho (nkîthîrwa)

Hivi ni vishazi tegemezi vinavyodokeza masharti yapasayo kutimizwa kabla kitendo hakijafanywa. Aidha, masharti haya huonyesha kuna uwezekano wa jambo fulani kufanyika au kutowezekana kwa jambo hilo. Kwa mfano,

S65 Nkîthîrwa ndî na mbesa nkîûra ngarî (Kîîgembe)

Ningekuwa na pesa, ningenunua gari ( Kiswahili)

Ningalikuwa na pesa ningalinunua gari ( Kiswahili)


S66 Nkîthîrwa ndî na kaana ngikaendia cukuru (Kîîgembe)

Ningekuwa na mtoto ningempeleka shuleni ( Kiswahili)


Ningalikuwa na mtoto ningalimpeleka shuleni ( Kiswahili)

Muundo huu wa kishazi tegemezi chenye kitambulisho *nkîthîrwa* kinaweza kuwasilishwa ifuatavyo

S65




S66




Michoro ya uwakilishi wa virai hivyo, inaonyesha muundo wa kirai tenzi na kirai kihusishi kinapotokea na kichwa cha kirai. RN ni dada ya H' wala si kijalizo cha H kwani RN inapanua H' hadi H'' na kisha kujipanua hadi kirai kamili. Katika mifano ya S65 sentensi hizo zinaonyesha uwezekano wa kuwa na pesa na kununua gari na kuna uwezekano wa kuwa na mtoto na kumpeleka shuleni. Hata hivyo, mifano ya S66 inaonyesha kwamba hakuna uwezekano wa kupata pesa na kununua gari na pia, hakuna uwezekano wa kuwa na mtoto na kumpeleka shuleni. Katika Kîîgembe ni tofauti na Kiswahili kwani kishazi tegemezi *nkîthîrwa* ndicho hutumika kuwakilisha dhana hizi mbili, yaani nge na ngeli.

**5.2.1.2 Vishazi vitegemezi vyenye vitambulisho (nûntû bwa)**

Vishazi hivi hueleza sababu ya kufanyika kwa kitendo. Kwa mfano,

S67 Nûntû bwa kûonoka kwake, mûtûmîria nîaakûmwenda (Kîîgembe)

Kwa sababu ya kuokoka kwake, mhubiri anampenda ( kiswahili)

S68 Aûtemwa na kîbanga, nûntû bwa kûiya (Kîîgembe)


Amekatwa kwa upanga kwa sababu ya wizi ( kiswahili)

S69 Nûntû bwa ûthongi bwake, akûona mûkûrû (Kîîgembe)

Kwa sababu ya urembo wake amepata mume ( kiswahili)

Muundo huu wa kishazi tegemezi chenye kitambulisho *nûntû bwa* unaweza kuwasilishwa ifuatavyo;

S67




Nadharia ya Eksibaa huongozwa na neno kuu katika kirai. Kirai husishi kimewakilishwa na kihusishi ambacho ni neno kuu. RT ni dada ya H'. Hii ni kwa sababu inapanua H' hadi H'' na baadaye H'' hujipanua hadi kirai kamili. Mifano ya S67- S69 imeonyesha mifano ya sentensi changamano ya Kîîgembe yenye kitambulisho *nûntû bwa*. Katika mifano ya S67 na S68 inaonyesha kuwa muundo wa kishazi tegemezi unaweza kutokea kwa (KN). Aidha, katika mfano wa S68 kishazi tegemezi kinatokea upande wa (KT). Hii ni kumaanisha kuwa, kishazi tegemezi cha sentensi changamano ya Kîîgembe kinaweza kutokea upande wowote wa sentensi yaani kwa (KN) au (KT).

**5.2.1.3 Vishazi vitegemezi vyenye vitambulisho (kinya kwethîrwa)**

Vishazi hivi hueleza hitilafu au doa iliyo katika jambo fulani. Aidha, kishazi tegemezi hiki huashiria kinyume cha jambo fulani licha ya masharti kutimizwa. Kwa mfano;

S70 *Kinya kwethîrwa nathomere na inya* atakûrukîre(Kîîgembe)

Ijapokuwa alisoma kwa bidii hakupita mtihani (Kiswahili)

S71 Akwoywa na mûrano *kinya kwethîrwa atînkanya* (Kîîgembe)


Ameolewa na harusi hata kama si mrembo (Kiswahili)

S72 *Kinya kwethîrwa arîmaa bwega mûno* aûkûa (Kîîgembe)

Ijapokuwa alikuwa analima vizuri sana amekufa (Kiswahili)

Muundo huu wa kishazi tegemezi chenye kitambulisho *kinya kwethîrwa* unaweza kuwasilishwa ifuatavyo;

S71




Hapo awali ilielezwa kuwa, neno la msingi katika kishazi ni kitenzi. Kishazi tegemezi cha Kîîgembe kinaweza kuandamana na aina yoyote ya kitenzi. Mifano yaa vishazi tegemezi iliyoandikwa kwa herufi za inaonyesha kuwa katika mfano wa S70 ulitumia kitenzi halisi huku mfano wa S71 ulitumia kitenzi kishirikishi kipungufu. Katika mfano wa S72, kishazi tegemezi kimeandamana na kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu. Kulingana na Nadharia ya Eksibaa kila kirai huongozwa na neno kuu ambalo ni kichwa. Vitenzi vikuu vinapotumika na vitenzi visaidizi hutekeleza kazi ya kujaliza kwani ndio hukamilisha kirai au neno kuu ambalo ni kitenzi kisaidizi.

**5.2.1.4 Vishazi vitegemezi vyenye vitambulisho (nî kenda)**

Vishazi hivi hueleza kusudi la kufanya jambo yaani madhumuni au shahaba ya kutekeleza jambo fulani. Kwa mfano:

S73 Nî kenda tuthiria kûrima nomwanka twîthirwe twî na inya (Kîîgembe)

Ili tumalize kulima lazima tuwe na bidii (Kiswahili)


S74 Akûrumîre nî kenda ûthûra (Kîîgembe)

Alikutusi ili ukasirike (Kiswahili)

S75 Enderie munda nî kenda athoma (Kîîgembe)

Aliuza shamba ili asome (Kiswahili)

Muundo huu wa kishazi tegemezi chenye kitambulisho *nî kenda* unaweza kuwasilishwa ifuatavyo;




Nadharia ya Eksibaa huwakilishwa na neno kuu ambalo linaweza kuwa, kitenzi, nomino, kielezi, kivumishi na kihusishi kwani ndilo hubeba sifa za kirai. Kwa hivyo, kirai kitakuwa na sifa za kategoria fulani ya neno ambalo ndicho kichwa au neno kuu la kirai hicho. Kielelezo cha matawi kilicho hapo juu kinaonyesha muundo wa kishazi tegemezi ulio na KH na RT. H na T vimejipanua hadi H' na T' kisha kujipanua zaidi hadi kirai kamili kwani hivi ni virai ambavyo vimeundwa na neno moja pekee yaani kitenzi na kihusishi.

**5.2.1.5 Vishazi tegemezi vyenye vitambulisho (kethîrwa)**

Vishazi hivi huonyesha masharti ambayo yanadhihirika. Vishazi hivi vimekitwa kwenye virai vya maneno kama vile kirai nomino au kirai tenzi. Kwa mfano,

S76 *Kethîrwa ûkarîma bwea* ûaketha maketha yamaingî (Kîîgembe)

Ikiwa utalima vizuri utapata mazao mengi (Kiswahili)

S77 Andeni mpempe *kethîrwa nibûkwenda wîta ûcetha* (Kîîgembe)

Pandeni mahindi kama mnataka kwenda kucheza (Kiswahili)

S78 *Kethîrwa ntongi* ntûthîrwa ndî na mwekûrû ûmwe (Kîîgembe)


Kama ningekuwa tajiri singekuwa na bibi mmoja (Kiswahili)

S79 *Kethîrwa ûkatiwa rikone* ûrue (Kîîgembe)

Kama utaachwa jikoni upike (Kiswahili

Muundo huu wa kishazi tegemezi chenye kitambulisho *kethîrwa* unaweza kuwasilishwa ifuatavyo;

S76




Hiki ni kishazi ambacho kimeundwa na KH na RT. Katika Nadharia ya Eksibaa, kirai huwakilishwa na neno kuu ambalo ni kihusishi na kitenzi katika kielelezo hiki. Kielezi ni dada ya kitenzi kwani kimetumika kujaliza kirai kitenzi. Sentensi za S76 – S79 zimeundwa na vishazi viwili kila moja. Vipashio vilivyoandikwa kwa hati za mlazo ni vishazi tegemezi. Hapo awali ilielezwa kuwa kishazi tegemezi hakiwezi kujisimamia bila kuwa na kishazi huru. Vishazi hivi vikiondolewa katika muktadha wa sentensi haviwezi kusimama pekee na kuleta maana iliyo kamili. Hivyo, vinaitwa vishazi tegemezi kwa kuwa maana ya sentensi zinazoundwa na vishazi hivi haipatikani pasipo na kuhusisha vishazi vingine (huru) vya Kîîgembe.

Hartman (1972) anaeleza kuwa, kishazi tegemezi ni kishazi kinachowasilisha utegemezi kwa kawaida kwa kutumia neno 'kama'. Platt (1971) naye anaeleza kuwa kishazi tegemezi ni mojawapo wa kishazi elezi kinachoanza kwa neno 'kama' au viunganishi vingine vilivyo na maana sawa na 'kama', ambapo hali fulani katika kishazi kimoja inategemea kitu fulani ambacho kinatajwa katika kishazi kingine

#### 5.2.1.6 Vishazi tegemezi vyenye vitambulisho (rîrîa)

Hivi ni vishazi tegemezi ambavyo huonyesha wakati. Vinatumika kueleza wakati jambo fulani lilipofanyika. Kwa mfano;

S80 *Rîrîa akinya nkeja* (Kîîgembe)

Atakapofika nitakuja (Kiswahili)

S81 *Ntîî aûntuma ndûkene kûûra ithûngû îndi rîrîa kacoka nkeya kûkûona* (Kîîgembe)

Mama amenituma dukani lakini nitakaporudi nitakuja kukuona (Kiswahili)

Kutokana na mifano yote ya vitambulishi vya vishazi tegemezi vya sentensi ya Kîîgembe, inabainika kuwa, sentensi changamano ya Kîîgembe ina miundo miwili. Muundo wa kwanza ni sentensi changamano iliyo na kishazi tegemezi kinachotokea upande wa kikundi nomino. Pili, ni kishazi tegemezi kinachotokea upande wa kikundi tenzi. Mifano mbalimbali ambayo ilichanganuliwa inathibitisha hayo.

### 5.2.2 Miundo ya Vishazi Huru

Vishazi huwa na muundo wa kikundi nomino na kikundi tenzi, hivyo huwa sawa kabisa kimuundo na sentensi. Tofauti baina ya kishazi na sentensi ni kwamba kishazi ni kiambajengo cha kuundia sentensi ilhali sentensi si kiambajengo cha kuundia kishazi. Vishazi huru ni vile ambavyo vinaweza kusimama pekee kama sentensi sahili. sentensi sahili za Kiswahili sanifu na sentensi sahili za lahaja ya Kipemba zinaundwa na kishazi ambatani kimoja tu. Ipo miundo kadhaa ya sentensi sahili za Kîîgembe. Muundo unaohusisha Kikundi Nomino na Kikundi Kitenzi [KN + KT] ndio muundo wa msingi wa sentensi ya Kîîgembe kikundi tenzi [KT] pekee ndiyo miundo mkuu wa sentensi sahili za Kîîgembe. Kuna miundo mingine kadhaa inayotokana na miundo miwili hii kama ilivyotolewa katika mifano:

S82 *Nîakûrima* (Kîîgembe)

Analima (Kiswahili)

S83 *Kaana kawîta ndûkene* (Kîîgembe)

Mtoto ameenda dukani (Kiswahili)


S44 *Ntîî awîta mundene.* (Kîîgembe)

Mama ameenda shambani (Kiswahili)


S85 *Arîtwa nîbakubuîthia kîerio* (Kîîgembe)

Wanafunzi wanafanya mtihani (Kiswahili)

S82




S83




Vishazi huru vya sentensi ya Kîîgembe vinaweza kuanishwa kwa njia mbalimbali; Kwa mfano;

**5.2.2.1 Kishazi huru chenve kitenzi kisoelekezi**

Kitenzi kisoelekezi ni kitenzi ambacho hakichukui kitendwa. Kitenzi kisoelekezi ni kile ambacho hakihitaji nomino ili kukamilisha maana katika sentensi. Kirai Kitenzi katika lugha ndicho kinachoweza kuonyesha kitenzi kuandamana au kutoandamana na nomino. Hivyo, inahitajika kuchunguza ni kwa namna gani Kirai kitenzi kinaweza kuonyesha uelekezi katika lugha mahususi. vitenzi visovielekezi hutegemea nafasi ambamo vishiriki vya pekee vya vitenzi hivi huingizwa kwenye muundo, huathiri uwezo wa vitenzi vya aina hii kuteua kitendwa. Vitenzi visovielekezi vishiriki ndani havina uwezo wa kuteua litendwa. Kwa upande mwingine, vitenzi visovielekezi vishiriki nje huweza kuchukua kitendwa kwa vile nafasi yake ya kijalizi cha KT

ambayo hujazwa na  kitendwa. Katika mifano ifuatayo kishazi huru kimekoleshwa rangi.


S86 Ntîî **nîakûthambi**a nyûmba na mûtanocia **akîcetha** (Kîîgembe)

Mama anaosha nyumba na kaka anacheza (Kiswahili)

S87 Mwarîmû nî **akûritana** kîracine (Kîîgembe)

Mwalimu anafunza darasani  (Kiswahili)

Katika mfano S86 kuna vishazi huru viwili ambavyo vimeunganishwa na kiunganishi cha kuongeza  na vishazi hivi vina miundo ifuatayo:




Katika vishazi hivi kuna virai nomino vilivyo na nomino pekee yaani. *ntîî,  mûtanocia na nyûmba*  ambavyo ni virai kamili. Isitoshe, katika mfano S87 kuna kirai nomino chenye nomino moja yaani *mwarîmû* kirai tenzi nî *akûritana* na kirai elezi ambacho ni *kîracine*. Haya yote ni maneno yanayojisimamia kama virai kamili. RN ni dada ya T’ wala si N’ kwa kuwa N’ si kijalizo cha T’. RN kinakamilisha T’ hadi T’’ hadi kirai kamili.

### 5.2.2.2 Kishazi huru chenye kitenzi elekezi

Kishazi chenye kitenzi ambacho ni elekezi ni kishazi ambacho hakiwezi kukamilika kimaana bila ya kuwa na kitendewa au mtendewa. Kwa mifano;


S88 Kaana kaala kamûrîmîre biakûrîa bîbîngî mûno (Kîîgembe)

Mtoto yule alimlia vyakula vingi sana (Kiswahili)

S89 Mûrîmî ûrîa amûrîmîre mûtûrî oke munda yuonthe (Kîîgembe)

Mkulima yule alimlimia jirani yake shamba lote (Kiswahili)

Muundo wa kishazi hiki unaweza kuwakilishwa kwa kielelezo kifuatacho;




*Mûrîmî ûrîa* *amûrîmîre mûtûrî oke* *mûnda yuonthe*


Virai hivi vitatu viliweza kuwakilishwa kwa neno kuu la kirai ambalo ni nomino, kitenzi na nomino. Virai hivi vimeweza kupanuliwa na dada kwani RN ya kwanza imepanuliwa na kivumishi *ûrîa* huku RT ikipanuliwa na mtendewa ambaye ni *mûtûrî oke* huku RN ya mwisho ikipanuliwa na *yuonthe*. Kwa kurejelea mfano S88 mtendewa inawakilishwa katika kitenzi. Vilevile KN cha kishazi hiki kimeundwa kutokana na kirai nomino kilicho na kibainishi na kirai nomino. Katika mfano S89 mtendewa ambaye ni *mûtûrî oke* iliweza kurejelewa na {mû}. Aidha, kuna kirai nomino chenye nomino na kitenzi pekee kwa mfano; *Mûrîmî ûrîa, mûtûrî oke amûrîmîre mûtûrî oke na mûnda yuonthe.*

**5.2.2.3 Kishazi huru kisicho na kikundi nomino**

Hapo awali tulieleza kuwa neno la msingi katika kishazi ni kitenzi. Hivyo ni kumaanisha kwamba kishazi kinaweza kuwa kimekamilika bila kuwa na nomino. Kwa mfano;

S90 Tûkathambie kûîo (Kîîgembe)

Tukaoshe mapema (Kiswahili



Kulingana na Nadharia ya Eksibaa, kirai huwakilishwa na neno kuu ambalo ni kichwa cha kirai. Kategoria ya maneno ambayo inaelezea sifa za kirai katika kirai tenzi hiki, mifano, KE ni dada ya T’ yaani ni kijalizo cha kirai kitenzi ambazo kinapanua T’ hadi T’’ na T’’ kujipanua hadi kirai kamili. Katika kishazi hiki cha S90, kikundi nomino sisi kimeachwa na kiwakilishi chake kuonyeshwa kwa kipatanishi wingi *{tû}* ya nafsi ya kwanza wingi. Aidha, kishazi hiki kina kirai elezi kilichoundwa na neno moja pekee yaani *kûîo*. Katika mfano S91, kiwakilishi kipatanishi ni {nî} cha nafsi ya kwanza umoja na vilevile kikundi nomino kilichoachwa kinawakilishwa na {nî} ambacho ni mimi. Katika mfano huu kuna kirai elezi ambacho ni *mûranûne*.

### 5.2.2.4 Kishazi huru chenye kitenzi kishirikishi

Katika Kîîgembe, kishazi huru kinaweza kujitokeza kuwa na aina mbili ya vitenzi vishirikishi, yaani kitenzi kishirikishi kikamilifu na kitenzi kishirikishi kipungufu. Vitenzi vishirikishi vikamilifu vya Kîîgembe ni vitenzi ambavyo huwa na viambishi vya nafsi, ngeli na wakati. Aidha, vitenzi vishirikishi vipungufu ni vitenzi ambavyo havina viambishi vya wakati na viambishi vya ngeli. Kwa mfano:

S92 *Mûrîmî **narî na** nthitangi.* (Kîîgembe)
Mkulima alikuwa na jembe (Kiswahili)

S93 *Ntîî **noo î** mundene na mwarocia nîakûanda mpempe*
(Kîîgembe)
Mama angali shambani na dadangu anapanda mahindi.
(Kiswahili)

S94 *Muwatî o mwana **nîabatîri** kûinîra mwaana* (Kîîgembe)
Mlezi wa mtoto anapaswa kuimbia mtoto. (Kiswahili)

S95 *Mûkoobi nîaîtue* (Kîîgembe)
Mkopaji yu mgonjwa (Kiswahili)


S96 *Mûrii jûî kwa mûkoke* (Kîîgembe)
Kamba iko kwa mkewe (Kiswahili)

S97 *Ngarî eke îî naiti ya kîrîma* (Kîîgembe)
Gari lake liko chini ya mlima. (Kiswahili)

S98 *Mwarîmû ûû nîwe mwea mûno* (Kîîgembe)
Mwalimu huyu ndiye mzuri sana . (Kiswahili)

Muundo wa kishazi hiki unaweza kuwakilishwa kwa kielelezo kifuatacho;

S97




Nadharia ya Eksibaa hueleza kipambanuzi kama kipashio kinachobeba maneno ambayo kimuundo si lazima yawepo katika kirai. Kuhusishwa kwa maneno hayo hukusudia tu kufafanua neno kuu. Aghalabu vivumishi ndivyo hutumiwa kama vipambanuzi katika virai nomino ilhali vielezi ndivyo hutumiwa kama vipambanuzi katika virai vitenzi. Katika mchoro huu wa uwasilishaji wa muundo wa kishazi chenye muundo wa kitenzi kishirikishi neno ‘eke’ limetumika kama kipambanuzi cha kupambanua kirai nomino.

Katika mifano ya vishazi huru S92 – S94, vitenzi ambavyo vimekoleshwa rangi ni vishrikishi vikamilifu. Hii ni kumaanisha kuwa sentensi sahili ya Kîîgembe inaweza kuundwa na KN na KT. Sentensi S92 ina virai nomino viwili ambavyo vimeundwa na nonimo pekee. Hivi ni *mûrîmî na nthitangi*. Mfano wa S92 ni sentensi ambatano ambayo inawasilisha mawazo mawili kuwa mama angali analima na dadangu anapanda mahindi. Kitenzi kishirikishi kikamilifu kikiandamana na kitenzi kingine katika lugha ya Kîîgembe hubadilika na kuwa kitenzi kisaidizi. Mifano ya S95 – S98 ni ya vitenzi vishirikishi vipungufu. Kama ilivyoelezwa hapo awali, vitenzi vishirikishi vya Kîîgembe havina viambishi vya wakati na ngeli. Katika mfano wa S97 kitenzi kishirikishi kipungufu kinaweza kuandamana na kirai husishi kama inavyoonekana kwa mchoro wa S97.

**5.2.2.5 Kishazi kilicho na kirai elezi**

Kishazi huru cha Kiigembe kinaweza kuwa na kirai elezi ambacho kinaweza kuwa cha namna halisi, namna ya mfanano, vielezi vya mahali na wakati. Kwa mfano:

S99 Mwarîmû akeya rûjû rûkîri (Kîîgembe)

Mwalimu atakuja kesho asubuhi (Kiswahili)

S100 Mwîti nawîta mpaala mûno(Kîîgembe)

Msafiri anatembea polepole sana (Kiswahili)

S101 Kîerio kîu ni kîkîûmû mûno (Kîîgembe)


Mtihani huo ni mgumu sana (Kiswahili)

S102 Mwacie akûendua cibitari (Kîîgembe)

Mgonjwa amepelekwa hospitali (Kiswahili)

S103 Mûrûgi nîakûitanga nyama na kacîû (Kîîgembe)

Mpishi anakatakata nyama kwa kisu (Kiswahili)




Kulingana na nadharia ya Eksibaa kirai elezi ni kirai ambacho neno lake kuu ni kielezi. Katika mifano hii, virai tenzi na virai vumishi vinafuatwa na vielezi kadha yaani, katika mfano S99 kuna kirai elezi *rûjû, rûkîri* cha wakati. Aidha, S100 kuna kirai elezi ambacho kimeundwa na kirai cha namna hali *mpaala* na kielezi cha namna halisi *mûno*. Katika mfano wa S102 kuna kirai elezi ambacho ni cha mahali yaani *cibitari*. Isitoshe katika mfano wa S103 kirai elezi ambacho kimetumika ni kielezi cha ala au kifaa. Mifano hii ilionyesha miundo ya sentensi sahili ya Kîîgembe.

**5.2.2.6 Kishazi huru kilicho na kirai kivumishi**

Kirai kivumishi ni kirai ambacho kinawakilishwa na sifa za neno kuu ambalo ni kivumishi. Aidha, kinatoa habari zaidi juu ya nomino au kirai nomino. Kirai-kivumishi ni kirai ambacho muundo wake umekitwa katika kivumishi. Kwa kawaida muundo huu huwa ni wa kivumishi na neno au fungu la maneno. Vishazi vilivyo na virai vivumishi vya Kîîgembe vinaweza kuwa na miundo mbalimbali. Kwa mfano;

S104 Mûiki ûmûthongi mûno aukuma kîûrûne (Kîîgembe)

Bi. harusi mrembo sana ameingia kanisani (Kiswahili)

S105 Mûrîtwa umwe aîna îûku rîa kûandîkîra kîerîo kîake (Kîîgembe)

Mwanafunzi mmoja ako na kitabu cha kuandikia mtihani wake. (Kiswahili)

S106 Ûria mûkûî ntîmwendete (Kîîgembe)

Yule mfupi simpendi. (Kiswahili)

S107 Mwarî ûmûkûrû mûno aîna nthoni (Kîîgembe)

Msichana mzee sana anaona haja (Kiswahili)

Katika mifano hii inadhihirisha kuwa muundo wa kishazi huru unaweza kujitokeza kama; virai vumishi ambavyo vimeundwa na kivumishi na kielezi, kivumishi pekee, au kivumishi na kivumishi kingine.

**5.2.2.7 Kishazi huru chenye kirai nomino**

Kulingana na Nadharia ya Eksibaa kirai Nomino hutawaliwa na neno kuu ambalo ni nomino au kiwakilishi chake. Neno kuu katika kirai ndilo huweza kubeba sifa za kirai kile. Kirai nomino cha Kîîgembe kina miundo mbalimbali kama vile;

1. Nomino kutanguliwa na kivumishi. Mfano;

S108 Ûû mwamba nimbi eyerete naa kwetû? (Kîîgembe)

Huyu mwizi anakujia nini huku kwetu? (Kiswahili)

S109 Ûrîa mwarî mûraya mûno atîkethacia antû (Kîîgembe)

Yule msichana mrefu sana hasalimii watu (Kiswahili)

2. Kivumishi kinaweza kuunganishwa pamoja na nomino. Mfano;

S110 Mwekûrû ûkû awîta ûtacia rûî (Kîîgembe)

Mke wako ameenda kuteka maji (Kiswahili)

S111 Nyûkwe endete sususu mûno Kîîgembe)

Mama yako anapenda umbea sana (Kiswahili)

3. Nomino inaweza kuandamana na vivumishi viwili

S112 Mûkûrû ûyû ûmûraya nî wetû (Kîîgembe)

Mzee huyu mrefu ni wetu. (Kiswahili)

S113 Munda yûrîa ywetû nî yûandî mûngao

Shamba hilo letu limepandwa maharage.

4. Kirai nomino kinaweza kuwa nomino pekee.

S114 Mûrogi aûkua (Kîîgembe)

Mrogi amekufa (Kiswahili)

S115 Cûkuru îkûruorwa (Kîîgembe)

Shule imefunguliwa (Kiswahili)

Mifano hii imetumika kuonyesha miundo mbalimbali ya kirai nomino cha sentensi ya Kîîgembe RN kimeundwa na N pekee, nomino na vivumishi viwili, kivumishi kilichounganishwa na nomino na nomino na kivumishi.

**5.2.3 Miundo ya Vishazi Viambatani**

Vishazi ambatani ni vishazi ambavyo vimeundwa na zaidi ya vishazi huru viwili au zaidi vilivyounganishwa na viunganishi. Ipo miundo kadhaa ya Vishazi Viambatani vya sentensi ambatano ya Kîîgembe. Vishazi viambatani vinatusaidia kubainisha miundo ya sentensi ambatano. Vishazi Viambatani vya sentensi ya Kîîgembe, vinaweza kuanishwa kwa njia mbalimbali; Kwa mfano;

**5.2.3.1 Vishazi viambatani vyenye muundo wa vishazi huru viwili na kiunganishi**

Sentensi ambatani za lahaja ya Kîîgembe zina miundo yenye kuhusisha vishazi viambatani viwili au zaidi. Vishazi hivyo huwekwa pamoja kwa kutumia viunganishi.

Miundo ya sentensi ambatani za lahaja ya Kipemba pia huhusisha sentensi sahili mbili au zaidi. Wakati mwingine sentensi sahili huungana na sentensi changamani. Ipo miundo ya sentensi ambatani inayohusisha sentensi changamani mbili au zaidi.

Uunganishaji huo ndio msingi wa sentensi ambatani. Kwa mfano;

S116 *Nakûrîma na kûanda* (Kîîgembe)

Analima na kupanda (Kiswahili)

S117 Mûritwa ûmûraya nîakûandika na mwarîmu akîritana (Kîîgembe)

Mwanafunzi mrefu anaandika na mwalimu anafunza (Kiswahili)

S118 Ntîî oke nî mwarîmu na îthe oke nî mûrîmi (Kîîgembe)


Mama yake ni mwalimu na baba yake ni mkulima (Kiswahili)

Ukichunguza kwa makini sentensi za hapo juu utaona kuwa ndani ya kila sentensi kuna vitenzi vikuu viwili. Vitenzi hivyo ndivyo vinavyounda vishazi ambatano vya sentensi hizo. Kishazi kilichokaa mwanzo wa sentensi kinasimamia upatanisho wa

kisarufi katika sentensi husika. Baadhi ya wataalamu wamezichambua sentensi za aina hii kama zichambuliwavyo sentensi sahili.

Muundo wa vishazi viambatani unaweza kuwasilishwa kwa mchoro ufuata

S116




Kulingana na Nadharia ya Eksibaa kila kirai huwakilishwa na neno kuu. Kichwa cha kirai ambacho ni neno kuu la kirai huweza kuwa neno moja ambalo hubeba sifa kuu za kirai. Aidha, virai hivi vyote, kipashio muhimu na cha lazima ni kichwa cha kirai. Vipashio vingine vyote ni huria (si vya lazima). Nadharia ya Eksibaa inaongozwa na dhana ya neno kuu (kichwa) katika kirai na uhusiano wake na vipengele vingine katika kuunda kirai. Virai vilivyo katika kielelezo S116 vimewasilishwa na neno kuu tu.

Mifano hii inathibitisha muundo wa kirai ambacho kimeundwa na neno moja ambalo ni kitenzi cha pekee. Mifano ambayo imetolewa inathibitisha kuwa sentensi ya Kîîgembe ina muundo wa sentensi ambayo ina vishazi viambatani ambavyo vina vishazi huru viwili S116 – S118. Kwa mfano; S116 vishazi huru vimetumika viwili ambavyo ni; *nakûrîma* na *kûanda*. Aidha, Obuchi na Mukhwana (2010) anasema kuwa, sentensi changamano inaweza kuwa na kishazi huru kimoja au zaidi.

#### 5.2.3.2 Vishazi viambatani vyenye muundo wa zaidi ya vishazi huru viwili


S119 Nîbendete kûrîma na kûanda (Kîîgembe)

Ninapenda kulima na kupanda (Kiswahili)

S120 Baîyîre na babunjia nyûmba na bayûkîa into bionthe (Kîîgembe)

Waliiba na kuvunja nyumba na kuchukua kila kitu (Kiswahili)

S119




Kulingana na Nadharia ya Eksibaa, mahali ambapo kirai kinatokea lazima kuwe na kategoria ya leksia. Kategoria hizi za maneno ndizo hubeba sifa za kirai. Kwa mfano, kitenzi katika RT kwa kurejelea kielelezo cha S119. Hii ni kumaanisha kuwa, kila kunapotea kirai kitenzi lazima kuwepo na kitenzi jinsi ambavyo imewasilishwa na S119. Nadharia ya Eksibaa huongozwa na kichwa ambacho ni neno kuu la kirai ambalo ni kitenzi katika mfano wa S119.


**5.2.3.3 Vishazi viambatani vyenye vishazi huru na tegemezi**

S65 Nkîthîrwa ndî na mbesa kîûra ngarî (Kîîgembe)

Ningekuwa na pesa , ningenunua gari ( Kiswahili)

S66 Nkîthîrwa ndî na kaana ngikaendia cukuru (Kîîgembe)

Ningekuwa na mtoto ningempeleka shule ( Kiswahili)



Nadharia ya Eksibaa huwakilishwa na neno kuu ambalo linaweza kuwa, kitenzi, nomino, kielezi, kivumishi na kihusishi kwani ndio hubeba sifa za kirai. Kwa hivyo, kirai kitakuwa na sifa za kategoria fulani ya neno ambalo ndilo kichwa au neno kuu la kirai hicho. Kielelezo cha matawi kinaonyesha muundo wa sentensi yenye kishazi tegemezi na kishazi huru. Kwa mifano ambayo ilitumika kutoka S65 – S66. Kwa mfano; vishazi huru katika hizi sentensi ni kama zifuatazo; *kîûra ngarî na ngikaendia cukuru*. Vishazi tegemezi ni kama vile; *ûkîthîrwa waandire, nkîthîrwa ndî* na *mbesa na nkîthîrwa ndî na kana.*

Vishazi viambatani kama vilivyoelezwa hapo awali vilisaidia kuchanganua miundo ya sentensi ambatano ya Kîîgembe. Vishazi viambatani vina miundo ifuatayo; vishazi huru viwili na kiunganishi, vishazi vyenye muundo wa zaidi ya vishazi huru viwili na vishazi vyenye vishazi huru na tegemezi.

**5.3 Hitimisho**

Katika Sura ya Tano utafiti huu ulichanganua miundo ya sentensi ya Kîîgembe kwa kufafanua muundo wa kishazi. Aidha, utafiti huu ulieleza aina ya vishazi katika sentensi ya Kîîgembe na kubaini kuwa kuna aina tatu za vishazi ambavyo ni; vishazi huru, vishazi tegemezi na vishazi viambatani. Mtafiti alichanganua muundo wa sentensi changamano ya Kîîgembe kwa kuangazia vishazi tegemezi vyenye vitambulisho mbalimbali. Isitoshe, utafiti huu ulionyesha miundo ya sentensi sahili ya Kîîgembe kwa kuchanganua miundo ya kishazi huru. Tulieleza hapo awali kuwa, sentensi za Kiswahili zinaundwa na vipashio anuai vinavyobainika katika ngazi tofauti. Mofu hujenga neno, maneno hujenga virai, virai hujenga vishazi na vishazi hujenga sentensi ila katika kazi hii tumeangazia vipashio viwili tu, yaani virai na vishazi. Inapaswa ieleweke kwamba maelezo haya yalitumika kama msingi wa uchambuzi na ufafanuzi wa Nadharia za Eksibaa ambayo uonyesha muundo wa viambajengo vya sentensi.

Vilevile, utafiti ulionyesha miundo ya sentensi ambatano kwa kurejelea miundo mbalimbali ya vishazi viambatani. Mtafiti alifafanua muundo wa sentensi za Kîîgembe kwa kurejelea uhusiano na mpangilio wa viambajengo vya sentensi kulingana na Nadharia ya Eksibaa. Hata hivyo, sentensi ya Kîîgembe huundwa kwa

mpangilio maalumu ila si kupachika maneno tu. Uhusiano wa viambajengo hivi ndio hufanikisha miundo mbalimbali ya sentensi ya Kîîgembe. Kutokana na matokeo hayo, miundo ya vishazi katika lahaja ya Kîîgembe inaonekana kufanana kwa kiasi fulani na miundo ya vishazi katika Kiswahili. Mfano, katika Kiswahili kuna vishazi tegemezi, vishazi huru na vishazi ambatani. Ila vitambulisho vinavyotambulisha vishazi tegemezi vya Kîîgembe ni tofauti na za Kiswahili. Kwa mfano, *nkîthîrwa* ni kishazi kinachosimamia dhana mbili za vishazi tegemezi vya Kiswahili yaani 'nge' na 'ngeli'. Hata hivyo, vishazi tegemezi vingi vya Kîîgembe vinafanana na vishazi vya Kiswahili. Hali hii inaonyesha kuwa inawezekana muundo wa vishazi katika lugha mbalimbali za Kibantu unafanana.

# SURA YA SITA
# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

## 6.1 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kuchunguza muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe. Malengo yalikuwa mawili, ambayo ni; kueleza miundo ya virai na kufafanua miundo ya vishazi. Muundo wa utafiti uliotumika ulikuwa wa kimaelezo katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data. Pia utafiti huu ulifanyika katika maeneo tawala matatu nayo ni Laare, Maua na Mûrîngene. Walengwa wa utafiti walikuwa ni wakaazi wote wa Igembe ambao ni watumiaji wa asili wa lahaja ya Kĩĩgembe. Kati yao walioteuliwa ni walengwa (30) ambao ni watu kumi wa kwanza kuhojiwa katika kila eneo. Watu hawa ndio waliotumika kama sampuli ya washiriki wa utafiti huu.

Data ya sentensi ya Kĩĩgembe ilizalishwa na mtafiti kwa kuwa mzawa wa Kĩĩgembe na pia kutafitiwa nyanjani. Data za sentensi ya Kĩĩgembe iliweza kuchanganuliwa kwa kutumia mtindo wa maelezo. Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Eksibaa. Maadili ya kiutafiti yalizingatiwa, ambayo ni pamoja na kupata kibali cha kufanya utafiti, kujadiliana na kundi lengwa ili kuepukana na matatizo ya upendeleo, kuwa wazi katika utafiti ili kupata taarifa kwa urahisi, kulinda haki za watu vilevile faragha na usikivu, kuheshimu usiri wa wale waliohusika katika utafiti na kuweka siri zao.

Kutokana na utafiti huu ilibainika kuwa, Kĩĩgembe kina aina tano ya virai ambavyo ni virai nomino, virai vielezi, virai vitenzi, virai vivumishi na virai vihusishi. Utafiti huu ulichanganua muundo wa sentensi ya Kĩĩgembe kwa kuangazia virai vyenye miundo ifuatayo; Kirai nomino cha nomino moja pekee, kirai nomino cha nomino na kishazi tegemezi, kirai nomino cha nomino na kivumishi, kirai nomino cha kiwakilishi pekee, Kirai nomino chenye muundo wa kiwakilishi na kivumishi, kirai nomino chenye muundo wa kitenzijina na kirai nomino chenye nomino mbili. Aidha, utafiti ulieleza miundo ya virai vivumishi kwa kuonyesha miundo mbalimbali kama vile kirai kivumishi chenye kivumishi pekee, muundo wa kirai kivumishi chenye muundo wa zaidi ya kivumishi kimoja, kirai kivumishi chenye kivumishi na kielezi na kirai kivumishi chenye kivumishi na nomino.

Aidha, utafiti ulifafanua miundo ya virai elezi na kuonyesha kuwa virai elezi vya Kîîgembe vinaweza kujitokeza na miundo ifuatavyo; kirai kielezi chenye kielezi pekee na kirai kielezi chenye kielezi zaidi ya kimoja. Katika miundo ya virai husishi. utafiti huu ulibainisha kuwa Kîîgembe kina virai husishi vyenye kihusishi na kielezi na kirai husishi chenye muundo wa kihusishi na nomino. Kwa upande mwingine, virai vitenzi vilijitokeza na miundo ifuatayo; kirai kitenzi chenye kitenzi halisi pekee, kirai kitenzi chenye muundo wa kitenzi na kielezi na kirai kitenzi chenye muundo wa vitenzi viwili. Aidha, kirai nomino cha Kîîgembe kiliwakilishwa na vipengele vinane vifuatavyo; nomino moja pekee, nomino na kivumishi, kiwakilishi na kivumishi, kiwakilishi pekee, nomino na kishazi tegemezi, kitenzijina na kivumishi, kitenzijina pekee na nomino, kivumishi na kishazi tegemezi vumishi.

Vilevile, utafiti huu ulifafanua aina ya vishazi katika sentensi ya Kîîgembe na kubaini kuwa kuna aina tatu ya vishazi ambavyo ni; vishazi huru, vishazi tegemezi na vishazi viambatani. Vishazi tegemezi vya Kîîgembe huwakilishwa na vitambulisho vifuatavyo; *nkîthîrwa, nûntû bwa, rîrîa, kinya kwethîrwa, nî kenda na kethîrwa.* Aidha, ilibainika kuwa vishazi tegemezi vikikamilishwa na vishazi huru vya Kîîgembe kuunda sentensi changamano ya Kîîgembe.

Ilibainika kuwa, kishazi tegemezi cha Sentensi changamano ya Kîîgembe kinaweza kutokea upande wa kikundi nomino au upande wa kikundi tenzi. Miundo ya sentensi sahili ya Kîîgembe ilibainika ni pamoja na; sentensi sahili ya kitenzi pekee, kikundi nomino na kikundi tenzi au kikundi tenzi pekee.

Vilevile, utafiti huu ulionyesha miundo ya sentensi ambatano kwa kurejelea miundo mbalimbali ya vishazi viambatani. Kutokana na miundo ya vishazi viambatani sentensi ambatano ya Kîîgembe ina miundo ifuatayo; sentensi ambatano yenye muundo wa vishazi huru viwili na kiunganishi, yenye muundo wa zaidi ya vishazi huru viwili na yenye vishazi huru na tegemezi. Mtafiti alibainisha muundo wa sentensi za Kîîgembe kwa kurejelea uhusiano na mpangilio wa viambajengo vya sentensi kulingana na Nadharia ya Eksibaa kupata kwamba, sentensi ya Kîîgembe huundwa kwa mpangilio maalumu ila si kupachika maneno tu. Uhusiano wa viambajengo hivi ndio hufanikisha miundo mbalimbali ya sentensi ya Kîîgembe.

## 6.2 Hitimisho

Kulingana na utafiti huu, kuna mambo mbalimbali ambayo utafiti ulihitimisha kwa kuzingatia muundo wa sentensi ya Kîîgembe. Kila sentensi ya Kîîgembe huundwa kwa sehemu mbili za msingi yaani kikundi nomino na kikundi tenzi. Sehemu hizi mbili za sentensi ya Kîîgembe huwa na visehemu vyake vidogo. Hata hivyo, utafiti huu ulijishughulisha na aina za virai na vishazi katika uundaji wa sentensi ya Kîîgembe. Utafiti huu ulibaini aina tano za virai vya Kîîgembe ambavyo ni, virai nomino, virai tenzi, virai vivumishi, virai husishi na virai vielezi. Aidha, ilibainika kuwa, vishazi vya Kîîgembe ni vya aina tatu vikiwemo vishazi huru, vishazi tegemezi na vishazi viambatani. Kutokana na matokeo hayo, miundo ya virai na vishazi katika lahaja ya Kîîgembe inaonekana kufanana kwa kiasi fulani na miundo ya virai na vishazi katika Kiswahili. Kwa mfano, katika Kiswahili kuna RN, RT, KV, KH na KE. Aidha, kuna vishazi tegemezi, vishazi huru na vishazi ambatani. Ila vitambulisho vinavyotambulisha vishazi tegemezi vya Kîîgembe ni tofauti na vya Kiswahili. Kwa mfano, *nkîthîrwa* ni kishazi kinachosimamia dhana mbili za vishazi tegemezi vya Kiswahili katika Kîîgembe yaani 'nge' na 'ngeli'. Hata hivyo, vishazi tegemezi vingi vya Kîîgembe vinafanana na vishazi vya Kiswahili. Hali hii inaonyesha kuwa inawezekana muundo wa virai na vishazi katika lugha mbalimbali za Kibantu unafanana.

## 6.3 Mapendekezo ya Utafiti wa Baadaye

Kutokana na upeo wa utafiti huu, utafiti wa baadaye unaweza kufanywa kuhusu mambo yafuatayo;

i Tafiti za baadaye zinaweza kufanywa kuonyesha ulinganisho baina ya sentensi ya Kîîgembe na sentensi ya Kiswahili sanifu.

ii Tafiti za baadaye vilevile, zinaweza kufanywa kuhusu muundo wa lahaja zingine za Kimeru kama vile, Kitigania na Kiigoji .

iii Tafiti fuatishi zinaweza kuhusu mofosintaksia ya Kîîgembe kwa kurejelea Nadharia kama vile Uminimalisti.

## MAREJELEO


Besha, R. M. (1994). *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Dar es Salaam: Macmillan Aidan Ltd.

Chomsky, N. (1957). *Syntactic Structures.* The Hague: Muoton.

Chomsky, N. (1970). *Aspect of the Theory of Syntax. Cambridge:* MIT Press

Chomsky, N. (1986*). Knowledge of Langauge, Its Nature, Origin and Age.* New York: Praeger.

Cowper, E. (1992). *A Concise Introduction to Syntactic Theory:The Government-Binding Aproach:* Chicago, The University of Chicago Press .

Fromkin, V. (1974*). An Introduction to Language*. New York: Holt, Rinehart and Winston, Inc.

Fromkin, V. (2000*). Linguistics: An Introduction to Linguistics Theory*. Blackwell Publishers Inc. Malden, USA: Massachussetts.

Guthrie, M. (1948). *The Classification of Bantu Langauges*: Oxford University Press.

Habwe, J. na Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili* Nairobi: Phoenix Publishers.

Hartman, R.K (1972). *Dictionary of Language and Linguistics*. London: Longman Inc.

Harley, H. (1995) *Abstracting Away From Abstract Case.* In J. Berkman (ed), Proceedings of Nels 25, GLSA, Amherst, pp 207- 221

Jackendoff, R. S. (1977). *Syntax: A Study of Phrase Structure*. Cambridge, Mass. MIT Press

Jerono, P. (2003). Kishazi Huru Arifu cha Kiswahili: Mtazamo wa x-baa. (Tasnifu ya Uzamili haiyachapishwa) Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Kanake, J. (2013). Makosa ya Kifonolojia Miongoni mwa Wanafunzi wa Kiigembe katika Ujifunzaji wa Kiswahili; *(*Tasnifu ya Uzamili haiyachapishwa) Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Khamisi, A. A. (2011). *Uchambuzi wa Kiswahili Fasaha: Sarufi na Lugha*, Zanzibar: Chuo Kikuu cha Elimu Chukwani.

Khamis, A. M. na Kiango, J. G. (2002), Uchanganuzi wa Sarufi ya Kiswahili, Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Kapinga, M. C. (1983). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu.* Dar es Salaam. TUKI.

Kirimi, N. (2016). Uchanganuzi wa Makosa ya Kifonolojia na Kimofolojia yanayojitokeza katika kazi za Wanafunzi wa Tigania (Tasnifu ya uzamili haiyachapishwa) Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kobia, J. M. (2008). Taswira za Kiuana katika Nyimbo za Tohara za Wanaume Miongoni mwa Waigembe, (Tasnifu ya Uzamili haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Koech, L. (2013). Sintaksia ya Kijalizo cha Kiswahili Sanifu: Mtazamo wa x-baa. (Tasnifu ya Uzamili haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kothari, C. R. (1990). *Research Methods: Techniques and Procedures*, (Toleo la pili), New Delhi: New Age International (P) Limited Publishers.

Kothari, C.R. (2009). *Research Methodology. Methods and Techniques* (Toleo la pili), New Delhi: New Age International (P) Limited Publishers.

Leffel, K. na Bouchard, D. (1991). *Views on Phrase Structure Kluwer Academic* Publishers, Dordrecht, The Nertherlands.

Lyons, J. (1986). *Introduction to Theoretical Linguistics*. London: Cambridge University Press. Katika Lappin, S.(Mhr). *The handibook of contemporary semantic theory*. Oxford Cambridge,MA: Blackwell.

Mathews, P.H. (1997). *A Concise Dictionary of Linguistics* Oxford: Oxford University Press

Maringah, E. (1987). Muundo wa Kitenzi cha Kimbeere. (Tasnifu ya Uzamili haiyachapishwa) Chuo Kikuu cha Egerton.

Massamba, D.P.B. na wenzake (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu* (SAMIKISA). *Sekondari na Vyuo*, Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Massamba, D.P.B. na wenzake (2009). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dares Salaam. TUKI.

Mbaabu, I. (1991). *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili.* Nairobi: Longman.

Mbaka, H. M. (2013). Phrase Structure of Gichuka. (Unpublished M.A Thesis). Chuka University.

Mkude, J. J. D. (1983). Uchanganuzi wa Sentensi za Kiswahili: Dar es Salaam: TUKI

Mukuthuria, M. (1997). Njeo katika Kitenzi cha Kitigania. Tasnifu ya Uzamili katika Kiswahili, [haijachapishwa] Chuo Kikuu cha Egerton.

Mukuthuria, M. 2004. Kuathiriana kwa Kiswahili na Kimeru: Mfano Kutokana na Wanafunzi wa Tigania. PhD Thesis: Chuo Kikuu cha Egerton.

Ndwiga, M.S. (2008). A Syntactical Examination of Empty Categories in the Syntax of Gichuka: Government and Binding Perspective (Unpublished M.A Thesis) University of Nairobi.

Neekemiah, N. R. (2010). Noun Phrase Structure in Kihangaza. (Unpublished M.A Thesis) University of Dar es Salaam.

Newmeyer, F. J. (1986). *Linguistic Theory in America* 7th Edition Orlando: Academic Press Inc. Chicago University Press.

Njogu, K., Mwihaki, A. na Buliba, A. (2006). *Sarufi ya Kiswahili*: *Uchanganuzi na Matumizi.* Nairobi*:* Jomo Kenyatta Foundation.

Obuchi, S na A. Mukhwana (2015). *Muundo wa Kiswahili: Ngazi na Vipengele.* Jomo Kenyatta Foundation.

Omusula, F. B (1998). Ulinganishi wa Mifanyiko ya Kimofolojia Baina ya Mnyambuliko wa Kitenzi cha Kiswahili na cha Kikabarasi. (Tasnifu ya Uzamili haiyachapishwa) Chuo Kikuu cha Nairobi

Platt, J.T. (1971). *Grammatical Form and Grammatical Meaning: A Tagmemic View of Fillmore's Deep Structure Case Concepts*. Amsterdam and London: North Holland

Radford, A. (1981). *Transformaional Syntax.* Cambridge: Cambridge University Press.

Radford, A. (1988). *Transformational Grammar.* Cambridge: Cambridge University Press

Rubanza, Y. I. (2003). *Sarufi: Mtazamo wa Kimuundo,* Dar es Salaam. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Taitumu, B. (2014). Kimeru Word-Formation Processes. (Unpublished M.A Thesis) University of Nairobi.

Walliman, N. (2011). *Research Methods: The Basic,* London & New York: Routledge Taylor & Francis Group

Wesana-Chomi, E. (2017). *Kitangulizi cha Muundo Viambajengo wa Sentensi za Kiswahili.* Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

## KIAMBATISHO I: TAKWIMU ZA TASNIFU

Jumla ya maneno…………………………………………………….24,196

Kurasa (zikiondolewa za mwanzo, marejeleo na viambatisho)………… 82

Jumla ya sentensi zilizochanganuliwa……………………………..………120

\

## KIAMBATISHO 2: SENTENSI YA KIIGEMBE

S1 Ntîî awîta ndukene (Kîîgembe)
Mama ameenda dukani (Kiswahili)

S2Mûrîmî nîakûrîma (Kîîgembe)
Mkulima analima ( Kiswahili)

S3 Mûrîtwa ûmûraya nîakwandîka (Kîîgembe)
Mwanafunzi mrefu anaandika ( Kiswahili)

S4 Mwaana ûû nî mwathîki (Kîîgembe)
Mtoto huyu ni mtiifu ( Kiswahili)

S5 Nthaka înthongi nîkûrîma mundene ( Kîîgembe)
Ghulamu mtanashati analima shambani ( Kiswahili)

S6 Ntîî nîakurua irio akîthambia cûlia (Kîîgembe)
Mama anapika huku akiosha sufuria ( Kiswahili )

S7 Mwarimû nîakûritana bwea mûno( Kîîgembe)
Mwalimu anafunza vizuri sana ( Kiswahili)

S8 Ûrîa mwini wa rwîmbo kuuma Mutuati. (Kîîgembe )
Yule mwimbaji wa wimbo kutoka Mutuati. (Kiswahili)

S9 Mwarimû nîakûritana (Kîîgembe)
Mwalimu anafundisha (Kiswahili)

S10 Ngûkûû îrîa îrareterwe îoro îukua (Kiigembe)
Kuku aliyeletwa jana amekufa( Kiswahili)

S 11Mwaana ûmûkuî aûkûlûka ( Kiigembe )
Mtoto mfupi amepita ( Kiswahili)

S12 Johana nî ûria mûrîmi wa mpempe. ( Kîîgembe)
Johana ni yule mkulima wa mahindi ( Kiswahili)

S13 Mwarîmû nî ûrîa mûkuî mûno (Kîîgembe)
Mwalimu ni yule mfupi sana ( Kiswahili)

S14 Mwarîmû ûyû nîakuritana aritwa baake.( Kîîgembe)
Mwalimu huyu anafunza wanafunzi wake ( Kiswahili)

S15 Mwarî ûrîa mwikumia aûkoloma ( Kîîgembe)
Msichana yule mwenye maringo ameketi (Kiswahili)

S16 Mûritwa ûmûraya akwîja (Kîîgembe)
Mwanafunzi mrefu amefika( Kiswahili)

S17 Mwekûrû ûyû mûkuî endete kûrîma rûkîrî mûno (Kiigembe)
Mama huyu mfupi anapenda kulima asubuhi sana Kiswahili

S18  Mûritwa awîta cûkûru   (Kîîgembe)
Mwanafunzi ameenda shule.(Kiswahili)

S19 Ntîî nîakûrimira mwarocia (Kîîgembe)
Mama anamlimia dadangu (Kiswahili)

S20  Nîwe ûkareta mûîkania  (Kîîgembe)
Wewe utaleta bwana harusi  (Kiswahili)

S21 Mûiki ûrîa ûraikîrue îoro nî ûmûnthongi  (Kîîgembe)
Bibi arusi aliyeolewa jana ni mrembo  (Kiswahili)

S22 Miraa îria îraûrîrwe îoro nî yeetû  (Kîîgembe)
Miraa iliyonunuliwa jana ni yetu (Kiswahili)

S23 Mûate yûrîa yûraûrîrwe yûkûthûka  (Kîîgembe)
Mkate ulionunuliwa umeharibika (Kiswahili)

S24 Mûate yûû nî yûmwea (Kîîgembe)
Mkate huu ni mzuri (Kiswahili)

S25 Mwekûrû ûyû ûmûraya akûra munda? (Kîîgembe)
Mama huyu mrefu amenunua shamba? (Kiswahili)

S26 Maûta yakwa yakûthira (Kîîgembe)
Mafuta yangu yameisha (Kiswahili

S27 Wee nîakûthambîa mwaana (Kîîgembe)
Yeye anaosha mtoto (Kiswahili)

S28 Kîî kîkûrîrwa mûrîtwa (Kîîgembe)
Hiki kimenunuliwa mwanafunzi (Kiswahili)

S29 Yûû mûraya yûatemwa (Kîîgembe)
Huu mrefu utakatwa (Kiswahili)

S30  Yaa maîngî nî yaû ?(Kîîgembe)
Haya mengi ni ya nani? (Kiswahili)

S31  Kîî kînene kîatûka nîkîetû (Kîîgembe)
Hiki kikubwa kimevunjika ni chetu  (Kiswahili)

S32 Kûtheka kûkatûwîrîa mûno (Kîîgembe)
Kucheka kutatufurahisha sana (Kiswahili)

S33 Kûîna nîkûkwea (Kîîgembe)
Kuimba ni kuzuri (Kiswahili)

S34 Kûîna kwake nîkûtûwîria (Kîîgembe)
Kuimba kwake kunafurahisha (Kiswahili)

S35 Kûcetha kûû tî kûkwea (Kîîgembe)
Kucheza huku si kuzuri (Kiswahili)

S36 Kûthoma kwake nî kwakûrîarania (Kîîgembe)
Kusoma kwake ni kwa kushangaza (Kiswahili)

S37 Mwekûrû o mûthoi nî ûyû (Kîîgembe)
Mke wa msasi ni huyu (Kiswahili)

S38 Mûwati o mwana awîta (Kîîgembe)
Mlezi wa mtoto ameenda (Kiswahili)

S39 Mwarîmû o twana nîaûtûrîtana (Kîîgembe)
Mwalimu wa watoto anafunza (Kiswahili)

S40 Mûrîtwa ûmuraya ûmûthongi aûkîruka kîerîo.(Kîîgembe)
Mwanafunzi mrefu mrembo amepita mtihani (Kiswahili)

S41 Mwana ûmûkuî mûno nîakûrîra (Kîîgembe)
Mtoto mfupi sana analia (Kiswahili)

S42 Mwarîmû ûmûme mûno nîakûandîka (Kîîgembe)
Mwalimu mwerevu sana anaandika (Kiswahili)

S43 Mwekûrû wa îtonga akwîja (Kîîgembe)
Mke wa tajiri amekuja (Kiswahili)

S44 Ntîî awîta mundene (Kîîgembe)
Mama ameenda shambani (Kiswahili)

S45 Mwarîmû akûritana bwea mûno (Kîîgembe)
Mwalimu amefunza vizuri sana (Kiswahili)

S46 Mpempe cia mûndene ikûma (Kîîgembe)
Mahindi ya shambani yamekauka (Kiswahili)

S47 Aini ba kanicene bakwiya (Kîîgembe)
Waimbaji wa kanisani wamefika (Kiswahili)

S48 Biakûrîa vya ngûûkû bîkûya (Kîîgembe)
Vyakula vya nyanya vimeiva (Kiswahili)

S49 Kîratû kîa mûranû nî kîthongî (Kîîgembe)
Kiatu cha harusi ni kizuri (Kiswahili)

S50 Akûwa (Kîîgembe)
Ameanguka (Kiswahili)

S51 Nîakûthoma (Kîîgembe)
Anasoma (Kiswahili)

S52 Mwarîmû akûrîtana mûno (Kîîgembe)
Mwalimu amefunza sana (Kiswahili)

S53 Munda niyûkûrîmîka bwea (Kîîgembe)
Shamba linalimika vizuri (Kiswahili)

S54 Ndamûtîrîmîre akinaa (Kîîgembe)
Nilimkuta akiimba (Kiswahili)

S55 Noo akûthamba (Kîîgembe)
Angali anaoga (Kiswahili)

S56 Mwari awikûa na mûrano ( Kîîgembe)
Msichana ameolewa kwa harusi (Kiswahili)

S57 Mbenderîa miraa mûrûme (Kîîgembe)
Niuzie miraa bwana (Kiswahili)

S58 Mwari urîa ûraîkîrue nî ûmûthongi( Kîîgembe)
Msichana yule aliyeolewa ni mrembo (Kiswahili)

S59 Mûkûrû ararire iriû birori (Kîîgembe)
Mzee alikula ndizi zilizooza (Kiswahili )

S60 Tûkîmenyana kûîo, tûikania(Kîîgembe)
Tungejuana mapema, tungeoana (Kiswahili)

S61 Ûkethirwa ûmwendete, ûkamwîra (Kîîgembe)
Ukiwa unampenda, utamwambia (Kiswahili)

S62 Mwana awîta kûtheeka mbûri na ina nîakûrua(Kîîgembe)
Mtoto ameenda kufunga mbuzi na mamake anapika (Kiswahili)

S63 Mwarimû nîakûritana îndî mûrîtwa nîakûmama(Kîîgembe)
Mwalimu anafunza lakini mwanafunzi analala (Kiswahili)

S64 Tûkîonana kûeo, ûîmbenderia mîraa(Kîîgembe)
Tungeonana mapema ungeniuzia miraa.

S65 Nkîthîrwa ndî na mbesa nkîûra ngarî (Kîîgembe)
Ningekuwa na pesa, ningenunua gari ( Kiswahili)
Ningalikuwa na pesa ningalinunua gari ( Kiswahili)

S66 Nkîthîrwa ndî na kaana ngikaendia cukuru (Kîîgembe)
Ningekuwa na mtoto ningempeleka shuleni ( Kiswahili)
Ningalikuwa na mtoto ningalimpeleka shuleni ( Kiswahili)

S67 Nûntû bwa kûonoka kwake mûtûmîria nîaakûmwenda (Kîîgembe)
Kwa sababu ya kuokoka kwake mhubiri anampenda ( kiswahili)

S68 Aûtemwa na kîbanga nûntû bwa kûiya (Kîîgembe)
Amekatwa kwa upanga kwa sababu ya wizi ( kiswahili)

S69 Nûntû bwa ûthongi bwake akûona mûkûrû (Kîîgembe)
Kwa sababu ya urembo wake amepata mume ( kiswahili)

S70 Kinya kwethîrwa nathomere na inya atakûrukîre (Kîîgembe)
Ijapokuwa alisoma kwa bidii hakupita mtihani ( Kiswahili)

S71 Akwoywa na mûrano kinya kwethîrwa atînkanya (Kîîgembe)
Ameolewa na harusi hata kama si mrembo ( Kiswahili)

S72 Kinya kwethîrwa arîmaa bwea mûno aûkûa (Kîîgembe)
Ijapokuwa alikuwa analima vizuri sana amekufa ( Kiswahili)

S73 Nî kenda tuthiria kûrima nomwanka twîthirwe twî na inya (Kîîgembe)
Ili tumalize kulima lazima tuwe na bidii ( kiswahili)

S74 Akûrumîre nî kenda ûthûra(Kîîgembe)
Alikutusi ili ukasirike (Kiswahili)

S75 Enderie munda nî kenda athoma (Kîîgembe)
Aliuza shamba ili asome (Kiswahili)

S76 Kethîrwa ûkarîma bwea ûaketha maketha yamaingi (Kîîgembe)
Ikiwa utalima vizuri utapata mazao mengi (Kiswahili)

S77 Andeni mpempe kethîrwa nibûkwenda wîta ûcetha (Kîîgembe)
Pandeni mahindi kama mnataka kwenda kucheza (Kiswahili)

S78 Kethîrwa ntongi ntîthîrwa ndî na mwekûrû ûmwe (Kîîgembe)
Kama ningekuwa tajiri singekuwa na bibi mmoja (Kiswahili)

S79 Kethîrwa ûkatiwa rikone ûrue (Kîîgembe)
Kama utaachwa jikoni upike (Kiswahili)

S80 Rîrîa akinya nkeja (Kîîgembe)
Atakapofika nitakuja (Kiswahili)

S81 Ntîî aûntuma ndûkene kûûra ithûngû îndi rîrîa kacoka nkeya kûkûona (Kîîgembe)
Mama amenituma dukani lakini nitakaporudi nitakuja kukuona (Kiswahili)

S82 Nîakûrima (Kîîgembe)
Analima (Kiswahili)

S83 Kaana kawîta ndûkene (Kîîgembe)
Mtoto ameenda dukani (Kiswahili)

S84 Mwiti  nî ûmûûme (Kîîgembe)
Mwiti ni mwerevu (Kiswahili)

S44  Ntîî awîta mundene. (Kîîgembe)
Mama ameenda shambani (Kiswahili)

S85 Arîtwa nîbakubuîthia kîerio (Kîîgembe)
Wanafunzi wanafanya mtihani (Kiswahili)

S86 Ntîî nîakûthambia nyûmba na mûtanocia akîcetha (Kîîgembe)
Mama anaosha nyumba na kaka anacheza (Kiswahili)

S87 Mwarîmû nî akûritana kîracine (Kîîgembe)
Mwalimu anafunza darasani  (Kiswahili)

S88 Kaana kaala kamûrîrîre biakûrîa bîvîngî mûno (Kîîgembe)
Mtoto yule alimlia vyakula vingi sana (Kiswahili)

S89 Mûrîmî ûrîa amûrîmîre mûtûrî oke munda yuonthe (Kîîgembe)
Mkulima yule alimlimia jirani yake shamba lote (Kiswahili)

S90 Tûkathambie kûîo (Kîîgembe)
Tukaoshe mapema (Kiswahili)

S91 Nî mbîtite mûranûne  (Kîîgembe)
Ninaenda harusini (Kiswahili)

S92 Mûrîmî narî na nthitangi. (Kîîgembe)
Mkulima alikuwa na  jembe (Kiswahili)

S93 Ntîî noo akurima mundane na mwarocia nîakûanda mpempe (Kîîgembe)
Mama angali analima shambani na dadangu anapanda mahindi. (Kiswahili)

S94 Muwatî  o mwana nîabatîri kûinîra mwaana (Kîîgembe)
Mlezi wa mtoto anapaswa kuimbia mtoto. (Kiswahili)

S95 Mûkoobi nîaîtue (Kîîgembe)
Mkopaji yu mgonjwa (Kiswahili)

S96 Mûrii jûî  kwa mûkoke (Kîîgembe)
Kamba iko kwa mkewe (Kiswahili)

S97 Ngarî eke îî naiti ya kîrîma (Kîîgembe)
Gari lake liko chini ya mlima. (Kiswahili)

S98 Mwarîmû ûû nîwe mwea mûno (Kîîgembe)
Mwalimu huyu ndiye mzuri sana . (Kiswahili)

S99 Mwarîmû akeya rûjû rûkîri (Kîîgembe)
Mwalimu atakuja kesho asubuhi  (Kiswahili)

S100 Mwîti nawîta mpaala mûno(Kîîgembe)
Msafiri anatembea polepole sana (Kiswahili)

S101 Kîerio kîu ni kîkîûmû mûno (Kîîgembe)
Mtihani huo ni mgumu sana (Kiswahili)

S102 Mwacie akûendua cibitari (Kîîgembe)
Mgonjwa amepelekwa hospitali (Kiswahili)

S103 Mûrûgi nîakûitanga nyama na kacîû (Kîîgembe)
Mpishi anakatakata nyama kwa kisu (Kiswahili)

S104 Mûiki ûmûthongi mûno aukuma kîûrûne (Kîîgembe)
Bi. harusi mrembo sana ameingia kanisani (Kiswahili)

S105 Mûrîtwa umwe aîna îûku rîa kûandîkîra kîerîo kîake (Kîîgembe)
Mwanafunzi mmoja ako na kitabu cha kuandikia mtihani wake. (Kiswahili)

S106 Ûria mûkûî ntîmwendete (Kîîgembe)
Yule mfupi simpendi. (Kiswahili)

S107 Mwarî ûmûkûrû mûno aîna nthoni (Kîîgembe)
Msichana mzee sana anaona haja (Kiswahili)

S108 Ûû mwamba nimbi eyerete naa kwetû? (Kîîgembe)
Huyu mwizi anakujia nini huku kwetu? (Kiswahili)

S109 Ûrîa mwarî ûmûraya mûno atîkethacia antû (Kîîgembe)
Yule msichana mrefu sana hasalimii watu (Kiswahili)

S110 Mwekûrû ûkû awîta ûtacia rûî (Kîîgembe)
Mke wako ameenda kuteka maji (Kiswahili)

S111 Nyûkwe endete susussu mûno Kîîgembe)
Mama yako anapenda umbea sana (Kiswahili)

S112 Mûkûrû ûyû mûraya nî wetû (Kîîgembe)
Mzee huyu mrefu ni wetu. (Kiswahili)

S113 Munda yûrîa ywetû nî yûandî mûngao
Shamba hilo letu limepandwa maharage.

S114 Mûrogi aûkua (Kîîgembe)
Mrogi amekufa (Kiswahili)

S115 Cukuru îkûruûrwa (Kîîgembe)
Shule imefunguliwa (Kiswahili)

S116 Nakûrîma na kûanda (Kîîgembe)
Analima na kupanda (Kiswahili)

S117 Mûritwa ûmûraya nîakûandika na mwarîmu akîritana (Kîîgembe)
Mwanafunzi mrefu anaandika na mwalimu anafunza (Kiswahili)

S118 Ntîî oke nî mwarîmu na îthe oke nî mûrîmi (Kîîgembe)
Mama yake ni mwalimu na baba yake ni mkulima (Kiswahili)

S119 Nîbendete kûrîma na kûanda (Kîîgembe)
Ninapenda kulima na kupanda (Kiswahili)

S120 Baîyîre na babunjia nyûmba na bayûkîa into bionthe (Kîîgembe)
Waliiba na kuvunja nyumba na kuchukua kila kitu (Kiswahili)

# KIAMBATISHO 3: KIBALI CHA UTAFITI

**THIS IS TO CERTIFY THAT:**
***MR. MUTWIRI FRED JOHN***
**of CHUKA UNIVERSITY, 109-60400**
**CHUKA,has been permitted to conduct**
**research in *Meru County***

**Permit No : NACOSTI/P/19/81045/28878**
**Date Of Issue : 3rd April,2019**
**Fee Recieved :Ksh 1000**



**on the topic: *MUUNDO WA SENTENSI YA KIIGEMBE: MTAZAMO WA EKSIBAA***

**for the period ending:**
***1st April,2020***

.............................
***Applicant's Signature***

.............................
***Director General***
***National Commission for Science, Technology & Innovation***

## KIAMBATISHO 4: BARUA YA KIBALI CHA UTAFITI

**NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION**

Telephone:+254-20-2213471,
2241349,3310571,2219420
Fax:+254-20-318245,318249
Email: dg@nacosti.go.ke
Website : www.nacosti.go.ke
When replying please quote

NACOSTI, Upper Kabete
Off Waiyaki Way
P.O. Box 30623-00100
NAIROBI-KENYA

Ref: No. **NACOSTI/P/19/81045/28878**

Date: **3rd April 2019**

Mutwiri Fred John
Chuka University,
P. O. Box 109-60400
**CHUKA.**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION**

Following your application for authority to carry out research on ***"Muundo wa sentensi ya kiigembe: Mtazamo wa Eksibaa"*** I am pleased to inform you that you have been authorized to undertake research in **Meru County** for the period ending **1st April, 2020.**

You are advised to report to **the County Commissioner and the County Director of Education, Meru County** before embarking on the research project.

Kindly note that, as an applicant who has been licensed under the Science, Technology and Innovation Act, 2013 to conduct research in Kenya, you shall deposit **a copy** of the final research report to the Commission within **one year** of completion. The soft copy of the same should be submitted through the Online Research Information System.


**DR. STEPHEN K. KIBIRU, PhD.**
**FOR: DIRECTOR-GENERAL/CEO**

Copy to:

The County Commissioner
Meru County.

The County Director of Education
Meru County.

**KIAMBATISHO 5: RAMANI YA MAENEO TAWALA YA IGEMBE**




ASILI: Meru County Intergrated Development Plan.